# Nipashe

Jumanne Januari 29, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579827

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mahakama ilivyomwachia huru bosi mkuu wa NIDA

UKURASA 3




A 13

# Tril. 1.5/-, CAG 'moto' bungeni



• **Wabunge** pia kujadili hatima Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 26

### POLISI YAUA WANANE TUHUMA ZA UJAMBAZI

JESHI la Polisi mkoani Kigoma, limesema limeua watu wanane kwa tuhuma za ujambazi. Kamanda wa Polisi mkoani Kigoma, Martin Ottieno...



Baadhi ya wachuuzi wa samaki wakisubiri kitoweo hicho, bila mafanikio katika soko la Feri, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuadimika kutokana na mgomo wa wavuvi, uliotokana na madai ya kukamatwa kwa nyavu zao na kunyanyaswa na askari wa doria wawapo baharini. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Lukuvi ataka majina ya maofisa ardhi kikwazo hati

UKURASA 3

## Hakimu kortini tuhuma za rushwa ya 710,000/-

• **Yadaiwa** kutumwa kwa Tigo Pesa- *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** SIMBA 20 WAIFUATA AL AHLY KWA HASIRA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Tril. 1.5/-, CAG 'moto' bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MKUTANO wa 14 wa Bunge la 11 unaanza leo jijini Dodoma, huku mambo matatu yakitarajiwa kulitikisa katika mijadala ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Mambo hayo ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018 na taarifa ya shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ambayo inatarajiwa kuliibua tena sakata la kutoonekana kwa matumizi ya Sh. trilioni 1.5 katika taarifa za hesabu za serikali.

Sakata la kutoonekana kwa matumizi ya Sh. trilioni 1.5 liliibuka wakati wa Bunge la Bajeti, siku moja baada ya kuwasilishwa kwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2016/17.

Jambo la tatu linalotarajiwa kutikisa mkutano huo wa Bunge, ni taarifa ya shughuli za Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ambayo inatarajiwa kutoa mapendekezo yake kuhusu hatima ya CAG, Prof. Mussa Assad, baada ya kumhoji hivi karibuni.

Prof. Assad alihojiwa na kamati hiyo wiki iliyopita kutokana na tuhuma za kulidhalilisha Bunge baada ya kutoa kauli Marekani kuwa anafikiri Bunge ni dhaifu.

Kamati hiyo pia ilimhoji Mbunge wa Kawe, Halima Mdee (Chadema), Januari 22, mwaka huu, kutokana na tuhuma dhidi ya Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango huyo kuwa aliunga mkono kauli ya CAG kuwa Bunge ni dhaifu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Ofisi ya Bunge, masuala mengine yatakayojadiliwa katika mkutano huo, ni taarifa za kamati 15 za kudumu za Bunge ambazo zitawasilisha taarifa zake za mwaka kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016.

Mkutano huo wa wiki mbili pia ni mahususi kwa ajili ya uwasilishaji wa miswada ya serikali na kuwapa fursa wabunge kuzungumzia masuala yanayoendelea nchini, iwapo yatajitokeza.

Mbali na muswada kuhusu marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, miswada mingine inayotarajiwa kuwasilishwa ni ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018, Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018, Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, Namba 4 wa Mwaka 2018.

**KIAPO**

Katika mkutano huo, wabunge watashuhudia kiapo cha uaminifu cha Mbunge Mteule wa Jimbo la Temeke (CCM), Abdallah Mtolea, aliyepita bila kupingwa Desemba 20, mwaka jana, baada ya wagombea waliokuwa wamechukua fomu kuwania nafasi hiyo kukosa sifa.

Uchaguzi wa Temeke ulifanyika, baada ya Mtolea aliyekuwa Mbunge kwa tiketi ya CUF hadi Novemba 2018, kutangaza mchana kujivua uanachama wa chama hicho na baadaye jioni kujiunga na CCM na kupitishwa kuwania ubunge.



Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Kijazi, akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, sehemu ya awamu ya pili ya vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo vilivyotolewa na Rais John Magufuli Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Katibu Mkuu Tamisemi, Mhandisi John Nyamhanga (katikati) na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Vijana), Andrew Massawe. **PICHA: IKULU**

# Majadiliano bomba la mafuta Juni

**Na Mwandishi,** KAMPALA

SERIKALI za Uganda na Tanzania zimekubaliana kuwa majadiliano yanayohusu utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Tanga yatakamilike ifikapo Juni mwaka huu, ili kuendelea na hatua ya ujenzi wa bomba hilo.

Hayo yalielezwa kwa nyakati tofauti jijini Kampala na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani na Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini wa Uganda, Irene Muloni, baada ya kufanyika kikao cha mawaziri wa nchi hizo wanaohusika na mradi huo.

"Kwa ujumla tumejipanga kuwa majadiliano yote ya mradi na maandalizi mengine ya mradi kati ya pande zote mbili yakamilike Juni, ili ujenzi wa mradi uanze mwezi Juni na tunataka kukamilisha mradi huu ndani ya miezi 36, baada ya ujenzi kuanza," alisema Dk. Medard Kalemani.

Dk. Kalemani alisema mradi ulishaanza kutekelezwa kwa kufanyika kazi za awali ikiwamo tathmini ya mazingira ambayo kwa upande wa Tanzania imekamilika na upatikanaji wa eneo kutapojengwa matangi matano yatakayohifadhi mafuta lita 500,000 kila moja mkoani Tanga, ambapo taratibu za ujenzi zinaendelea.

Aliongeza kuwa mradi huo unatekelezwa hatua kwa hatua, hivyo kuna kazi zinazoendelea kufanyika wakati majadiliano yakiendelea ikiwamo kazi za utafiti wa kijiokemia, kijiolojia na kijiotekniko na kuna kazi zitakazofuata baada ya majadiliano kukamilika.

Vilevile alisema baada ya kumalizika kwa majadiliano kati ya serikali ya Tanzania na Uganda, hatua itakayofuata ni majadiliano ya kimkataba kati ya serikali ya Tanzania na wawekezaji wa mradi ambao ni kampuni ya Total E&P ya Ufaransa, Tullow Oil ya Uingereza na CNOOC ya China na pia serikali ya Uganda itafanya majadiliano husika na wawekezaji hao.

Akizungumzia kikao hicho, Dk. Kalemani, alisema baada ya kusainiwa kwa mkataba wa mradi huo mwaka 2017, kulikuwa na masuala mengi ya kujadili, lakini katika vikao mbalimbali vya ngazi ya mawaziri, wameendelea kukubaliana katika masuala mengi yatakayowezesha mradi kusonga mbele.

Kwa upande wake, Waziri Muloni alisema mazungumzo kati ya pande hizo mbili yamefanyika vizuri na yale waliyokubaliana, kila pande unaenda kuyawasilisha katika uongozi wa juu wa nchi kabla ya kuendelea na hatua nyingine za majadiliano.

# Hakimu kortini tuhuma za kupokea rushwa 710,000/-

**Na Enock Charles**

HAKIMU wa Mahakama ya Mwanzo ya Ukonga jijini Dar es Salaam, Dickson Mwasenga (46), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala na kusomewa mashtaka matatu ya kupokea rushwa ya jumla ya Sh. 710,000.

Akisomewa mashtaka hayo jana na Mwendesha Mashtaka wa Mahakama hiyo, Devota Mihayo, mbele ya Hakimu Samuel Obasi, ilidaiwa mshtakiwa alipokea rushwa hiyo ili kufanya upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017 iliyokuwa inamkabili ofisa wa Benki ya CRDB, Ngomoi Mmbaga (42).

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa Februari 22, 2017, mshtakiwa alipokea Sh. 210,000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga kupitia Tigo Pesa ili kumpa upendeleo ofisa huyo wa benki katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Aprili 14, 2017, mshtakiwa alipokea Sh. 100,000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga, kupitia Tigo Pesa ili kumpa upendeleo ofisa huyo wa benki katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa Mei Mosi, 2017, mshtakiwa alipokea Sh. 400,000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga kupitia Tigo Pesa ili kumpa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Mihayo alidai mahakamani hapo kuwa, kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 Kifungu 15(1) ya Mwaka 2017.

Mwendesha mashtaka huyo pia alisoma mashtaka matatu dhidi ya Mmbaga ya kutoa rushwa, ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017 katika mahakama hiyo ya mwanzo.

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, Februari 22, 2017, mshtakiwa Ngomoi Mmbaga alituma Sh. 210,000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia Tigo Pesa, ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Aprili 14, 2017, mshtakiwa huyo alituma Sh. 100,000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia Tigo Pesa, ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa Mei Mosi, 2017, mshtakiwa Ngomoi Mmbaga, alituma Sh. 400,000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia Tigo Pesa ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Mihayo alidai mahakamani hapo kuwa, kwa kufanya hivyo ni kinyume cha Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2017.

Washtakiwa wote walikana mashtaka na kesi hiyo kupangwa kutajwa tena Februari 19, mwaka huu.

**KUHAMIA KINYEREZI**

Katika hatua nyingine, Mahakama ya Wilaya ya Ilala inatarajiwa kuhamishiwa katika jengo jipya la mahakama lililoko eneo la Kinyerezi jijini Dar es Salaam kuanzia Februari 11, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa kwenye kuta za mahakama hiyo, mashauri yote yanayoendelea na yatakayofunguliwa, yatasikilizwa katika jengo jipya la Kinyerezi kuanzia tarehe hiyo.

"Wananchi na wadau wote wa mahakama mnajulishwa kuwa, mashauri yote yanayoendelea na yatakayofunguliwa yatasikilizwa katika jengo la Kinyerezi," inaelezwa katika taarifa hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Mahakama yamfutia kesi bosi Nida

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewafutia kesi na kuwaachia huru aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu na wenzake sita, baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kusema hana nia ya kuendelea na kesi dhidi yao.

Walikuwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.16.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, baada ya upande wa Jamhuri kuwasilisha ombi la DPP la kuwaondolea washtakiwa hao mashtaka. Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali, Simon Wankyo na Leonard Swai.

Wankyo alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, (Jaji Mteule) Willibard Mashauri.

Hata hivyo, DPP ameomba kuwaondolea washtakiwa mashtaka yanayowakabili kwa kuwa hana nia ya kuendelea kuwashtaki chini ya kifungu cha 91 kifungu kidogo cha (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20 iliyofanyiwa marekebisho 2002.

Upande wa utetezi ulidai kuwa hauna pingamizi kuhusu washtakiwa kuondolewa mashtaka.

Hakimu Mtega alisema kwa kuwa pande zote zimeridhia, mahakama yake haina pingamizi imekubali kuwaondolea washtakiwa mashtaka hayo chini ya kifungu cha 91 kidogo cha (1).

Mbali ya Maimu, washtakiwa wengine ni Meneja Biashara wa NIDA, Avelin Momburi na Mkurugenzi wa Tehema, Joseph Makani. Pia Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kutumia madaraka vibaya, kula njama, kutumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. 1,169,352,931.

Ilidaiwa kwenye shtaka la kwanza Maimu na Mwakatumbula kati ya Januari 15 hadi 19, 2010 katika makao makuu ya NIDA wilayani Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam,

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na wabunge wa viti maalum, Amina Makilagi (katikati) na Fatma Toufiq, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## Magogo mikononi mwa Takukuru

**Na Khadija Kalili,** IKWIRIRI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Pwani, kupitia Kituo Maalumu cha Ikwiriri imekamata magogo ya miti aina ya mninga 20 yakiwa yamefichwa kwenye nyumba, yenye thamani ya Sh. 4,370, 448.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Sadiki Nombo, alisema kuwa taarifa hiyo ilitolewa na mwananchi mmoja (jina linahifadhiwa) na baada ya kupata taarifa hizo Takukuru ilifanya uchunguzi wa haraka ambao ulifanikisha kukamatwa kwa mfanyabiashara mmoja aliyekutwa na magogo hayo.

Alisema pia imebainika kuwapo kwa mtandao mkubwa unaosaidia kufanikisha utoroshaji wa mazao ya misitu kwa njia ya rushwa huku wakisababisha serikali kukosa mapato yatokanayo na uvunaji, usafirishaji wa mazao ya misitu.

## Lukuvi ataka majina maofisa ardhi wanaochelewesha hati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewaagiza wakuu wa idara za ardhi kwenye halmashauri zote nchini kuwapatia mara moja wananchi waliocheleweshewa hati miliki za ardhi ili waanze kulipia kodi.

Aidha, ameagiza maofisa hao kumpelekea orodha ya maofisa ardhi waliochelewesha hati hizo, ili wachukuliwe hatua za kisheria, akisema kuwa vitendo hivyo ni sawa na makosa ya uhujumu uchumi kutokana na wenye hati hizo kutolipa kodi.

Lukuvi alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kushtukiza katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kutembelea ofisi ya kutunza kumbukumbu za Idara ya Ardhi, ambapo alibaini uozo wa watendaji wa idara hiyo.

Alisema kwenye ofisi hiyo alibaini baadhi ya wananchi kuomba kumilikishwa ardhi kwa zaidi ya miaka 10, lakini maombi yao hayajafanyiwa kazi na wananchi hao hawajawahi kulipa kodi kama sheria ya ardhi inavyoelekeza.

"Kuna mtu hapa naona alishaomba hati miliki tangu mwaka 2011 na alilipa Shilingi milioni 1.5, sasa hapa kuna mafaili zaidi ya 1,000 nataka niletewe majina ya watu waliochelewesha mafaili haya ili tuwashughulikie hata kama wapo nje ya Mbeya," aliagiza Lukuvi.

Aidha, alisema ucheleweshaji wa hati hizo ni viashiria vya uwapo wa vitendo vya rushwa katika ofisi hiyo, hivyo akaagiza hati zote zilizocheleweshwa zitolewe na wananchi waendelee kulipia maeneo yao.

Waziri Lukuvi alisisitiza kuwa idara za ardhi kwenye halmashauri zote nchini ni tatizo kwa maelezo kuwa matatizo yote ya ardhi yanayolitesa taifa kwa sasa yamesababishwa na maofisa ardhi hao.

Vilevile, aliwaagiza wakurugenzi wote wa halmashauri zote nchini kuzisimamia ofisi za ardhi ili zifanye kazi ambazo zinaendana na matakwa ya halmashauri zao ili kuondoa makandokando yanayojitokeza.

Awali akitoa taarifa ya utendaji kazi wa ofisi hiyo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango miji wa Jiji la Mbeya, Emeliana Kihunrwa, alisema kwa sasa viwanja vilivyopimwa ndani ya jiji hilo ni 26,500, lakini vilivyotolewa hati ni 23,000.

Hata hivyo alisema kuna mitaa 34 ambayo wameiainisha kwa ajili ya kuanza kupimwa na kumilikishwa wananchi ili kuwawezesha kulipa kodi za pango la ardhi.

Alisema wameunda tume ya maofisa ardhi wanne kwa ajili ya kupitia mafaili yote ya watu walioomba hati na kubainisha changamoto mbalimbali ili zitatuliwe na watu hao wapewe hati zao.

"Kwa sasa tumeanza kushughulikia changamoto hii kwa kuunda tume ya kupitia mafaili yote na kuhakikishia kuwa mpaka kufikia Machi mwaka huu watu wote walioomba hati watapatiwa hati zao," alisema Kihunrwa.


**MPOKI AND ASSOCIATES ADVOCATES**

**CORRECTION ON ADVERTISEMENT ISSUED ON 25TH JANUARY 2019 NOTICE OF SALE**

**ALL THAT LANDED PROPERTY KNOWN AS PLOT NO 20 REGENT ESTATE DAR ES SALAAM CITY REGISTERED UNDER CT NO 52464 LO NO 191030 REGISTERED IN THE NAME OF ABLA ESTATE DEVELOPERS AND AGENCY COMPANY LIMITED**

1. **NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT,** under power contained in the mortgage deed dated 25th day of June 2008 in favour of CRDB BANK PLC and every other power enabling me to do so, **I MPALE KABA MPOKI, OF MPOKI AND ASSOCIATES, ADVOCATES** on behalf of the lender hereby advertise the sale of the captioned property owned by ABLA ESTATE DEVELOPERS AND AGENCY COMPANY LIMITED.

2. THE property is built on a plot with a title deed issued on the 1st day April 2001 for a term of 33 Years, the title has an unexpired term of 16 years and the plot measures about 28250 square meters.
   Situate on the property is a 6 storey 3 Star running hotel, along Bagamoyo Road, about 11.7 kilometres from Dar es Salaam Airport, close to Makumbusho Village Museum, the hotel is close to several offices, historical centres and business premises.
   The Hotel known as ABLA HOTEL APARTMENT is a luxurious Hotel apartment with fully furnished one, two and three bedroom apartments with a fully equipped kitchen making an ideal destination for families or business travelers. The Hotel has a modern fitness centre, a large swimming pool and a sauna.
   There is also a spacious conference hall with modern facilities a big parking place is also available.

3. INTERESTED MEMBERS OF THE PUBLIC ARE INVITED to submit bids for the purchase of the property.

4. Bids in sealed envelopes clearly marked "BID FOR THE PURCHASE OF PROPERTY ON PLOT 20 REGENT ESTATE KINONDONI DAR ES SALAAM", indicating the offer for the property with full address of the bidder shown and the same should be submitted so as to reach the undersigned on the address below before 16.00 hours on the 5th February 2019, Bids shall be opened on the 5th February 2019 ay 16.30 hours at the office mentioned below. Bidders are invited to attend during the event if they so wish.

5. Bidders should note that the information supplied herein is without liability to the seller as to its correctness. Independent valuation and inspection of the property is highly recommended.

6. The property is sold in a condition as it is, the seller nor sellers agent warrant the condition of the property, the seller agrees to permit buyer or buyers representatives reasonable access to the premises to complete the said inspection

7. The seller shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all.

8. It is a condition of the bid that bidders submit their bids accompanied by Bankers cheque in favor of CRDB BANK PLC of an amount equivalent to 10% of the bid price. For a successful bidder this amount shall be treated as advance payment. Unsuccessful bidders will have their bid commitment refunded in full without any deductions.

9. The successful bidder shall be bound to make a 25% down payment on the offer price within 4 days of the date of the award; and the balance shall be paid within 14 days thereafter

   In the event the balance is not paid within 14 days the seller shall forfeit the down payment and the next highest bidder shall be awarded the option to purchase.

10. Members of the public and or bidders who are desirous of viewing and or inspecting the property may do so subject to the appointment and prior consent of the seller agent on the address below:
    **ISSA BENDERA,**
    **COMRADE AUCTION MART,**
    **P.O. BOX 61508,**
    **DAR ES SALAAM,**
    **TANZANIA.**
    **PHONE NO 0758-212728**
    **0623-212728**

11. Bids mentioned in paragraph 4 hereinabove should be addressed to the address below:

    **MPALE KABA MPOKI**
    **MPOKI AND ASSOCIATES, ADVOCATES,**
    **NO 4 REGENT STREET, OFF CHATO STREET,**
    **NEAR SUNRISE PRIMARY SCHOOL,**
    **P.O. BOX 14232,**
    **DAR ES SALAAM.**
    **PHONE: 0773-187777**
    **0715-187777**

215029002

## KAHAMA TOWN COUNCIL

**Bid No LGA/155/2018/2019/WSDPII/02 –**

**RE ADVERTISED**

**For**

**EXTENSION OF THE WATER TRANSMISSION PIPELINE AND DISTRIBUTION NETWORK AT NGOGWA-KITWANA VILLAGES**

**Invitation for Bids**

**Date: 29/01/2019**

1. This Invitation for Bids follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in Development Business,
2. The Kahama Town Council has received financing from Development Partners and the Government of United Republic of Tanzania towards the cost of the **Extension of the water transmission pipeline and distribution Network at Ngogwa-Kitwana Villages** and intends to apply part of the portion of the funds to cover eligible payments under the contract for which this invitation for Bid is issued.
3. The Kahama Town Council now invites sealed bids from **only** eligible and qualified Piped system and Civil works contractors registered with CRB in class **Two (2) and above for carrying out the Extension of the water transmission pipeline and distribution Network at Ngogwa-Kitwana Villages** with the following activities: -
   - Excavate, supply of Steel and PVC pipes and lay in trenches and backfill pipes for transmission line with total length of 14,897m.
   - Excavate, supply of HDPE and PVC pipes and lay in trenches and backfill pipes for Distribution networks line with total length of 7,568m.
   - Construction of storage Tanks, On the ground tank and raised tank
   - Supply and install valves, fittings and specials.
   - Excavate for and construct pipeline manholes with internal diameters 1,000mm x 800mm x 1,000mm
   - Excavate for and construct pipeline thrust blocks and markers, air valves, Washouts and gate valves markers
   - Construct two taps domestic points with soak way pits.
   - Construct Cattle troughs with all fittings
4. Bidding will be conducted through the National Competitive Bidding (NCB) procedures specified in the Public Procurement Act, No. 7 of 2011and Public Procurement (Amendment) Act of 2016 and the Public Procurement (Goods, Works, Non Consultancy Service and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations – Government Notice No. 446 of 2013 and Public Procurement (Amendment) Regulation of 2016 and are open to all eligible bidders.
5. Interested eligible Bidders may obtain further information from and inspect the Bidding Documents at the office of the **Secretary of Tender Board, Kahama Town Council, P. O. Box 472 - Kahama,** Tanzania, From 7:30 am to 3:30 pm Monday to Friday inclusive except on public holidays.
6. A complete set of Bidding Documents in English, in hard copy and additional sets may be purchased by interested Bidders on the submission of a written application to the address given under paragraph 5 above and upon payment of a non-refundable fee of TZS 100,000 (Tanzanian shilling one hundred thousand) or its equivalent. Those who participated in the previous tender before this re advertisement will only pay TZS 50,000.00. Payment should either be by Cash, Banker's Draft, or Banker's Cheque, payable to the **Town Director, Kahama Town Council, P. O. Box 472, - Kahama.**
7. All bids in one original plus Two copies properly filled in, and enclosed in plain envelopes written on top of that envelope **Extension of the Water Transmission Pipeline and Distribution Network at Ngogwa-Kitwana Villages TENDER NO: - LGA/155/2018/19/WSDPII/W/02** must be delivered to the address, **Secretary of Tender Board, Kahama Town Council, P.O BOX 472 - KAHAMA at or before 11:00 local times on Tuesday , 12/02/2019 Bids** will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Bidders' representatives who choose to attend in the opening ceremony at Kahama **Town Council Hall,** allocated at **Boma Road in Kahama Town** on their own cost.
8. Late bids, portion of bids, electronic bids, and bids not received, bids not opened at the bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Anderson D. Msumba**
**TOWN DIRECTOR**
**KAHAMA**


# Waliovamia hifadhi waamriwa kuondoka

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka wananchi wote wanaovamia maeneo ya hifadhi kuacha mara moja na kurejea katika maeneo yao ya awali.

Aliyetoa agizo hilo ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, huku akikemea vikali vitendo vya baadhi ya wananchi wanaovamia maeneo ya hifadhi na kuingiza mifugo pamoja na kupanda mazao kinyume cha sheria na kuwataka kusubiri hadi hapo wizara husika zitakapolipatia ufumbuzi suala la vijiji na vitongoji 366 vilivyoainishwa kuwapo katika maeneo ya hifadhi kulingana na taratibu.

Naibu Waziri Kanyasu alisisitiza kuwa yeyote atakayekwenda kinyume cha agizo hili atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Hivi karibuni, kumekuwapo na taarifa za uvamizi wa makundi ya mifugo ndani ya mapori ya akiba na misitu ya hifadhi.

Zipo taarifa kutoka maeneo mbalimbali kama mapori tengefu, mapori ya akiba na misitu ya hifadhi kuwa kuna wananchi wanaswaga mifugo na kuingiza ndani ya hifadhi.

Aidha, kumekuwa na taarifa za maeneo oevu kuvamiwa na baadhi ya wananchi.

Naibu Waziri Kanyasu aliziagiza taasisi husika za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro, (NCAA), Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuendelea kuzuia uvamizi huo na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wavamizi bila ya kisingizio chochote.

Onyo hili limetolewa, kufuatia baadhi ya wananchi kuanza kuvamia maeneo ya hifadhi kwa kuingiza mifugo na kupanda mazao kufuatia kutokuelewa vema maagizo yaliyotolewa na Rais John Magufuli Januari, mwaka huu na kuanza kuvamia maeneo ya hifadhi badala ya kubaki katika maeneo waliyomo wakati wakisubiria ufumbuzi wa migogoro.

Aidha, Kanyasu alielekeza kuwa si maeneo yote 366 yatakayotolewa kwa wananchi.

Januari 15, mwaka huu, Rais Magufuli, aliziagiza wizara zote zinazohusika (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Rais Ikulu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi) kusitisha mara moja kuviondoa vijiji na vitongoji vinavyodaiwa kuwepo katika maeneo ya hifadhi na kuzitaka wizara zote zinazohusika kukutana iii kubainisha na kuanza mchakato wa kurasimisha maeneo ya vijiji na vitongoji hivyo.

Kanyasu alifafanua kuwa, agizo la Rais Magufuli, halikumaanisha kuwa sasa wananchi wanaruhusiwa kuvamia, kuingiza mifugo na kulima katika maeneo ya hifadhi.


## KAHAMA TOWN COUNCIL

**Bid No LGA/155/2018/2019/C/03**

**Consultancy services for Detailed Engineering Design, Preparation of Tender Documents, Cost Estimates, Environmental and Social Impact Assessment(ESIA) and Revenues Enhencement Strategies at Zongomera Investment Area in Kahama Town Council)**

**Expression of Interest**

**Date:29/01/2019**

1. This invitation for expression of interest follows the General Procurement Notice (GPN) which appeared in [insert media] Issue no. [Insert the issue No.] dated [insert dates of issue of GPN].
2. The Government of the United Republic of Tanzania has set aside funds for the operation of the Kahama Town Council during the financial year 2018/2019. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for the Consultancy services for Detailed Engineering Design, Preparation of Tender Documents, cost Estimates, Environmental and Social Impact Assessment(ESIA), and Revenues Enhancement Strategies at Zongomera Investment Area in Kahama Town Council)
3. The Kahama Town Council now invites eligible consultants firms to indicate their interest in providing the services as shown above for the implementation period of sixty (60) days.
4. Interested consultants firms must provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting consultant's profile, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc. Consultants may associate to enhance their qualifications.
5. A consultant will be selected in accordance with the procedures set out in the Public Procurement Act No. 7 of 2011 and the Public Procurement Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 (hereinafter called Procurement Regulations).
6. Selection will be conducted through the Quality and Cost based selection procedures specified in the Public Procurement Regulations.
7. Interested eligible consultants may obtain further information from the office of the **Secretary, Kahama Town Council Tender Board, P. O. Box 472 Kahama. Email: td@kahamatc.go.tz from 7.30am to 3.30pm** on Monday to Friday inclusive except on public holidays.
8. Expressions of Interest (EoI) must be delivered to Kahama Town Council Offices located at Boma road at or before 11 on 12/02/2019.
9. Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Anderson D. Msumba**
**TOWN DIRECTOR**
**KAHAMA TOWN COUNCIL**

215028802


# Kodi ya pango kwa taasisi za dini yafutwa

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imefuta kodi ya pango la ardhi kwa taasisi na madhehebu ya dini kuanzia mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Hatua hiyo ilitangazwa Jumapili na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, jijini Mbeya, wakati wa ibada ya kuwaweka wakfu viongozi wa Jumuiya Kuu ya Kanisa la Kibaptisti Tanzania (BCT).

Lukuvi alisema Rais John Magufuli ameiagiza wizara hiyo kutoyatoza kodi madhehebu ya dini kwa sehemu ambazo zimeandaliwa kwa ajili ya kufanyia ibada.

"Rais ameagiza kuanzia Julai Mosi mwaka huu wa fedha, madhehebu ya dini yasilipe kodi ya ardhi kwa maeneo ambayo huduma za maombi na ibada zinatolewa."

Hata hivyo, alisema: "Msamaha huu hauhusu maeneo ambayo kuna miradi ya kuingiza fedha ambayo tunajua madhehebu mengi yameanzisha."

Lukuvi alifafanua kuwa maagizo hayo tayari yametolewa kwa makamishna wa ardhi wa kanda na mikoa pamoja na maofisa ardhi wa majiji, manispaa na halmashauri nchi nzima.

Pia Lukuvi alitoa nafasi ya kukutana na viongozi wa dini ambao wana migogoro ya ardhi kwenye maeneo ambayo wanatoa huduma.

"Najua kuna migogoro mingi kwenye maeneo ambayo mnatoa huduma, hivyo nawakaribisha ofisini kwangu Dodoma na kama migogoro itakuwa mikubwa nitafika mpaka eneo la mgogoro," alisema Lukuvi na kuongeza:

"Wizara yangu imepewa jukumu la kutatua migogoro ya ardhi kabla ya mwaka 2020 na tusipotatua migogoro ya dini inaweza kusababisha uvunjifu wa amani nchini, hivyo hatutaki kuifuga migogoro iliyopo."

Awali, Askofu wa Kanisa la Baptisti nchini, Arnold Manase, alisema kanisa lake ni moja ya madhehebu yanayoongoza kuwa na migogoro ya ardhi na baadhi ya waumini wa kanisa hilo.

"Kwa kuwa waziri mwenye dhamana upo, naomba nafasi nije ofisini kwako nikueleze migogoro iliyopo ndani ya kanisa langu, ili uangalie namna ya kuitatua, maana migogoro imekithiri mpaka kufikia hatua ya kujenga makundi miongoni mwa waumini," alisema Manase.

TANGAZO

# Maeneo muhimu yanayohitaji marekebisho katika Mswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa, 2018

**1) Mamlaka yaliyopitiliza anayopewa Msajili wa Vyama vya Siasa kwenye masuala ya ndani ya chama.**

Mswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa, 2018 unabadilisha jukumu la msingi la Msajili wa vyama vya siasa kutoka kuwa “msajili” mpaka kuwa “mdhibiti”. Mamlaka makubwa anayopewa Msajili katika Mswada huu yanafanya utekelezaji wa majukumu yake kwenda kinyume na misingi ya demokrasia na Katiba. Mswada unampatia Msajili mamlaka makubwa ya kudai taarifa – orodha ya wanachama, taarifa ya fedha ya chama, na “taarifa yoyote itakayohitajika.” Zaidi, ikiwemo mamlaka ya kuingilia masuala ya ndani ya uongozi wa chama, kama orodha ya wanachama, kuweka vikwazo kwenye katiba za vyama, na masuala ya kinidhamu ya ndani ya chama.

Kwa kuzingatia kuwa msajili anateuliwa na (na anaweza kuondolewa na) Rais, ambaye ni mwenyekiti wa chama tawala, hii inaleta mgongano wa kimaslahi. Msajili hapaswi kuwa na mamlaka kwenye masuala yanayohusiana na taarifa nyeti au mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama, kazi yake ijikite katika kanuni za usajili wa chama.

**Mapendekezo**

- Ili kuepuka mgongano wa maslahi, Msajili anapaswa kuandaa miongozo kwa vyama vya siasa kusimaia shughuli zake za utendaji bila yeye (Msajili) kuingilia. Kifungu cha 4 (5)(e) kinapaswa kubadilishwa kumuondolea Msajili mamlaka ya kuingilia mapato na matumizi ya rasilimali za vyama vya siasa badala yake aandae miongozo itakayowezesha vyama kujisimamia na kuwajibika bila yeye kuingilia.
- Rekebisha kifungu cha 5B kumuondolea mamlaka Msajili kuomba taarifa kwa viongozi au wanachama wa vyama vya siasa badala yake aombe taarifa kwa vyama kama taasisi sambamba na kufuata mapendekezo katika kutekeleza adhabu hizi:
- Kumuondelea kinga ya kushtakiwa Msajili na maafisa wote katika ofisi ya Msajili kama ilivyopendekezwa katika kifungu cha 6.
- Mamlaka ya Msajili yajikite katika (a) kusajili chama (b) kusajili viongozi wa kitaifa wa vyama na kutoa adhabu kwa kuzingatia mapendekezo haya:
- Msajili anaweza kushauri vyama kubadilisha katiba zao lakini si kuvilazimisha. Utoaji wa adhabu unapaswa kufuata mchakato ulioanishwa.
- Taarifa za vyama zinazoiwasilishwa kwa Msajili bila kuvunja sheria nyingine au haki za kikatiba. Adhabu zitolewe kwa kuzingatia mapendekezo haya:
- Kinga zote zinazotolewa katika kifungu 19(2) na 19(3) cha Sheria ya sasa zijumuishwe kwenye kifungu cha 19A
- Ondoa mabadiliko 22(a) na (b)
- Vyama vya siasa vifanyiwe ukaguzi wa mapato na matumizi kwa mwaka na maamuzi yoyote ya kusitisha fedha zao za ruzuku yafanyike kwa kuzingatia ushahidi na yapendekezwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Ondoa kabisa kifungu cha 21E kinachopendekezwa.

2) Mabadiliko yazingatie kuwa sheria haijengi hofu au kupendekeza adhabu kali

Kwa kiasi kikubwa Mswada unafanya marejeo kwenye adhabu, hii inajitokeza karibu kwenye marekebisho yote. Suaal hili linajenga hali ya hofu wakati mtu anaposoma muswada, kwamba upo uwezekano wa kufanya kosa fulani.

Vilevile, adhabu zilizowekwa kwa makosa mengi hasa makosa ya kiutendaji hazilandani na makosa. Hazizingatii misingi ya kisheria, hususani misingi ya sheria za utawala na makosa ya kanuni za adhabu.

Ingawa vyama vya siasa vinapaswa kudhibitiwa, lakini vilevile, katika demokrasia changa, vinahitaji kulelewa. Kuanzisha mchakato wa kutoa maonyo, adhabu kali na kutokuoneshwa wazi utofauti uliopo kati ya makosa binafsi na makosa ya taasisi ni suala la kutazamwa kwa umakini.

**Mapendekezo**

- Makosa ya jinai yasirudiwe katika Sheria hii kwani tayari yapo kwenye Sheria ya Kanuni ya Adhabu.
- Ondoa marejeo yoyote ya adhabu kutoka kwenye sehemu kuu ya maelezo ya sheria na zielezewe kwenye kifungu cha nyongeza kwenye sheria na kuitwa: Makosa na Adhabu. Ama weka mchakato ulioelezewa hapo chini kwenye kila kifungu ukielezea kosa na adhabu husika. Hii ikihusisha vifungu 5A(4)(6); 5B(2)(3)(5); 8C(3)(4), 8D(4); 8E(3); 12C(4); 19A(3); 21D(1)(2)(3)(4).
- Makosa ya kiutendaji, kama yalivyoainishwa katika sheria hii yanapaswa kufuata mchakato huu:
  - Kwa kiwango cha chini, majibu yanatakiwa kutolewa baada ya barua tatu za onyo kutumwa.
  - Kama hakuna majibu yaliyopokelewa au hatua iliyochukuliwa kurekebisha kosa, chama ama taasisi inaweza kutozwa faini ambayo inayoendana na uhalisia.
  - Kusimamishwa kwa muda, iwapo yafuatayo yamefikiwa: notisi ya maandishi ya kutaka kukisimamisha chama ikiwemo maelezo ya kutosha kuhusu kosa lililofanyika, na nakala za barua zilizoandikwa na Msajili kukipa chama taarifa kuhusu makosa yake.
  - Kufuta usajili iwapo makosa yameendelea kutendeka baada ya kipindi cha kusimamishwa kwisha, au pale inapotokea kutoridhishwa na majibu ya suala lililosababisha kusimamishwa.
  - Uamuzi wa Msajili kufuta usajili wa chama uhusishe Baraza la Vyama vya Siasa na kuwepo na uwezo wa kukata rufaa mahakamani.

**3) Kukandamizwa kwa haki ya uhuru wa kujieleza**

Marekebisho yaliyoainishwa kwenye Mswada yamegusa maeneo matatu yanayoingilia haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza . Kwanza kuna katazo jipya kwa vyama vinavyofanya kazi kama vikundi vya uhamasishaji au vikundi vya harakati, vikundi hivyo vinaelezwa kuwa ni “vikundi vinavyoshawishi mitazamo ya wananchi au matendo ya serikali.” Kazi hizo ni msingi muhimu wa kazi za chama chochote cha siasa na hazipaswi kuzuiwa. Pili, muswada umeainisha kuwa ni kosa kwa chama “kutoa kauli ambazo si za kweli” Kimsingi kifungu hiki kinatishia demokrasia na haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza kwani ni ngumu kuainisha upi ni ukweli na upi ni uongo hasa katika masuala yenye utata hasa inapotokea mvutano wa kimtazamo au itikadi za kisiasa. Vifungu kama hivi pia vinaweza kusababisha kukosekana kwa usawa katika utekelezaji wa sheria. Tatu, Mswada unampa malaka Msajili kuruhusu au kutokuruhusu elimu ya uraia na shughuli za kuvijengea vyama vya siasa uwezo.

**Mapendekezo**

- Katika kifungu cha 3(a)(5)(g), Msajili anaweza kutoa miongozo ya utoaji elimu ya uraia kwa vyama vya siasa lakini si kusimamia.
- Ondoa uwezekano wa Msajili kuzuia shughuli za kuvijengea uwezo vyama vya siasa, badala yake anaweza kutoa ushauri au kuweka miongozo.
- Ondoa (7) kutoka Kifungu cha 6A na hariri (6) kuruhusu vyama vya siasa kufanya shughuli za kuhamasisha umma na kushawishi utendaji wa serikali
- Kuweka wazi kuwa kipengele 21D(2) kinahusika tu na kauli zinazotolewa kwa Msajili kama sehemu ya kufuata masharti ya sheria.
- Kurejesha hitaji la vyama kuchapisha rejesta kwenye kipengele cha 8C(3).

**4) Vikwazo pale vyama vinapotaka kuungana na kushirikiana**

Marekebisho yamekuja na kanuni kwenye eneo ambalo hapo awali halikuwa limefafanuliwa kwa kina na sheria iliyoko ya Vyama Vya Siasa – suala la vyama kuungana na kushirikiana. Katazo hili jipya linasema kuwa vyama vitaruhusiwa kuungana “ndani ya siku 21 kabla ya kupendekezwa kwa wagombea wa uchaguzi mkuu” – kikwazo ambacho kinaweza kusababisha vyama vishindwe kuungana. Zaidi, na muhimu mno, Sheria inampa mamlaka waziri kutengeneza kanuni za kusimamia kuungana kwa vyama – huu ni mgongano wa wazi wa kimaslahi ukizingatia kazi ya waziri kwenye chama cha siasa.

**Mapendekezo**

- Sheria mpya iruhusu vyama vya siasa kuungana muda wowote kabla ya kampeni kuanza na iondoe takwa la Waziri kutengeneza kanuni zitakazosimamia muunganiko wa vyama. Izingatiwe pia Sheria iliyopo imeweka muda wowote.

**5. Marekebisho ya sheria yametumia vifungu na maneno yasiyo na maana ya moja kwa moja ambayo kisheria yanaweza kuwa na maana zaidi ya moja hivyo kuruhusu maamuzi yasiyo na usawa.**

Baadhi ya vifungu katika sheria hii vinampa Msajili mamlaka ya kufanya maamuzi yenye madhara makubwa kwa vyama kwa kufuata kile “anachokiamini” au kwa “kutoridhishwa" na jambo fulani.

**Mapendekezo**

Vifungu na maneno yoyote yenye utata na yanayoweza kutoa mianya ya maamuzi yasiyo na usawa yatolewe maana au kuondolewa kabisa katika sheria.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ahadi ya kuwalipa korosho izingatiwe

**TANGU** Novemba mwaka jana, Rais John Magufuli, alipotangaza kuwa serikali itanunua korosho baada ya kubaini kuwa kampuni za ununuzi wa zao hilo hazikuwa na nia njema, baadhi ya wakulima wamekuwa wakilalamikia kucheleweshwa kwa malipo yao.

Wamekuwa wakidai kuwa mchakato wa kuwalipa umechukua muda mrefu licha ya kuwa walishahakikiwa, na kwamba ucheleweshaji huo umewaathiri sana.

Waliokuwa wanalalamika kuwa kucheleweshewa malipo kumekuwa kukiwakwamisha kufanya mambo ya msingi ambayo walikuwa wameyapanga.

Hata hivyo, kwa upande wake serikali imekuwa ikisema kuwa fedha za kutosha kuwalipa zipo, isipokuwa tatizo lilikuwa ni baadhi ya watu kutumia fursa hiyo kufanya mbinu chafu za udanganyifu kwa lengo la kujipatia fedha wasizostahili, na kwamba njia pekee ilikuwa ni kufanya uhakiki wa kina kujiridhisha kuwa wanaolipwa ni wale wanaostahili.

Kimsingi, serikali ilibaini njia mbalimbali zilizokuwa zinatumiwa na wajanja wachache kutaka kujinufaisha kwa njia mbalimbali ikiwamo kuwagundua hata watu wasio na mashamba wakiwa na korosho, hivyo kuhoji hizo korosho wanazipata wapi?

Tunachoweza kukisema ni kuwa kila upande ulikuwa na haki ya kusimamia msimamo wake. Tunamaanisha kwamba wakulima walikuwa na haki ya kudai malipo yao kwa wakati kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na majukumu ya msingi kama kutimiza mahitaji ya watoto wao kwenda shule na mengine.

Kwa upande wake serikali nayo ilikuwa na nia njema ya kufanya uhakiki wa malipo ya korosho kwa kujua kuwa zilikuwapo njama za kufanya udanganyifu, na ndiyo maana baada ya uhakiki kubaini njama hizo ilizifungia baadhi ya akaunti.

Jana serikali ilitangaza kwamba kufikia Februari 15, mwaka huu wakulima wote wanaoidai serikali malipo ya zao hilo watakuwa wamelipwa malipo yao.

Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha malipo yote ya fedha za korosho yawe yamelipwa tarehe hiyo, na kwamba kufikia wakati huo serikali haitarajii kuendelea kusikia neno la uhakiki.

Aliagiza akaunti za benki 191 za wakulima zilizokuwa na mkanganyiko, taarifa zitolewe kwa wahusika ili waweze kuzirekebisha na wakulima walipwe fedha zao kwa wakati na kuzima malalamiko, huku akitaka kuboresha mfumo wa upashanaji habari.

Kwa ahadi hiyo bila shaka serikali itakuwa imeridhika kuwa wahusika sahihi sasa wanaweza kulipwa fedha zao na pengine ndio maana suala hili limepewa uzito kwa kutangazwa na Waziri Mkuu, ambaye pia amekwenda mkoani Mtwara kufuatilia ulipaji wa fedha hizo.

Kinachopaswa kufanyika sasa ni kwa wahusika ambao ni wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wakulima wote wanaodai wanalipwa haraka iwezekanavyo kabla ya kupita muda ulitotajwa.

Itakumbukwa kuwa Rais Magufuli katika siku za karibuni aliwahi kusema kuwa haelewi kwanini wakuliwa wa korosho hadi sasa hawajalipwa fedha zao ilhali fedha za malipo hayo zipo.

Wakulima wa korosho tunawapongeza kwa kuonyesha uvumilivu na subira kwa muda wote ambao walikuwa wanahangaikia malipo yao na bila shaka sasa watapata haki yao.

Tunawahimiza wahusika wa malipo hayo kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anatimiza wajibu wake ili wakulima wote walipwe bila kuwapo mkwamo na watakaoshindwa kuwajibika wachukuliwe hatua stahiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**TUSIWE SEHEMU YA MATATIZO**
**KERO NA MATATIZO YOYOTE YANATAKIWA KUTATULIWA KWA HARAKA NA SIYO KUENDELEA KUYAFUGA. TUAZIMIE KUZIONDOA KERO ZILIZOPO NA ZILE ZITAKAZOKUJA, TUKIEPUKA SISI WENYEWE KUWA SEHEMU YA MATATIZO HAYO. TUSIWE VIKWAZO KATIKA SULUHISHO. MARIDHIANO NI DAWA. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuhimize maadili, unyofu janga la udanganyifu katika mitihani

Na Raphael Kibiriti

**MOJA** ya habari zilizotikisa katika kurasa za mbele za magazeti na vituo vya televisheni na redio wiki iliyopita, ilikuwa ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne kwa mwaka 2018.

Kilichoingezea mtikisiko habari hiyo ni suala la kuendelea kujitokeza kwa udanganyifu katika mitihani hiyo kama ilivyokuwa kwa mwaka wa 2017.

Wizi na udanganyifu wa mitihani ni janga ambalo limejitokeza kwa nyakati tofauti katika mitihani ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili, kidato cha nne na kile cha sita. Kwa mfano wanafunzi 33 walifutiwa matokeo yao baada ya kubainika kufanya udanganyifu katika mtihani wa darasa la nne mwaka 2017.

Sasa kwa matokeo yaliyotangazwa wiki iliyopita ya kidato cha nne kwa mwaka 2018, watahaniwa 254 walifutiwa matokeo yao kutokana na udanganyifu na kuandika matusi.

Cha kusikitisha zaidi katika kituo kimoja, uongozi wa shule uliwapatia jukumu maalumu baadhi ya wanafunzi wa kidato cha pili na tatu.

Wanafunzi hao walipewa jukumu la kuchukua mitihani kutoka kwa watahaniwa kupitia kwenye madirisha na matundu yaliyotobolewa kwenye vyumba vya mitihani na kuwafikishia walimu wa masomo waliokuwa kwenye chumba maalumu kwa lengo la kukokotoa majibu.

Kwamba wanafunzi hao walishirikiana na walimu kunakiri majibu yaliyoandaliwa na hatimaye kwa kushirikiana na askari polisi aliyekuwa kituoni, majawabu yalirejeshwa kwa watahaniwa ndani ya chumba cha mtihani.

Muungwana anasema kitendo hiki kimsingi ni cha kusikitisha kwani kinatishia uhai wa taifa, hivyo kinabidi kudhibitiwa kwa nguvu zote. Ni bahati mbaya kwamba jamii yetu imeonekana kuendekeza nadharia isiyo sahihi kuwa mtu anapaswa kufanya chochote katika upeo wake ili tu ashinde au ufaulu. Mila zetu zinaonekana kukubaliana hata kupanda migongo ya wengine, ukiwa katika harakati za kusaka mafanikio.

Na mbaya zaidi, baadhi ya wazazi na walezi wamechangia kwa hili kwa kutotoa kipaumbele cha kuchagiza maadili chanya kwa watoto wao kama vile uaminifu, juhudi na unyofu.

Badala yake, wamekuwa wakishinikiza watoto wao wafaulu kwa viwango vya juu ili tu waje kupata kazi nzuri au kuwa na maisha mazuri baadaye na hilo litawezekana tu iwapo watafanya vyema shuleni na vyuoni kwa kupata ufaulu au alama za juu zaidi.

Yapo madhara mengi, lakini baadhi ni pamoja na kashfa ama kupoteza hadhi na heshima kwa jamii, ndugu na jamaa zake pale mwanafunzi anapokamatwa akitumia 'nondo' ili afaulu mitihani yake. Kila mahali ni kunyooshewa kidole na kupewa majina kama yale ya 'mzee wa nondo' hali inayoweza ikasababisha msongo wa mawazo na hatimaye kuathiri afya yake.

Mtihani ni mchezo wa kanuni, sasa mwanafunzi anapoiba mitihani au anapofanya udanganyifu,anakuwa hatendi haki kwa wanafunzi wenzake ambao wamesoma muda wote wakijisomea ili wafaulu. Sasa inapotokea wanakuwa wanashindana na mtu anayetumia nondo ili afaulu inakuwa si haki kwa wenzake.

Kwa bahati mbaya udanganyifu ama wizi katika mitihani si suala la kufanyika mara moja tu, kwani suala linapoanza hatimaye huwaaminisha wanafunzi kwamba kumbe ni rahisi kuendelea kudanganya katika mazingira mengine ya kimaisha. Na matokeo yake hata wakiwa kazini, ndipo hapo tunapopata Wahandisi wanaojenga madaraja yanayoanguka baada ya muda mfupi au daktari anayefanya upasuaji wa kichwa badala ya mguu.

Ni rai ya Muungwana kwa shule, wazazi na wadau nchini kulipiga vita janga hili la udanganyifu katika mitihani kwa kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wote ambao kwa njia moja au nyingine wanabainika kuhusika nalo.

Vyanzo mbalimbali vinaonyesha kwamba taifa letu liko nyuma kielimu ikilinganishwa na baadhi ya nchi za Afrika Mashariki.

Tukilea kizazi cha watu wasio na elimu na waliojaa udanganyifu, hatuwezi kushindana katika uga wa kimataifa, hivyo tuhimize maadili na unyofu.

# TANGAZO

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA MWAKA WA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2018 | 30.09.2018 |
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,211 | 2,740 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,969 | 7,829 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 19,921 | 22,728 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 21,706 | 14,179 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 441 | 392 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 53,208 | 55,548 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,697 | 3,906 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 757 | 562 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **112,909** | **107,884** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 10,279 | 23,453 |
| 18 | Amana za Wateja | 76,457 | 58,244 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,735 | 2,221 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 38 | 43 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 885 | 978 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | | |
| 26 | Baadae | 61 | 60 |
| 27 | Dhima Nyingine | 369 | 347 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | ***JUMLA YA DHIMA*** | **91,824** | **85,347** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **21,085** | **22,537** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,025 | 20,025 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,006 | 3,652 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | -889 | -1,534 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | -1,058 | 394 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **21,085** | **22,537** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 16,935 | 10,851 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,300 | 4,139 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,595 | 636 |
| | | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19% | 21% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 10% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 61% | 67% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 49% | 52% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84% | 86% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 8% | -21% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 5% | -17% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2018

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **20,025** | **-** | **(1,487)** | **3,132** | **464** | **9** | **22,143** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (1,058) | | | | **(1,058)** |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | 598 | (598) | - | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2018** | **20,025** | **-** | **(1,947)** | **2,534** | **464** | **9** | **21,085** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,025** | **-** | **(2,048)** | **3,517** | **454** | **9** | **21,957** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | 113 | | | | 113 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | - |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (220) | 210 | 10 | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2017** | **20,025** | **-** | **(2,155)** | **3,727** | **464** | **9** | **22,070** |

**Tumelipa Millioni moja tu kama adhabu ya SMR**

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO LINGANISHI YA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31.12.2018 | 31.12.2017 | 31.12.2018 | 31.12.2017 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,800 | 2,507 | 8,924 | 9,876 |
| 2 | Gharama za Riba | 704 | 1,120 | 3,423 | 4,057 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | *1,097* | *1,387* | *5,501* | *5,819* |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 58 | 343 | 271 | 1,057 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1,311 | 379 | 1,817 | 392 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | *555* | *697* | *1,968* | *1,910* |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 71 | -11 | 247 | 96 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 174 | 222 | 949 | 935 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 310 | 485 | 772 | 879 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | *1,705* | *1,473* | *6,294* | *5,958* |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 550 | 532 | 2,386 | 2,340 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 128 | 85 | 224 | 129 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 1,026 | 856 | 3,684 | 3,489 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,422)** | **(111)** | **(913)** | **323** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 30 | 56 | 146 | 210 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | *(1,452)* | *(167)* | *(1,058)* | *113* |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | *(1,452)* | *(167)* | *(1,058)* | *113* |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 69 | 69 | 69 | 69 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (73) | (8) | (53) | 6 |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (73) | (8) | (53) | 6 |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -1.29% | -0.09% | -0.83% | 0.10% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -6.66% | -0.76% | -4.85% | 0.52% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 72.37% | 45.98% | 57.78% | 50.55% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 1.17% | 1.43% | 5.87% | 5.99% |


### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO LINGANISHI YA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31.12.2018 | 31.12.2017 | 31.12.2018 | 31.12.2017 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,800 | 2,507 | 8,924 | 9,876 |
| 2 | Gharama za Riba | 704 | 1,120 | 3,423 | 4,057 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | *1,097* | *1,387* | *5,501* | *5,819* |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 58 | 343 | 271 | 1,057 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1,311 | 379 | 1,817 | 392 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | *555* | *697* | *1,968* | *1,910* |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 71 | -11 | 247 | 96 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 174 | 222 | 949 | 935 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 310 | 485 | 772 | 879 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | *1,705* | *1,473* | *6,294* | *5,958* |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 550 | 532 | 2,386 | 2,340 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 128 | 85 | 224 | 129 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 1,026 | 856 | 3,684 | 3,489 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,422)** | **(111)** | **(913)** | **323** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 30 | 56 | 146 | 210 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | *(1,452)* | *(167)* | *(1,058)* | *113* |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | *(1,452)* | *(167)* | *(1,058)* | *113* |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 69 | 69 | 69 | 69 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (73) | (8) | (53) | 6 |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (73) | (8) | (53) | 6 |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -1.29% | -0.09% | -0.83% | 0.10% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -6.66% | -0.76% | -4.85% | 0.52% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 72.37% | 45.98% | 57.78% | 50.55% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 1.17% | 1.43% | 5.87% | 5.99% |


Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

**Saini:**

**RAMA KRISHNA MARAKANI**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 17 JAN 2019

**AMANI MWIDETE**
Mkuu wa fedha
Tarehe: 17 JAN 2019

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 17 JAN 2019

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

**Saini:** **LIM TEONG LIAT**
Mwenyekiti wa Bodi
Tarehe: 17 JAN 2019

**CHARLES RWECHUNGURA**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 17 JAN 2019

# Uongozi Posta wapewa miezi 6 kurejesha mali

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ameutaka uongozi wa Shirika la Posta (TPC) kurudisha mali za shirika hilo vikiwamo viwanja na majengo ndani ya miezi sita.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam alipofungua kikao cha 26 cha Baraza Kuu la Wafanyakazi wa shirika hilo, lililojumuisha viongozi na wawakilishi wa baraza hilo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

"Ifikapo Juni 30, mwaka huu, mali zote za shirika ziwe zimerudi kuwa mali ya Shirika la Posta, hata kama mliuziana zirudi, hizi ni mali za serikali na ninyi hamtakuwa wa kwanza kurudisha majengo na viwanja kwa kuwa wenzenu wa Shirika la Reli wamerudisha," alisema.

Kamwelwe pia aliuagiza uongozi wa shirika hilo kuhakikisha ndani ya kipindi ya miezi sita, wilaya zote 186 nchini zinakuwa na huduma za posta.

Alisema TPC ina watumishi 821 nchi nzima, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa bidii, kuwa wabunifu na kuchapa kazi kwa kuzingatia taaluma zao ili kuongeza ufanisi, tija na ukuaji katika kuwahudumia wananchi.

Waziri huyo pia aliuagiza uongozi wa shirika hilo kuhakikisha unatumia mifumo ya kielektroniki kusafirisha fedha badala ya kutumia mfumo wa zamani wa wafanyakazi kushika pesa za mauzo, makusanyo na mapato mkononi.

Vilevile, aliushukuru uongozi wa shirika hilo kwa kuendelea kulipa deni la wastaafu ambalo limefikia kiasi cha Sh. bilioni 6.5 na kuwaahidi kushirikiana nao ili serikali iweze kurudisha fedha zao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Kanali Mstaafu Dk. Haruni Kondo, alisema shirika halijapewa mtaji na serikali, huku akiwapongeza wafanyakazi kwa ushirikiano wao na kwa kulifikisha shirika lilipo kwa kuwa wanadai deni la Sh. bilioni 6.5 serikalini kwa kulipa wastaafu.

## Mahakama yamfutia kesi bosi Nida

INAENDELEA UK. 3

wakiwa watumishi wa umma kwa nafasi walizokuwa nazo walitumia madaraka vibaya.

Wanadaiwa waliidhinisha malipo kwa Gotham International Limited (GIL) ya Dola za Marekani 2,700,000 bila ya kutumia viwango vya kubadilisha fedha za kigeni vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kinyume na kifungu cha 19.3 cha mkataba kati ya NIDA na GIL, hivyo kuifanya GIL kupata faida ya Sh. 3,969,000.

Maimu na Mwakatumbula katika shtaka jingine wanadaiwa kati ya Juni 3 na 5, 2013, katika makao makuu hayo walitumia madaraka vibaya kwa kuidhinisha malipo kwa GIL ya Dola za Marekani milioni 1.8, bila ya kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha, hivyo kuifanya GIL kupata faida ya Sh. 106,346,000.

Washtakiwa hao wawili wanadaiwa Juni 20, 2014 katika makao makuu hayo, waliidhinisha tena malipo ya Dola za Marekani 675,000 kwa GIL bila ya kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha, hivyo kuifanya kampuni hiyo kupata faida ya Sh. 42,471,000.

Maimu na Mwakatumbula wanadaiwa kutumia madaraka yao vibaya kwa kupitisha malipo mengine ya Sh. milioni 6 kwa GIL bila ya kupiga hesabu kwa kutumia viwango vya kubadilisha fedha, hivyo kuifanya kampuni hiyo kupata faida ya Sh.14,661,676.76.

Maimu na Mwakatumbula wanadaiwa kati ya Januari 15, 2010 na Mei 16, 2015 katika makao makuu ya NIDA kwa kuidhinisha malipo kwa GIL ya Dola za Marekani bila ya kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha za kigeni waliisababishia NIDA kupata hasara ya Sh. 167,445,676.76.




Mratibu wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU (Nacopha) Kanda ya Dar es Salaam, Edna Edson, akimkabidhi Mkuu wa Stoo ya dawa na vifaa tiba wa Hospitali ya Amana, Dk. Namsifu Mzava, msaada wa dawa za kutibu magonjwa nyemelezi kwa watoto wenye maambukizi ya VVU kupitia mradi wa Sauti Yetu kwa hisani ya USAID, katika halfa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

28 Januari, 2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu** tarehe **04/02/2019** kampuni ya **Mainline carriers Limited** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es Salaam Port** kuelekea **Tunduma**, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T653DFA/T245BYM**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20.0 |
| Upana | - | mita | 4.3 |
| Kimo | - | mita | 4.6 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaama Port hadi Tunduma Kupitia Mikumi,** gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.


# BoT yawaita wadau maoni sheria mpya ya fedha

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu (BoT), imesema inakusanya taarifa mbalimbali za wadau ili kuanza mchakato wa kutengeneza kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

Meneja wa Usimamizi wa Benki Zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni wa BoT, Victor Tarimu, aliiambia Nipashe jana kuwa, usajili wa watoa huduma ndogo za fedha utaanza rasmi kanuni zitakapotolewa na benki hiyo.

"Ni vyema jamii ikafahamu kwamba, mchakato huu utakuwa shirikishi ili kuhakikisha kuwa kanuni zitakazotolewa zinaendana na hali halisi ya biashara ya watoa huduma ndogo za fedha," alisema.

Meneja huyo aliongeza: "Kwa sasa hivi, tuko kwenye mchakato wa kukusanya taarifa muhimu toka kwa wadau zitakazotumika katika kutengeneza kanuni."

Tarimu aliwataka wadau wanaotoa huduma za fedha kwa wananchi Tanzania Bara, kuwasilisha taarifa zao BoT kabla ya Januari 31, mwaka huu.

"Wadau hawa hawajumuishi vyama vya Akiba na Mikopo (Saccos) kama tulivyobainisha katika tangazo la Januari 5, mwaka huu. Kwa sasa, hakuna hatua yoyote ya kisheria inayoweza kuchukuliwa dhidi ya mdau yeyote atakayeshindwa kuwasilisha taarifa kwa kuwa sheria haijaanza kutumika," alisema.

Meneja huyo alisema upo uwezekano wa muda wa kuwasilisha taarifa BoT kuongezwa na kwamba utafanyika baada ya tathmini ya mwitikio wa wadau ifikapo Januari 31, mwaka huu, yaani keshokutwa.

"Hadi sasa, kwa wastani wadau ambao wanakadiriwa kufikia asilimia 60 ya walengwa, wamekwishawasilisha taarifa zao Benki Kuu kama ilivyoagizwa. Tunatarajia hadi keshokutwa, asilimia 80 ya wadau watakuwa wamewasilisha taarifa zao," alisema.

HABARI KITAIFA

# Trafiki wanolewa

**Na Yasmine Protace,** PWANI

ASKARI wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Pwani, wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzifahamu zaidi sheria wanazosimamia kila siku katika utekelezaji wa majukumu yao ya usalama barabarani.

Katika mafunzo hayo ya siku moja yaliyofanyika Kibaha yalihusisha wakuu wa usalama barabarani toka wilaya zote, pamoja na wawakilishi watano toka kila wilaya mkoa wa Pwani na ofisi ya mkuu wa kikosi hicho mkoa (RTO) ambao baada ya mafunzo hayo, watakwenda kufundisha wenzao waliyojifunza.

Lengo ni kuwa na utendaji wenye mfumo mmoja katika mafunzo hayo, yaliyoratibiwa na kuwezeshwa na RSA ambao ni mabalozi wa usalama barabarani nchini.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Mnadhimu Mkuu Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi, Barnabas Mwakalukwa, aliwataka askari waliopata mafunzo hayo kuyatumia kivitendo kwa kwenda kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao ikiwamo kuwaelimisha wenzao ambao hawajapata mafunzo hayo ili kufikia lengo lililokusudiwa.

"Mafunzo haya yatumiwe vizuri ili kuleta mafanikio katika usalama wa barabarani," alisema Mwakalukwa.

Naye Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Pwani, Mrakibu Msaidizi Mosi Ndozero, aliwaagiza wakuu wa usalama barabarani wilaya zote kwenda kusimamia watendaji waliochini yao kuhakikisha wanatoa huduma bora siku zote na kupunguza malalamiko yasiyo ya lazima dhidi ya Jeshi la Polisi.

Mwezeshaji kutoka Nenda Salama Barabarani, Irene Mselem, alieleza kuwa kampeni ya nenda salama barabarani ilianza Desemba Mosi mwaka jana kwa mikoa sita ya Pwani, Mwanza, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, lakini wameamua kujikita katika utoaji wa elimu kwa Mkoa wa Pwani kwa kuwa ndio lango la kuingia na kutoka kwenda mikoa mingi nchini na nchi jirani.

Ameongeza kuwa kwa kuanzia wamejikita kwa utoaji elimu katika shule za msingi 5 na sekondari 5 za Wilaya ya Kibaha wakiamini Kibaha inapitiwa na idadi kubwa ya magari kila siku.

Mkuu wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia Mkoa wa Pwani, Mrakibu Msaidizi Sija Kadogosa, aliahidi kuitumia elimu aliyoipata kwenda kuelimisha askari walio chini yake kwa kuwa nao ni miongoni mwa wadau wakuu wa usalama barabarani.

# Watendaji mitaa wapigwa msasa kodi ya majengo

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani Iringa, imewaomba watenda wa mitaa na kata katika Manispaa ya Iringa kusaidia ukusanyaji wa kodi ya majengo katika maeneo yaliyoidhinishwa.

Akizungumza katika kikao cha TRA na watendaji, Meneja wa TRA Mkoa wa Iringa, Lamson Tulyanje, alisema kodi ya majengo inatozwa kwa ajili ya nyumba zilizopo katika maeneo yaliyoidhinishwa.

Alisema watendaji hao wanatakiwa kusimamia ukusanyaji wa kodi ya majengo katika maeneo yao kwa kutumia mfumo wa bili za majengo kutoka TRA.

"Kodi ya majengo ni chanzo kingine cha mapato ya serikali, hivyo watendaji wote wanatakiwa kusajili nyumba zote zinazostahili kulipa kodi ya majengo kwenye daftari ya makazi katika maeneo yao," alisema Tulyanje.

**Sheria ya utoaji kodi ya majengo ya mwaka 1983 imeainisha maeneo yanayotozwa kodi ya majengo kuwa ni halmashauri ya miji, miji midogo na majiji.**

Alisema sheria ya utoaji kodi ya majengo ya mwaka 1983 imeainisha maeneo yanayotozwa kodi ya majengo kuwa ni halmashauri ya miji, miji midogo na majiji.

Tulyanje aliongeza kodi ya majengo ilikuwa inakusanywa na halmashauri ya miji, majiji na manispaa zote nchini, lakini mwaka 2016 kupitia Bunge la Bajeti serikali ilirekebisha sheria ya kodi ya majengo na kuipa TRA jukumu la kukadiria, kukusanya na kuhesabu kodi ya majengo katika halmashauri zote.

Aidha, alisema nyumba zote katika maeneo ya kutozwa kodi zitatozwa kodi ya majengo isipokuwa nyumba zilizojengwa kwa udongo, nyumba zilizoezekwa kwa nyasi au nyumba zote zenye kufanana na hizo.

Alisema sheria ya kodi ya majengo inataja kiasi cha kodi kuwa ni Shilingi 10,000 kwa nyumba za kawaida na Shilingi 50,000 kwa kila ghorofa kwa nyumba za ghorofa na kuongeza kuwa kodi hiyo inalipwa kwa mwaka mara moja.

Naye Ofisa Utumishi wa Manispaa ya Iringa, Omary Mkangama, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Hamid Njovu, aliwataka viongozi na wananchi kushirikiana na TRA, ili kupata taarifa za kaya zenye sifa za kulipa kodi ya majengo ili waweze kutengenezewa na kupewa hati za madai mapema ili kuzuia usumbufu unaoweza kujitokeza.



Askofu Dk. Batholomayo Shegah, Mkuu wa Mafunzo Chuo Kikuu cha Biblia cha Japan (JBI) Afrika, akimkabidhi tuzo ya utendaji kazi huduma na utumishi uliotukuka, Askofu John Kyashma wa Kanisa la River of Healing Ministry of Tanzania Kiluvya kwa Komba, iliyotolewa na Taasisi ya Outreach Care katika Kanisa la Light House Christian Centre jijini Dar es Salaam. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wazazi watakaokaidi kupeleka watoto kidato 1 kukiona

**Na Ndalike Sonda,** BUKOMBE

SERIKALI wilayani Bukombe mkoani Geita, imesema mzazi au mlezi atakayeshindwa kumpeleka shule mwanafunzi aliyefaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, atachukuliwa hatua za kisheria.

Kauli hiyo ilitolewa mjini Ushirombo na Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, kwenye sherehe ya maadhimisho ya miaka 25 ya upadri wa paroko wa Parokia ya Bikira Maria Msaada wa Daima-Ushirombo Jimbo Katoliki la Kahama, Padri Peter Kandundu.

Nkumba alisema serikali imeamua kutoa elimu bila malipo, hivyo mzazi hanabudi kuhakikisha mwanafunzi anashiriki kikamilifu masomo yake bila vikwazo kutoka kwa mzazi au mlezi.

Aidha, Nkumba aliwaagiza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kusimamia kikamilifu sekta ya elimu, ili kila mwanafunzi aliyeandikishwa darasa la kwanza na wale waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu wanahudhuria masomo.

Katika hatua nyingine, Nkumba aliwataka wazazi na walezi kuendelea kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kuchangia miradi mbalimbali ikiwamo ya sekta ya elimu, afya na mingine muhimu.

Nkumba alisema serikali wilayani Bukombe inatambua mchango wa Kanisa Katoliki katika wilaya hiyo, kutokana na kuwa mstari wa mbele katika kuchangia miradi ya maendeleo ikiwamo ya elimu, afya na maji.

Alisema kanisa hilo wilayani Bukombe limekuwa mstari wa mbele katika kusaidia miradi ya maendeleo, na kwamba serikali itaendelea kuunga mkono juhudi hizo na zinazofanywa pia na madhehebu mengine ya dini.

Naye Padri Kadundu aliwataka waumini kuzidi kumwombea, huku akiwapongeza waumini na viongozi wa serikali kwa maombi na sala zao.

# Mchakato ujenzi madaraja korofi wakamilika

**Na Futuna Seleman**

SERIKALI imesema mpango mkakati wa kumaliza kero ya madaraja korofi Manispaa ya Ilala uko mbioni kutekelezwa, ili kumaliza adha ya muda inayowakabili wananchi wa Ulongoni A na B na Mongolandege Jimbo la Ukonga jijini Dar Salaam.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI, Mwita Waitara, aliyasema hayo akiwa katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya afya, ujenzi na elimu katika kata nane Manispaa ya Ilala.

Akiwa katika Daraja la Ulongoni B mara baada ya kulikagua alikiri uwapo wa changamoto katika eneo ambalo mvua kubwa zikinyesha wananchi kushindwa kuvuka katika eneo hilo.

Naibu Waziri Waitara, alisema eneo la daraja Ulongoni B, mvua ikinyesha daraja huvunjika, hivyo ni lazima lijengwe la kudumu na tayari serikali imetenga Shilingi milioni 500 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, ili ujenzi huo uanze mara moja baada ya makandarasi kujua kiwango cha fedha kitakachotumika kujenga daraja la kudumu katika eneo hilo.

"Tumeona tusipotezee fedha kwa kujenga kitu kisichomaliza tatizo kwa wananchi tayari fedha zimetolewa na Rais Magufuli wataalamu wanafanya usanifu zitengwe shilingi ngapi ili lijengwe daraja la kudumu, kazi inafanywa ndani ya mwezi huu, ikikamilika ujenzi utaanza wakati wowote," alisema.

**Tumeona tusipotezee fedha kwa kujenga kitu kisichomaliza tatizo kwa wananchi tayari fedha zimetolewa na Rais Magufuli wataalamu wanafanya usanifu zitengwe shilingi ngapi ili lijengwe daraja la kudumu.**

"Nasisitiza mambo mawili mnielewe Ulongoni B ujenzi utachelewa sababu lazima usanifu ufanyike kwanza, lakini daraja la watembea kwa miguu litaimarishwa kwa ushirikiano wa TARURA na Manispaa, daraja linalokaribia kukamilika ujenzi ni la Ulongoni A wananchi wanaoishi upande wa chini wa daraja hili watahamishwa na kulipwa fidia na Mongolandege litajengwa katika bajeti ya mwaka 2019/2020," alisema Waitara.

"Mradi wa daraja Ulongoni B utakaokwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya lami ya kilomita 7 utajengwa, unatekelezwa kupitia mradi wa uendelezwaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP), wafadhili kutoka Benki ya Dunia unaweza kuchelewa kidogo, hivyo wananchi vumilieni msisikilize maneno ya watu wasioitakia mema serikali ya awamu ya tano wanaopita kueneza maneno ya uongo ili muichukie serikali," alisema Waitara.

Akifafanua zaidi alisema daraja la Ulongoni A, mchakato wa ujenzi wake umekamilika na wananchi wanaoishi upande wa chini wa daraja hilo watahamishwa na watalipwa fidia.

Akiwa katika kata ya Majohe kwenye daraja la Bangulo linalounganisha barabara kubwa ya kwenda Pugu Sekondari hadi Mbondolwe inayounganisha G.mboto, Pugu, Majohe hadi Mbondolwe, ambayo iko Kata ya

Msongola inayounganisha Mbande hadi Mbagala, amesema barabara hiyo ni kubwa inategemewa na wananchi wengi ikikamilika itawasaidia watu wengi wanaotoka Mbagala kwenda Ubungo ama Morogoro itakuwa rahisi kwao kutokea Mbezi.

Alisema eneo lilipo daraja la Bangulo wakati wa mvua ni korofi, hivyo changamoto hiyo itatatuliwa kwa kuwa Tarura na Manispaa ya Ilala wanaifanya kazi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ilala Jumanne Shauri, alikiri fedha za mkandarasi kufanya upembuzi yakinifu ili daraja korofi la Ulongoni B liweze kujengwa iko tayari na usanifu utafanyika ndani ya miezi miwili.

"Wakishakamilisha daraja la Ulongoni A lenye miezi miwili, kazi ya ujenzi itaanza Ulongoni B, usanifu ukikamilika na lenyewe litaombewa fedha ambayo itajengwa na barabara ya kilomita 7 kutoka Gongolamboto kwenda Kinyereza, pia usanifu ukikamilika mkandarasi ataanza kazi hiyo.

Akizungumzia sekta ya elimu, Shauri alisema mwaka huu halmashauri hiyo imetenga Shilingi bilioni 3 katika sekta ya elimu, ambapo Idara ya Elimu Msingi wametenga Shilingi milioni 660 na sekondari zaidi ya Shilingi bilioni mbili.

Mengine yaliyojitokeza katika ziara ya Niabu Waziri Waitara akitokea kukagua daraja la Bangulo, alisimamishwa na wananchi wa Kata ya Majohe baadhi yao wakilalamikia changamoto ya upatikanaji wa maji, miundombinu ya barabara, kubwa ikiwa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wa Viwege.

Hata hivyo kero hiyo iliyojibiwa na Mhandisi Seleman Mngwira, Meneja wa Tanesco mkoa wa Pwani, akiwahakikishia wananchi kuwa kupitia mradi wa Peri Urban unaofadhiliwa na REA unaotarajiwa kutekelezwa hivi karibuni majadiliano na makandarasi wanaendelea ili mkataba usainiwe mwezi wa pili na watatu mkandarasi aanze kazi ya kusambaza umeme wananchi watapata huduma hiyo waondoe shaka.

Awali wananchi wanaotumia daraja la Ulongoni A walilalamikia usumbufu wakati wa mvua kuvuka katika eneo hilo kutokana na maji kujaa na mawasiliano kukatika hali inayochangia pia usafiri kuwa mgumu.

"Mvua ikinyesha shida hakupitiki tunagawanyika kama tunaishi visiwani," alisema Madesla Swai mkazi wa Ulongoni A.

Mariam Matega alisema eneo hilo korofi wakati wa mvua wanapata maradhi ya fungusi kutokana na kukanyaga maji machafu kwa vile mto hufurika na maji kusambaa hadi majumbani mwao.



Makatibu wakuu wa wizara mbalimbali Tanzania, wakifuatilia kikao cha majumuisho cha mawaziri wanaohusika na mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania kilichofanyika jijini Kampala-Uganda. **PICHA: WN**

# Waomba ujenzi wa zahanati kuendelea

**Na Ibrahim Yassin,** VWAWA

WANANCHI wa vitongoji vilivyopo kijiji cha Ilembo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Vwawa wilayani Mbozi, mkoani Songwe, wameiomba serikali kupitia halmashauri hiyo kuwaruhusu kuendelea na ujenzi wa zahanati ili kupunguza msongamano hospitalini.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo, aliusimamisha ujenzi wa zahanati hiyo kwa madai ya kuwapo na tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za mradi huo ambao umesimama kwa zaidi ya miezi 18, huku wananchi wakiendelea kutembea umbali mrefu kusaka tiba.

Wakizungumza jana na gazeti hili, walisema wamekuwa wakipata shida kutembea umbali mrefu kusaka huduma za matibabu katika hospitali ya wilaya iliyopo mjini Vwawa na kuongeza usumbufu mkubwa katika kupanga foleni.

Ester Mtafya, mkazi wa Ilembo, alisema imekuwa kero kubwa kwa wananchi hasa watoto, wazee na wajawazito, ambao wanatumia muda mrefu kusimama katika foleni na kwamba ujenzi wa zahanati yao ulifikia asilimia 90, hivyo wanaomba ujenzi ukamilike.

Aisile Kijalo, mkazi wa Ilembo, alisema wanaiomba serikali kuwaacha waendelee kuikamilisha zahanati hiyo ili wao waendelee kuwachunguza wanaodaiwa kufanya ubadhirifu kwa sababu kusimamisha mradi kunawaathiri wananchi.

Ester Bashasha, Kaimu Mganga Mkuu wilayani humo, alisema kutokana na adha wanayoipata wananchi, muda wowote ujenzi utaanza kwa kuwa serikali inafanya kila liwezekanalo kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Kazimbaya Makwega, alisema licha ya kuwapo na changamoto hizo, ifikapo mwezi ujao ana uhakika zahanati hiyo itaanza kufanya kazi.

Zahanati hiyo ya kijiji cha Mantengo, imegharimu kiasi cha Shilingi milioni 8 kutoka serikalini, huku wananchi wakichangia nguvukazi. Itakapokamilika itapunguza msongamano kwa wagonjwa wanaorundikana Hospitali ya Wilaya ya Mbozi.

# Mkakati Olympio kujenga madarasa

**Na Beatrice Moses**

KAMATI ya Shule ya Msingi ya Olympio jijini Dar es Salaam, imetangaza kujenga vyumba vinane vya madarasa na ofisi ya walimu ili kuleta ufanisi zaidi.

Hatua hiyo imetangazwa baada ya shule hiyo kufanya vizuri kwenye matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2018, ambapo iliingia kwenye kumi bora kwa shule za msingi Wilaya ya Ilala kwa kushika nafasi ya 6 katika shule 90.

Awali akizungumza na wazazi kuhusu maendeleo ya shule, aliyekuwa Mwenyekiti wa kamati hiyo, Enock Anyisile, alisema matokeo hayo kwa shule za serikali Olympio imekuwa ni ya kwanza.

"Kutokana na matokeo hayo, kumekuwa na ongezeko kubwa la watu kuomba kuhamishia watoto hapa au kuanza darasa la kwanza, lakini madarasa yaliyopo ni yale yale yaliyojengwa tangu mwaka 1957," alisema.

Shule hiyo kimkoa ilishika nafasi ya 14 kati ya 448, wakati kitaifa imeshika nafasi ya 72 kati ya shule 10,090.

Wazazi wengi walipokea matokeo hayo kwa furaha, ambapo licha ya kumpongeza Mwalimu Mkuu, Salum Mugamba, na walimu wengine wa shule hiyo, walichagua tena wajumbe wa kamati hiyo ili kuipa nafasi ya kutimiza malengo ya maendeleo waliyojiwekea.



## HABARI ARUSHA

# Naibu waziri ahimiza halmashauri kutoa mikopo kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, amewataka wakurugenzi watendaji wa halmashauri kuwapa mikopo vijana, wanawake na walemavu kupitia mapato ya ndani, ili waweze kujikomboa kiuchumi.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na vijana wa mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mwishoni mwa wiki.

Shonza alisema wakurugenzi watakaoshindwa kutoa mikopo kwa vijana, wanawake na walemavu watachukuliwa hatua ikiwamo kupoteza nafasi zao.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa kutoa mikopo hiyo kwa malengo ya kuyanyanyua kiuchumi makundi hayo matatu muhimu kwa jamii.

"Na ninyi vijana mkipatiwa mikopo hiyo mtumie fursa hiyo ipasavyo, ili kuhakikisha mnaboresha maisha yenu ipasavyo kwa kujinufaisha ipasavyo," alisema.

**Alitoa onyo kwa watakaonakili vitambulisho hivyo, kwa kuwa watawachukuliwa hatua kali za kisheria hivyo waridhike na hivyo vitambulisho vitakavyotolewa na serikali.**

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliwataka vijana wa eneo hilo kutumia fursa ya kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite bila malipo kwa kufanya kazi.

Alisema serikali imeamua wakati utaratibu wa kuingia ndani kwa kutumia vitambulisho maalum ukisubiriwa, watu wataingia bure.

"Kitambulisho rasmi cha kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite itakuwa Sh. 70,000 kwa mwaka mzima, hivyo vijana mjipange kwenye hilo kwa kuwa ni kiasi kidogo mno," alisema.

Alitoa onyo kwa watakaonakili vitambulisho hivyo, kwa kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria hivyo waridhike na hivyo vitambulisho vitakavyotolewa na serikali.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), mkoani Manyara, Mosses Komba, alisema vijana wanampongeza Rais John Magufuli kwa kuagiza ujenzi wa ukuta huo.

Alisema wanampongeza Mkuu wa Mkoa huo, Alexander Mnyeti, kwa kuagiza wana apolo kupita bila malipo kwenye ukuta huo unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite.

Alisema vijana wengi walishindwa kuingia ndani ya ukuta huo ila baada ya kauli ya Mnyeti hivi sasa vijana wengi waliokuwa wamekosa ajira hivi sasa wananufaika.



Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, akisalimiana na viongozi wa CCM, alipotembelea Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Halmashauri yajipongeza kumaliza migogoro sugu ya ardhi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Babati, imesema moja ya njia iliyotumiwa kutatua migogoro ya ardhi ya siku nyingi ni kuwahimiza watendaji wa vijiji na kata kufanya vikao vya kurekebisha mipaka yenye migogoro kwa kuwashirikisha wazee maarufu wa mila.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Hamisi Malinga, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu namna walivyofanikisha kutatua migogoro sugu ya ardhi. Alitaja mgogoro uliotikisa halmashauri hiyo ulikuwa kati ya Kijiji cha Orbesh Kata ya Secheda dhidi ya Kijiji cha Singu wilayani Mbulu, uliodumu kwa miaka 19.

"Nilimshirikisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbulu, Hudson Kamoga, na wataalamu wa pande zote mbili tukakaa pamoja na wananchi na kuainisha mipaka kwa kuridhiana wote na hatimaye wakamuita mkuu wa mkoa na kumaliza mgogoro huo," alisema.

Alitaja migogoro mingine ambayo imeshughulikiwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni pamoja na mgogoro wa Kijiji cha Manyara na Kijiji cha Magara uliodumu kwa miaka mingi. Mgogoro mwingine ni kati ya Kijiji cha Kiru Dick uliokuwa kati ya wananchi na mwekezaji.

"Hapa kwetu siasa ni chanzo cha migogoro ya ardhi na watu wa hapa kuwa na uwezo wa kuuza mifugo yao maana watu wako radhi wavamie hifadhi za taifa na watu wa huku hawaoni tabu kuingia ofisi ya kiongozi yeyote kwa kuwa wanauza ng'ombe na kuwafuata viongozi walipo," alifafanua.

Alisema miongoni mwa changamoto walizozibaini kuongeza migogoro ni baadhi ya wanasiasa kutengeneza matatizo ili wapate kura, viongozi wa vijiji kulegea kwa kutaka maslahi binafsi ili wapate kile walichokusudia.

Alitumia fursa hiyo kuwahakikishia watu wanaotaka kuwekeza katika halmashauri hiyo, kuwa mazingira ni mazuri kwa sasa na hakuna migogoro ya ardhi ya kuwazuia kuwekeza, hivyo amewakaribisha wafike na wataweza kujipatia maeneo ya kujenga viwanda na kujenga miundombinu mingine inayolenga kuwekeza.

Naye Bahati Boay, mkazi wa Hoshani, aliiambia Nipashe kuwa umakini wa Rais John Magufuli ndiyo unawafanya watumishi wajitume ili wasije wakatumbuliwa.

Alisema hali hiyo inawafanya wajitume kwa kadri wawezavyo ili kulinda nafasi zao.

# Wanaoishi bila kufunga ndoa wapewa mtihani

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MENEJA wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) mkoani Manyara, Hance Mwankenja, amesema watumishi wa umma wanaoishi na wenza wao bila kufunga ndoa ni vema wakafanya hivyo, ili waweze kutambulika kisheria na kunufaika na bima hiyo.

"Ninawashauri wafunge ndoa ili watambulike kisheria badala ya kuishi kijanjakijanja hali inayomnyima mwenza mmojawapo huduma ya bima ya afya," alisema.

Alitoa ushauri huo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu watumishi wanaoishi bila kufunga ndoa, huku mmoja kati yao akiwa siyo mtumishi wa umma anawezaje kunufaika na huduma hiyo akiwa mwenza.

Baadhi ya watumishi wa umma wilayani hapa walikuwa wakilalamikia kuwa wenza wao hawapewi kadi za bima ya afya na hivyo kukosa huduma ya afya inayotolewa na bima hiyo.

Akitoa ufafanuzi, Mwankenja aliwataka watumishi kuacha kulalamika dhidi ya jambo hilo badala yake wafuate masharti yanayotakiwa ili wenza wao wapate huduma ya bima ya afya.

"Unajua ndoa siyo maneno ni vitendo, hivyo, unaposema huyu ni mwenza wangu uwe umeambatanisha cheti cha ndoa, ili na sisi tukutambue wewe pamoja na mwenza wako tukuhudumie maana ndoa ni hitaji la kisheria," alisema.

Aidha, alisema watumishi wa umma wanaokaa na wenza wao bila kufunga ndoa, kwa mujibu wa serikali hawatambuliwi kuwa mume na mke.

Alisema ndoa inathibitishwa na mamlaka husika ziwe za dini au serikali kupitia kwa mkuu wa wilaya.

Aidha, aliwashauri viongozi wa dini baada ya kufungisha ndoa waumini wao, wawape vyeti vya ndoa ambavyo vitawasaidia wenza wao kupata huduma mbalimbali.

"Ni vizuri watambue cheti cha ndoa kinamtambulisha mwajiriwa lakini kinamsaidia kumtambua na kumpa fursa ya kupata mafao ya likizo, maana bila hicho hawezi kupata mafao ya likizo ya kusafiri na familia," alisema.

Alifafanua kuwa mwenza wa mtumishi ambaye hajafunga ndoa hawezi kupata matibabu isipokuwa watoto waliowazaa ili mradi wawe na vyeti vya kuzaliwa.

Baadhi ya watumishi ambao hawajafunga ndoa wakizungumza na Nipashe kwa sharti la kutokuandikwa majina, walisema wenza wao wanapougua ndio wanapata shida ya matibabu na hivyo wanalazimika kulipa gharama kubwa.

# Hospitali ya wilaya yakosa chumba cha upasuaji

**Na Paul William,** SIHA

HOSPITALI ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, inakabiliwa na ukosefu wa majengo muhimu ikiwamo chumba cha upasuaji, hali ambayo imekuwa changamoto kwa wagonjwa wanaotakiwa kupatiwa huduma ya upasuaji.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Andrew Method, wakati akitoa taarifa ya hospitali hiyo kwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jesca Mbogo.

Alisema kuwa, mbali na kukosa jengo hilo la upasuaji pia wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya watumishi wa afya 417 sawa na asilimia 70, kwa kuwa watumishi waliopo kwa sasa katika wilaya hiyo ni 178 pekee.

Changamoto nyingine za afya zinazoikabili wilaya hiyo ni upungufu wa vituo vya afya kulingana na miongozo ya serikali, ilhali kila kata inatakiwa kuwa na kituo kimoja.

"Tunakabiliwa pia na kutokulipwa kwa watumishi muda wa ziada (on call allowance) kwa muda mrefu sasa hali ambayo imekuwa ikiwakatisha watumishi morali wa kufanya kazi kwa bidii kutokana na kudai madeni ya muda mrefu," alisema Dk. Method.

Dk. Method alisema kuwa, hospitali hiyo ya wilaya kwa sasa inahudumia wakazi wapatao 116,313 ambao wanatoka kwenye kata 17, ambapo kila mwezi imekuwa ikihudumia wastani wa wagonjwa 3,000.

Mganga mkuu huyo alisema kuwa, katika mwaka wa fedha 2018/19 hospitali hiyo ilipokea Shilingi bilioni 1.5 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa majengo sita ya kutolea huduma za afya, ambapo majengo hayo ni jengo la stoo ya dawa, jengo la utawala, jengo la kufulia nguo, jengo la wazazi, jengo la vipimo vya mionzi, na jengo la kuhifadhia maiti.

Akizungumza baada ya kusomewa taarifa hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa UWT, Jesca Mbogo, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Siha kuhakikisha anasimamia kwa ukaribu fedha ziizotolewa na serikali ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kujengwa kwa majengo yenye thamani na fedha zilizotolewa.

**"Zingatieni mnasimamia agizo la serikali la kutoa huduma za afya pamoja na dawa bure kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano pamoja na kinamama wajawazito na wazee, hilo ni jambo muhimu sana mnalopaswa kulikumbuka,"**

Jesca aliwaomba watumishi wa afya katika wilaya hiyo ya Siha kuendelea kujitolea kufanya kazi kwa bidii, huku serikali ikiendelea kupambana kuhakikisha kuwa changamoto zote zinazowakabili zinapatiwa ufumbuzi ikiwamo kulipwa madeni yao.

"Zingatieni mnasimamia agizo la serikali la kutoa huduma za afya pamoja na dawa bure kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano pamoja na kinamama wajawazito na wazee, hilo ni jambo muhimu sana mnalopaswa kulikumbuka," alisema Jesca.

Aidha, naibu katibu huyo aliwataka watumishi hao wa afya kuwaeleza kinamama athari za udumavu na utapiamlo kwa watoto pindi wanapohudhuria kliniki, ili kutambua umuhimu wa kuwapatia watoto lishe bora, alisema kuwa kulingana na takwimu asilimia 29 ya watoto mkoani Kilimanjaro wanautapia mlo.



Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi Issah, akikagua shehena ya dawa za kulevya aina ya mirungi kiasi cha kilo 320, zilizokamatwa zikisafirishwa kupelekwa mkoani Arusha kwa kutumia gari. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wadaiwa sugu wa maji kupandishwa kizimbani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Bonde la Maji la Mto Pangani mkoani Kilimanjaro, inakusudia kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa maji, pamoja wale waliochimba visima bila vilabali.

Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Sengule Sengule, alisema kuwa kumekuwapo na tatizo baadhi ya wateja wakubwa ambao ni kapuni na taasisi kukwepa kulipa bili za maji.

Alisema kuwa kutokana na tatizo hilo Mamlaka ya Bonde la Maji la Mto Pangani inakusudio la kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wote kwa mujibu wa sheria.

"Kuna baadhi ya wateja wetu wakubwa ambao kampuni na taasisi zimekuwa zikikwepa kulipa bili za maji kwa zaidi ya miaka tano na kuendelea na tumewafuatilia, lakini bado wamekaa kimya, sasa sisi kama mamlaka ambayo inawasimamia wateja hao tumefikia hatua za kufuata sheria,"alisema Sengule.

"Sheria inaturuhusi sisi kama mamlaka kuwachukulia hatua za kisheria wadaiwa sugu wanaokataa kulipa bili, hivyo tumeamua kuchukua hatua ili walipe bili za maji kwa maslahi mapana ya nchi," alisema.

Alisema kuwa ni vema sasa wadaiwa sugu wote wakafuata sheria na kulipa madeni hayo kwa haraka, kwa sababu hatuishii kuwapeleka mahakamani tutaendelea kuchukua hatua zaidi.

"Kwa sababu hizi sheria hatutungi sisi, imetungwa na Bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi kwa maslahi mapana ya nchi, hivyo sisi kazi yetu ni kuzifuata sheria hizo," alisema.

Katika hatua nyingine alisema kuwa mamlaka hiyo pia imeanza zoezi la kuchunguza uchimbaji wa visimi katika maeneo mbalimbali na kwamba watakaobainika hawana vibali watachukuliwa hatua za sheria.

"Tupo kwenye zoezi la kuchunguza utoaji wa vibali vya uchimbaji wa visima na zoezi hili tayari limeshaanza Tanga na baadaye Kilimanjaro, ila nawaasa tu waliojichimbia visima bila kibali wafike wenyewe kwenye ofisi za mamlaka, wasisubiri adhabu," alisema.

Aidha, alisema kuwa kazi ya bonde ni kutoa vibali kwa watumia maji kwa kufuata sheria na kanuni za bonde pamoja na kutunza vyanzo vya maji, mito na mifereji yote.

## Mchele wa Tanzania wang'ara kimataifa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha mchele mzuri na msafi ambao una thamani ukilinganisha unaozalishwa katika nchi za Msumbiji, Kenya, Rwanda na Burundi.

Sambamba na hilo pia imetajwa kuwa nchi yenye idadi kubwa ya wanawake wanaozalisha kwa wingi zao hilo, ambapo huzalisha tani 5-8 kwa hekta, ukilinganisha na nchi ya Msumbiji na Kenya.

Hayo yamebainishwa na mtaalamu wa kilimo kutoka Jimbo la Zambezia nchini Msumbiji, Jaime Gado, alipotembelea nchini akiwa na timu ya wataalamu wa zao la mpunga kwa lengo la kubadilishana ujuzi na kujifunza kutoka kwa wakulima wa Tanzania kuhusu namna ya kuzalisha zao hilo.

Gado alisema mbali na changamoto ya kuwa na mashine zilizochakaa na ubovu wa miundombinu ikiwamo barabara, bado mkulima wa Tanzania amekuwa na hali ya kuzalisha mpunga ulio bora.

"Tumeona changamoto kadha wa kadha, lakini bado mkulima huyu amekuwa akizalisha kilicho bora, tatizo ni uhakika wa soko, naishauri mamlaka husika kuangalia namna ya kuwasaidia wakulima, ili waweze kuuza kwa wingi katika nchi zinazozunguka Bara la Afrika," alisema.

Aliongeza kuwa: "Nipende pia kuwapongeza JICA kwa kuweka utaratibu wa kuongeza thamani ya zao hili, kwa kusaidia kusimamia makubaliano kati ya wanunuzi na wakulima kwa wakulima wa Tanzania kupitia kwenye mradi wa TANRICE, kwa kuwa umekua mkombozi kwa wakulima wengi hususani waliopo kwenye skimu ya Lower Moshi," alisema.

Awali akizungumza wakati wa mafunzo hayo ambayo yalilenga kubadilishana uzoefu na wataalamu wa kilimo nchini Tanzania, Mshauri Mkuu wa kiufundi katika mradi huo, Monitori Tomitaka, alisema wanawake ndiyo wazalishaji wakubwa wa zao hilo.

Mshauri huyo wa mradi huo ambao unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), alisema kwa mwaka 2018 Tanzania ilizalisha tani 925 kwa hekta.

"Kwa Tanzania eneo linalolima mpunga ni kilomita za mraba 945,087, niwashauri wakulima kuzingatia makubaliano wanayokubaliana na wanunuzi wa mpunga, ili thamani ya mpunga wanaozalisha izidi," alisema Tomitaka.

Naye mtaalamu kutoka nchini Tanzania, Shedrack Msemo, alitaja miongoni mwa changamoto wanazokumbana nazo wakulima kuwa ni pamoja na miundombinu mibovu ya kuingia kwenye mashamba ya wakulima, kutokuwa na mashine bora ya ukoboaji wa mpunga pamoja na mashine za kuvunia mpunga.

Shirika la JICA, linatekeleza mradi wa TANRICE 2 nchini Tanzania na PROAP nchini Msumbiji na wataalamu wamekuwa wakibadilishana ujuzi kwa lengo la kusaidia kuongeza uzalishaji.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 29, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

ALIYEKAMATWA 'AKIJIIBIA GARI LAKE' SASA ALIPWA FIDIA NONO



## Kwa nini wengi wafariki kwa kung'atwa na nyoka

Ukurasa 15



# Ukosefu chumba cha kujihifadhi watesa mabinti shuleni Bariadi

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Waandishi wa michezo mnajidhalilisha!

"HERI ya Mwaka Mpya. Pole kwa kuendelea 'kumpigia mbuzi gitaa.' Tatizo ni waziri mwenye dhamana (HSU). Yuko wapi wa kumfunga paka kengele?" (L. Muhimba, Bukoba, 0689 564 995).

Huu ni ujumbe niliotumiwa na mwenye jina hilo hapo juu akinipa pole kwa kuendelea 'kumpigia mbuzi gitaa' kama nilalamikavyo mara kwa mara kuhusu waandishi wanaopuuza ushauri unaohusu uchafuzi wa lugha adhimu (iliyo na sifa na heshima kubwa) ya Kiswahili.

Wakati ndugu Muhimba anaandika kuwa "tatizo ni waziri mwenye dhamana" na kuuliza "yuko wapi wa kumfunga paka kengele," nami nauliza: "Baraza la Kiswahili (Bakita) limevunjwa ili kubana matumizi ya serikali ya awamu ya tano au linaafiki uchafuzi wa lugha yetu ya taifa?"

Kutoka Zanzibar nilitumiwa ujumbe ufuatao: "Ni jambo la kawaida siku hizi kwa baadhi ya waandishi wa habari, hasa wale wasiofundishika (wa michezo) kutuandikia; 'siku ya jana', 'siku ya leo' n.k.

"Je, kuna haja gani ya kuandika hivyo wakati neno 'jana', 'leo' na kadhalika yanawakilisha siku husika? Kwa maoni yangu huu ni upotoshaji wa matumizi ya maneno ya Kiswahili. Unalionaje jambo hilo? Tuendelee kuelimishana." (Kissiwa, Zanzibar 0713 768 335).

Pamoja na matumizi mabaya ya maneno ya Kiswahili, sasa hata sentensi zaandikwa shelabela (bila utaratibu; ovyo). Pia ni kama waandishi wanashindana kutumia maneno yenye maana tofauti na maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) yake huku wakichanganya na Kiingereza ilhali yamo ya Kiswahili yanayokidhi (kitendo cha kutosheleza makusudio) haja!

Mfano wa malalamiko ya ndugu Kissiwa ni huu ulioandikwa na gazeti la michezo wakati wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kule Zanzibar:

"Yanga kabla ya mechi za jana Jumapili ilikuwa nafasi ya tatu katika msimamo wa Kundi B ikifikwa na alama tatu, ikizidiwa ujanja na vinara Azam na Malindi ambazo kila moja ina alama nne baada ya kushuka uwanjani mara mbili na leo Jumatatu usiku wanacheza na Malindi kabla ya kumalizana na Jamhuri kesho kutwa Jumatano hii." (Maneno 55 katika sentensi moja)!

Mwandishi alikuwa na sababu gani kuandika " ... jana Jumapili ....," " ... leo Jumatatu," na " ... kesho kutwa Jumatano?" Hilo ni gazeti lililoandikwa Jumapili kwa ajili ya kusomwa kesho (Jumatatu). Mwandishi hakuwa na sababu ya kuandika 'jana' na kuongeza neno 'Jumapili' kwani msomaji anajua ni moja ya matukio ya mechi za jana (Jumapili) hivyo anasoma gazeti lililoandika habari za jana (Jumapili) na kusomwa leo (Jumatatu).

Ingeandikwa: "Kabla ya mechi za jana, Yanga ilikuwa ya tatu na alama tatu kwenye kundi B nyuma ya Azam na Malindi zenye alama nne kila moja kwa kucheza mechi mbili mbili. Leo usiku itacheza na Malindi na Jumatano na Jamhuri." (Maneno 39 katika sentensi mbili).

"Rooney akamatwa uwanja wa ndege akiwa chakali" ni kichwa cha habari za michezo. Kama waandishi wetu Kiswahili kinawashinda, wataweza Kiingereza? 'Chakali' maana yake nini? Hapana shaka mwandishi alikusudia neno 'chakari' lenye maana mbili. Kwanza ni mtu anayefanya kazi ya kunyonga waliohukumiwa kifo. Kwa muktadha huu, 'chakari' ni 'chicha' yaani kupita kiasi, chopi: amelewa chakari. Kwa hiyo 'chakali' halina maana yoyote kwa Kiswahili!

"Kwa hii Yanga! Simba inasubiri." Hiki ni kichwa cha gazeti la michezo kinachoonesha ushabiki wa mwandishi. Simba inasubiri kitu gani? Habari yenyewe imeandikwa: "Ni kweli Yanga imekuwa ikitegemea bakuli la mashabiki wake kuendesha baadhi ya mambo, huku kocha wake, Mwinyi Zahera kuna wakati akijipapasa mfukoni ili kuokoa jahazi, lakini asikuambie mtu, jamaa wamefunika mbaya."

Sentensi ilivyoandikwa haieleweki. Ingeandikwa: "Yanga inategemea msaada wa wanachama na mashabiki wake kujikongoja (kitendo cha kumsaidia mtu kama vile mgonjwa au mzee kwenda) huku kocha wake, Mwinyi Zahera akiisaidia kwa fedha zake." Nimeshindwa kuelewa maana ya " ... jamaa wamefunika mbaya" kwani haielezwi kilichofunikwa ni kitu gani. Huu ni uandishi wa kihuni!

"Ndio, katika Ligi Kuu, licha ya kuongoza kileleni, lakini Yanga pia inaongoza kwa kuwa na jezi nyingi ilifanya kufuru kwa kubadilisha uzi karibu kila mechi na hasa michuano tofauti." Sentensi imevurugwa kutokana na ushabiki wa mwandishi! Ingeandikwa:

"Licha ya Yanga kuongoza katika Ligi Kuu, pia huvaa jezi tofauti kila mechi." Hili la kubadilisha 'uzi' kila mechi siliafiki kwani maana ya 'uzi' ni ugwe mwembamba unaotokana na vitu kama pamba au hariri unaotumika kwa kushonea au kufumia. Hakuna timu yoyote duniani inayovaa 'uzi' bali huvaa jezi, yaani vazi rasmi la michezo linalovaliwa na timu nzima lakini si 'uzi' kama alivyoandika mwandishi kama waandikavyo wenzake 'uzi' badala ya jezi!

Aidha sioni 'kufuru' iliyofanywa na Yanga kwa kubadili jezi kila inapocheza na timu tofauti uwanjani. Maana ya 'kufuru' ni kitendo cha kusema au kutenda jambo lilolo kinyume na dini. Kitendo cha kumkana Mungu. Je, kubadili jezi kwa kila mchezo ni kumkufuru Mungu? He! Ina maana wanaobadili nguo kila siku wanamkufuru Mungu?

Mwandishi anaendelea: "Hata huku Unguja, wababe hao wakishiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi bado imetisha kwa kutinga ikiwa na seti nne za jezi na tayari mbili imeshatumia katika mechi zao dhidi la KVZ na Azam." Kama ndivyo waandishi wanavyofundishwa siku hizi, basi hatuna walimu stahiki bali wababaishaji!

'Wababe' ni watu wanaotumia nguvu kuwaonea wengine. Yanga ni wababe au wamepewa jina hilo kwa sababu anazojua mwandishi?

**Methali: Akipenda, chongo huita kengeza.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

# IFAHAMU MAMLAKA YA UPEKUZI

UPEKUZI ni kitendo cha kuingia aidha maungoni kwa mtu, ndani ya nyumba au kwenye makazi ya mtu kwa nia ya kutafuta kitu, vitu vilivyofichwa au vitu ambavyo vinahusiana na kosa la jinai na kwamba kitu au vitu hivyo vinaweza kusaidia katika upelelezi wa polisi, au katika kesi inayoendelea mahakamani kama sehemu ya ushahidi wa kuthibitisho au kukanusha kosa linalojadiliwa.

Upekuzi unaweza kufanyika kwa namna mbili, kwa kutumia hati ya upekuzi au upekuzi unaofanyika bila hati ya upekuzi kulingana na mazingira husika.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu cha 24 kinampa mamlaka na uwezo Ofisa wa Polisi kufanya upekuzi maungoni mwa mtu yeyote aliyemkamata na upekuzi huo unafanyika mara baada ya mtu kukamatwa na kuwa chini ya ulinzi.

Sheria hiyo pia, inampa uwezo wa kuchukua toka maungoni mwa mtu huyo kitu chochote cha hatari au kitakachosaidia upelelezi wa tuhuma zilizosababisha kukamatwa.

Aidha, sheria hiyo imetoa umuhimu wa kipekee kwa wanawake pale tendo la upekuzi linapotakiwa kufanyika dhidi yao. Aidha, iwe maungoni au hata kwenye makazi yake.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kifungu cha 26 kinatoa ufafanuzi wa jinsi mwanamke atakavyopekuliwa, kwamba upekuzi huo lazima ufanywe na polisi mwanamke au mwanamke yeyote ambaye anaaminika.

Mambo muhimu yakuzingatiwa katika upekuzi, kulingana na unyeti wa tendo la upekuzi, ni vyema kabla na baada ya upekuzi kufanyika ofisa wa polisi au mtu mwingine anayefanya upekuzi akawa na mashahidi wa kushuhudia upekuzi huo. Ni haki ya msingi kwa mmiliki wa nyumba, jengo au eneo linalotakiwa kupekuliwa kuonyeshwa na kuona hati inayoidhinisha upekuzi, pia ni muhimu mashahidi waione hati hiyo kabla ya utaratibu wa upekuzi kuanza.

Aidha, jamii na wananchi kwa ujumla wana haki ya kutambua mamlaka zilizopewa uwezo wa kuidhinisha upekuzi, ambazo ni Mkuu wa Kituo cha Polisi na Hakimu.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, inampa uwezo na mamlaka Ofisa wa Polisi ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Polisi (OCS), anapokuwa amepokea taarifa za kuaminika kwamba ndani ya nyumba, jengo au eneo fulani au kwenye chombo cha usafiri kuna vitu ambavyo anavitilia shaka ambavyo kwa sababu ya msingi vinasadikiwa kutumika kutenda kosa.

Mkuu wa Kituo anaweza kuidhinisha upekuzi kama anaamini kwamba ucheleweshaji wowote wa kufanyika upekuzi unaweza kusababisha utoroshwaji au uharibifu wa kitu au vitu vinavyotafutwa au vinavyoweza kuhatarisha maisha ya binadamu au mali.

Kwa upande wa hakimu naye anauwezo na mamlaka ya kuamuru upekuzi ufanyike kwenye nyumba, jengo au eneo lolote baada ya kupokea malalamiko au taarifa za kuaminika kwamba kwenye nyumba, jengo au eneo fulani kuna kitu au vitu visivyo halali au vielelezo muhimu. Amri hii hutolewa kwa maandishi na hujulikana kama hati ya upekuzi.

Pia kifungu cha 43 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinampa uwezo Ofisa wa Polisi kuvunja na kuingia kwenye nyumba au jengo au mahali popote kwa madhumuni ya kufanya upekuzi, iwapo patakuwa pamefungwa na mmiliki anakataa kutoa idhini baada ya kuonyeshwa hati ya kuamuru upekuzi ufanyike.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inampa uwezo Ofisa wa Polisi kufanya upekuzi kwa dharura kwenye nyumba, jengo au mahali popote endapo anazo sababu za msingi za kutaka kufanya upekuzi wa dharura.

Upekuzi wa dharura utafanyika bila hati ya kuidhinisha upekuzi yaani search order au search warrant. Upekuzi huu hufanyika baada ya mazingira kulazimu uharaka na kwamba kutokufanya hivyo kutasababisha uharibifu au utoroshwaji au kitu au vitu au mtu anayetafutwa kuhusiana na shaka au tuhuma.

Ni vizuri jamii ikaelewa kuwa, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai haitamki saa ya kufanya upekuzi, ila inasema upekuzi utafanyika kuanzia mawio hadi machweo ya jua na chini ya kifungu cha 42 upekuzi unaweza kufanyika hata usiku.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

UTAFITI

# Kwanini wengi hufariki kwa kung'atwa na nyoka?

MAELFU ya watu duniani hufariki kila mwaka kutokana na sumu kali ya nyoka baada ya kung'atwa.

Ukosefu wa matibabu na hata mwathirika kupewa matibabu yasiyofaa, hufanya vifo hivyo visikingike.

Kung'atwa na nyoka huenda kusionekane kuwa janga baya la kiafya. Lakini katika maeneo mengine duniani ni hatari ya kila siku inayosababisha maafa ama hata kubadilisha maisha ya mtu.

Kuna tatizo la waathirika kutopatiwa dawa kwa wakati unaofaa na katika matukio mengine, hupewa dawa ili kutibu jeraha lililosababishwa na nyoka tofauti.

TAKWIMU

Takriban watu 11,000 hudaiwa kufariki kila mwezi kutokana na kung'atwa na nyoka, ikiwa ni sawa na idadi ya watu waliofariki kwa ugonjwa wa ebola kati ya mwaka 2014 hadi 2016.

Aidha, kiasi cha zaidi ya watu 450,000 kwa mwaka wanadaiwa kupata majeraha yanayobadili maisha yao kama vile kukatwa mguu ama hata kupata ulemavu mwingine wa maisha.

Kiwango hicho cha matatizo kinamaanisha kwamba majeraha yanayosababishwa na kung'atwa na nyoka, inabidi sasa yapewe kipaumbele baada ya kusahaulika kwa muda mrefu.



Watoto wanaoelekea shule huenda wako hatarini pia. **PICHA: MTANDAO**

**HALI ILIVYO**

Katika maeneo yaliyoendelea kama vile Ulaya, Australia na Marekani Kaskazini, ni watu wachache wanaofariki kutokana na majeraha ya kuumwa na nyoka, licha ya kuwa na nyoka wengi tofauti wenye sumu kali zaidi.

Hiyo ikilinganishwa na vifo 32,000 katika eneo la Jangwa la Sahara na mara mbili ya Kusini mwa Bara la Asia.

Jamii nyingi zilizopo maeneo ya tropiki ziko katika hatari ya kung'atwa na nyoka porini, zikiwa zinatembea na hata usiku zikiwa zimelala nyumbani kwao.

Wakulima vijana ndio walio katika hatari kubwa zaidi, wakifuatiwa na watoto.

Sasa wakati idadi kubwa ya watu wanaoishi mashambani wakiwa hatarini, mbinu za kiafya zinazotumiwa katika maeneo ya bara la Afrika na Asia, haziwezi kukabiliana na janga hilo.

Mafunzo ya kliniki, usafiri wa dharura na dawa za bei nafuu huwa hayapatikani katika maeneo hayo pale mtu anapoumwa na nyoka.

MUHIMU

Kung'atwa na nyoka kunasababisha dalili zinazoweza kuhatarisha maisha ya mtu ikiwamo kutokwa na damu, kupooza na uharibifu wa tishu zisizoweza kurekebishwa.

Ni muhimu kwa waathiriwa wa majeraha ya nyoka kupata dawa zinazohitajika haraka iwezekanavyo baada ya kuumwa.

> Hii inamaanisha kwamba idadi ya chupa za dawa zinazohitajika ili kufanikiwa kutibu mgonjwa zinaongezeka kutoka 10 hadi 20 ama hata 30.

Antivenom ama dawa ya kukabiliana na sumu ya nyoka ndiyo inayohitajika kutibu majeraha ya kung'atwa na nyoka.

Dawa hiyo hutengenezwa kwa kutumia sumu ya nyoka aliyesababisha jeraha.

Hatua hiyo inamaanisha kwamba dawa tofauti inahitajika, kwa sababu kuna nyoka wenye sumu kali tofauti kama vile, koboko, swila na kifutu kwa uchache.

Sumu zinazopatikana katika sumu hiyo ya nyoka huwa tofauti kutokana na maeneo.

Hiyo inamaanisha kwamba dawa ya kutibu majeraha ya kuumwa na nyoka ni ngumu kupatikana na inaweza kuwa ghali mno.

**JINSI DAWA ZA SUMU YA NYOKA ZINAVYOUNDWA**

Kiwango kidogo cha sumu ya nyoka hudungwa katika mnyama kama vile farasi ama punda.

Hatua hiyo huchochea kinga ambayo hupigana na sumu hiyo ndani ya mwili wa mnyama.

Kinga hiyo hutolewa katika damu ya wanyama hao, kusafishwa na kufanywa kuwa dawa ya kukabiliana na sumu hiyo.

Dawa hizo zinapaswa kutumiwa hospitalini, kwa kuwa huwa na madhara makali kwa mgonjwa.

Katika maeneo ya Latin Amerika, dawa za kukabiliana na sumu kali ya nyoka hutengenezwa na kugharamiwa na serikali.

**VIFO**

Viwango vya vifo viko juu katika maeneo ya Jangwa la Sahara barani Afrika, ambapo dawa ya kukabiliana na sumu ya nyoka huuzwa kwa kati ya $140 hadi $300 (Sh. 321,160 hadi Sh. 688,200) kwa chupa, huku kati ya chupa tatu hadi 10 zikihitajika kuokoa maisha ya mwathiriwa.

Kwa mkulima wa Kiswazi anayepokea mshahara wa $600 ama Sh. 1,376,400 kwa mwaka, hawezi kugharamia dawa hiyo.

**DAWA HAFIFU**

Kutokana na ughali huo, kumesababisha kutengenezwa dawa hafifu ama zile zisizo sahihi katika soko, katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, hususan barani Afrika.

Dawa hizo huuzwa kwa dola 30 kwa chupa sawa na Shilingi 68,830.

Bidhaa hizo zilianza kutumika kwenye hospitali katika maeneo mbalimbali ya bara Afrika.

Hata hivyo, kuna ripoti nyingine kwamba baadhi ya dawa hizo huenda hazina uwezo wa kutibu sumu ya nyoka.

Tafiti ndogo ndogo kutoka hospitalini nchini Ghana na Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), zinasema kuwa wakati dawa hizo za bei rahisi zilipotumiwa vifo viliongezeka kutoka asilimia 2 hadi asilimia 10.

Mara nyingi dawa hizi za nyoka hutengenezwa kwa kutumia sumu za nyoka kutoka maeneo tofauti, ikilinganishwa na mahali ambapo dawa hizo huuzwa.

Kwa mfano dawa ya nyoka iliyoundwa na sumu ya nyoka wa India, inauzwa Afrika.

Nyingine hutengezwa kwa kutumia sumu sahihi, lakini ikiwa na kiwango kidogo cha kinga mwilini, hatua inayofanya dawa hiyo kuwa hafifu kutibu mtu aliyeng'atwa.

Hii inamaanisha kwamba idadi ya chupa za dawa zinazohitajika ili kufanikiwa kutibu mgonjwa zinaongezeka kutoka 10 hadi 20 ama hata 30.

**UKOSEFU WA MAJARIBIO**

Matatizo haya yamesababishwa na ukosefu wa kufanyia majaribio dawa hizo. Dawa nyingi lazima zifanyiwe vipimo ili kuthibitisha zinaweza kutibu. Lakini hili halifanyiki kwa dawa za kutibu sumu ya nyoka.

Mamlaka ya kusimamia dawa mara nyingi huidhinisha dawa hizi bila kuwa na ushahidi wa zipi zinaweza kutibu ama hata kulinganisha na matibabu mengine.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, Shirika la Afya Duniani (WHO) limezindua mpango wa kujaribu dawa hizo huku matokeo yake yakitarajiwa kuchapishwa baadaye mwaka huu.

Mpango huo utaruhusu wizara za afya, wauzaji dawa kuelewa ni dawa gani za kukabiliana na sumu ya nyoka zinazohitajika katika maeneo yao, mbali na kutafuta watengenezaji wanaoweza kutengeneza dawa hizo kwa bei rahisi. **BBC**

ELIMU

NA HAPPY SEVERINE, SIMIYU

# Ukosefu chumba cha kujihifadhi watesa mabinti shuleni Bariadi

HAWA Hussein (17) ni mwanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kidinda, Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu.

Anasema anakerwa na changamoto ya kukosekana kwa chumba cha kubadilisha taulo za kike (changing room) wakati binti anapoingia kwenye hedhi shuleni kwake.

Hawa anabainisha kwamba changamoto hiyo imewafanya wanafunzi wengi wa kike washindwe kufuatilia masomo yao vizuri, pindi wawapo katika siku zao kwa sababu ya kukosa vyumba maalumu vya kubadilishia taulo.

Anaongeza kwamba changamoto hiyo inawafanya wengi waamue kutoroka shule ili kutafuta sehemu stahiki za kujistiri.

Anabainisha kuwa pamoja na changamoto hiyo ya vyumba, wanalo pia tatizo la kupata hizo taulo kutokana na hali halisi ya uchumi duni wa familia zao.

Kwa mujibu wa maelezo yake, tangu aanze kupata hedhi mzazi wake hajawahi kumnunulia taulo hizo kutokana na pato dogo alilonalo na mara nyingi anatumia kitambaa cha kanga kujistiri.

"Tangu nianze kuona siku zangu za hedhi, sijawahi kutumia taulo za kisasa... huwa natumia vitambaa vya kanga," anasema na kuongeza:

"Huko nyuma niliwahi kutumia manyoya ya ngozi ya kondoo lakini yaliniumiza sana na kuniwasha, hivyo sasa nimebaki kutumia kitambaa cha kanga kujistiri."

Hawa anasimulia kuwa hata mama yake mzazi anatumia vitambaa vya kanga, na kwa hali hiyo ni ngumu kwake kununuliwa taulo za kisasa na wazazi wake kwa sababu hali ya uchumi hairuhusu.

"Na ndiyo maana huwa natoroka shule wakati wa hedhi na kwenda nyumbani kwa kuwa nashindwa kuvumilia kukaa muda mrefu na kitambaa hicho," anasema na kuongeza:

"Kwa kweli huwa nateseka sana wakati wa hedhi kwa sababu wakati mwingine hujikuta nachafua sketi, hali ambayo hunifanya nishindwe kunyanyuka mpaka pale wanafunzi wenzangu wanapokwenda mapumziko."

Hawa anasema suala la hedhi bila kuwa na taulo za kike pamoja na chumba cha kujistiri ni kazi bure, kwani uwezo wa kununua taulo za kike kwa walio wengi haupo.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kidinda, iliyoko wilayani Bariadi, mkoani Simiyu. **PICHA ZOTE: HAPPY SEVERINE**



Hawa Hussein (17), mwanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kidinda, Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu.



Ofisa Elimu, Afya na Mazingira wa Mkoa wa Simiyu, Juslin Gilbert

"Tunatoka familia duni, na hata zile taulo zinazowekwa shuleni hatugawiwi kila siku, huwa ni za dharura tu na hutolewa kipande kimoja pindi mwanafunzi anapopata dharura ya kuchafuka," anasema.

**JUDITH**

Judith Issa (12), anasoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Somanda B.

Kwa upande wake anasema suala la vyumba maalumu vya kubadilishia taulo za kike ni changamoto shuleni kwao kwa kuwa vyumba hivyo havipo.

Anatanabaisha jambo hilo kupewa kipaumbele zaidi ili hatimaye pawe na chumba hicho kumpa mtoto wa kike nafasi ya kubadilisha taulo hizo.

"Kwa mtazamo wangu, endapo vyumba hivyo havitajengwa, ni dhahiri watoto wa kike hawatafikia malengo yao kimasomo, kwa kuwa wengi wataendelea kutoroka wakati wa siku zao na hivyo kupitwa na baadhi ya masomo shuleni," anasema.

**MBADALA**

Judith anatoa rai kwamba shule, serikali na wadau kwa ujumla kuja na suluhisho mbadala la kukosekana kwa chumba maalumu cha kubadilishia taulo wanafunzi.

Anabainisha mbadala huo ni ule wa kuwa na choo ambacho kina miundombinu ya kuhifadhi taulo, kinachoweza kutumiwa na wanafunzi wakati wa hedhi.

Anasema mazingira rafiki ya kuwa na chumba pamoja na taulo za kike na maji, kutawasaidia sana watoto wa kike wasione hali hiyo kama ni adhabu.

"Wataoona hedhi ni jambo la kheri katika maumbile ya kila mwanamke," anasema.

**BAHATI MASUNGA**

Naye Bahati Masunga, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Dutwa, wilayani Bariadi, anasema mbali na shule nyingi kuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vyumba vya kubadilishia taulo, bado pia zina changamoto zingine.

> "Serikali za vijiji zihusike kuwaelimisha wazazi na jamii kuchangia mahitaji maalumu ya shule likiwamo hilo la vyumba vya kubadilishia ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki,"

"Zina changamoto za ukosefu wa maji ya uhakika na miundombinu rafiki kwa mabinti," anasema na kuongeza:

"Suala la maji kwa mfano ni muhimu katika matumizi mazima ya taulo ili kumfanya mtoto wa kike awe katika hali nzuri zaidi, aweze kujisafisha pindi achafukapo."

Bahati anasema, ubadilishaji wa taulo hauna budi uambatane na maji ili kumkinga mtoto wa kike na maradhi.

**MDAU WA ELIMU**

Mdau wa elimu anayefanya kazi na Mpango wa Kuinua Ubora wa Elimu nchini (Equip), Bakari Geni, anasema kuna madhara makubwa kwa watoto wa kike pale wanapokosa mahitaji muhimu ya hedhi na chumba cha faragha.

Geni anataja madhara hayo kuwa ni pamoja na wanafunzi kutoroka shule na hivyo kukosa baadhi ya vipindi.

"Kuna vyumba vichache vya faragha kwenye shule nyingi wilayani Bariadi... vingine havijakamilika na wala havina vifaa muhimu, yakiwamo maji," anasema.

Aidha, Geni anasema kwamba hata kwa baadhi ya shule zilizojitahidi kutekeleza agizo la wizara la kujenga vyumba hivyo, bado hazikufuata miongozo elekezi.

"Vyumba hivyo vimekuwa vikijengwa nje au pembeni mwa vyoo vya shule," anasema.

**WAZAZI WACHANGIE**

Geni anasema serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha miundombinu ya elimu, hivyo ni vema wazazi wakahusishwa na kuelimishwa juu ya kuchangia mahitaji muhimu ya watoto wao ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya faragha na kuchangia vifaa vyake.

"Serikali za vijiji zihusike kuwaelimisha wazazi na jamii kuchangia mahitaji maalumu ya shule likiwamo hilo la vyumba vya kubadilishia ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki," anasema.

Hedhi salama kwa wanawake, na hasa wanafunzi ni miongoni mwa masuala yanayofanyiwa kampeni kubwa nchini na katika nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Lakini kampeni hizo zinakabiliwa na vikwazo vingi ambavyo visipotafutiwa ufumbuzi, huenda juhudi zote hizo zisizae matunda kusudiwa na zikasababisha maumivu makubwa kwa watoto wa kike.

**UTAFITI**

Utafiti wa mwaka 2010 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) unaonyesha kuwa kati ya wanafunzi wa kike 10 barani Afrika, mwanafunzi mmoja hutoroka shule wakati wa kipindi chake cha hedhi.

**TGNP**

Na utafiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) unaonyesha kuwa wanafunzi wa kike wamekuwa wakitoroka shule kwa siku 60 kwa mwaka pindi wanapokuwa kwenye hedhi.

Haya yanatokea pamoja na Malengo Namba Nne na Tano ya Malengo Endelevu ya Dunia (SDGs) kusisitiza kuwapo kwa elimu bora inayotolewa kwa usawa.

Kwa kiasi kikubwa malengo hayo yanalenga kuweka usawa katika utoaji elimu ya msingi kati ya wavulana na wasichana. Hata hivyo, ni nchi chache tu ndizo zilizoyafikia malengo hayo katika ngazi zote za elimu.

**MWALIMU**

Mwalimu wa Afya wa Shule ya Msingi Somanda A, Anna Masale, anasema huduma ya maji ni muhimu katika hedhi salama kwa kuwa wapo wanafunzi ambao hukumbwa na hali hiyo wakiwa shuleni, hivyo ni lazima wapate maji ya kujisafisha.


**OFISA ELIMU**

Ofisa Elimu, Afya na Mazingira wa Mkoa wa Simiyu, Juslin Gilbert, anasema kumekuwapo na jitihada kwa baadhi ya shule wilayani humo kutenga asilimia ya fedha za ruzuku kutoka serikalini (capitation grant) kwa ajili ya kuwahudumia wanafunzi wa kike.

Anasema shule zinachukua hatua hiyo kutokana na agizo la serikali linalowataka wafanye hivyo.

"Ingawa mpaka sasa utekelezaji wa agizo hilo bado ni changamoto, tayari mwongozo umekwishatolewa na ni lazima lifanyiwe kazi," anasema.

JIELIMISHE



Chombo cha Change-4 kutoka China kikiwa mwezini. **PICHA: MTANDAO**

# Mmea uliopandwa mwezini na Change-4 sasa wanyauka

MMEA uliopandwa na wanaanga wa China mwezini, umechukua takriban siku nane kuota, lakini sasa umekauka.

Chombo cha angani kutoka China kwa jina la Change-4, kiliacha kunyunyizia maji mbegu hiyo ya pamba kama ilivyopangwa na Chuo Kikuu cha Chongqing, ambacho kilitunga jaribio hilo.

China ilipanda mmea wa kwanza mwezini umuhimu ukiwa ni kuendelea na uchunguzi angani.

Mmea huo uliota katika chombo ndani ya Change-4 ambacho kilitua katika eneo la mbali la mwezini Januari 3 mwaka huu.

Eneo ambalo mmea huo ulikuwa umepandwa usingeweza kuishi katika usiku wa mchana kufuatia tukio la kupatwa kwa mwezi (Lunar Eclipse).

Kwa wakati huo wote, ujumbe wa China ulilazimika kulala na mifumo yao yote ililala ili kuhifadhi kawi.

Hivyo basi, mmea huo haukunyunyiziwa maji na hatimaye kulazimika kufa kama ilivyokuwa imepangwa.

**MAJARIBIO MENGINE**

Chombo hicho cha China pia kilibeba mbegu za viazi na arabidopsis, mmea kutoka kwa jamii ya haradali pamoja na matunda na mayai ya chuchu.

Ilitarajiwa kuwa nyuzi joto duniani zitashuka hadi vipimo vya 52 ili viumbe hao wagande, chuo hicho kilisema katika taarifa Jumane iliyopita.

Wakati nyuzi joto zinapoanza kupanda mwezi ujao, viumbe vitaruhusiwa kuota katika chombo kilichozibwa.

"Hata hivyo, baadhi ya matokeo yalishangaza matarajio yetu," anasema mtunzi wa jaribio hilo, Xie Gengxin, katika runinga ya China.

Uwezo wa kupanda mimea mwezini ni muhimu katika uchunguzi wa siku zijazo angani na hasa kwa ziara kama ile ya sayari ya Mars, ambayo itachukua takriban miaka miwili na nusu kuwasili inakoenda.

Hiyo, itamaanisha kwamba wanaanga wataweza kupanda vyakula vyao angani, na hivyo kupunguza haja ya kurudi duniani ili kubeba chakula zaidi.

KWA NINI UTAFITI WA MWEZINI

Kimsingi, kuna hamu kubwa katika suala la kuutumia mwezi kama kituo hususani kwa safari za kuelekea sayari ya Mars kwa kuwa ni karibu na dunia, anasema Watson Katika utafiti uliochapishwa kwenye jarida Ingo wa lishe bora duniani, basi ni vizuri wajaribu kuukaribia.

**BBC**



UTAFITI

# Utafiti wabainisha vigezo vya waajiri mwaka 2019

## ■ Mchanganyiko wa ujuzi, yaani ubunifu, ushawishi...

KILA mwaka watu hujiwekea maazimio mapya kwa lengo la kujiimarisha katika nyanja tofauti maishani.

Wengine wanapotafuta kazi, wale walio na kazi wanatafakari ni jinsi gani wanaweza kujiendeleza katika taaluma zao.

Ili kutoa mwongozo kwa watu wanaotafuta kazi, watafiti kutoka Baraza la Kiuchumi Duniani, waliamua kulivalia njuga suala hilo.

Katika ripoti yao mpya kwa jina 'Hatima ya Baadaye ya Kazi', wataalamu wa baraza hilo walijaribu kuunganisha teknolojia mpya na zile zinazojitokeza ili kutathmini kiwango cha juu cha ufanisi kazini.

Lengo lao lilikuwa kuelewa uwezo wa teknolojia mpya katika mpango wa kuunda ajira mpya na kuboresha kazi za kampuni za uzalishaji.

Matokeo yaliyotokana na uchambuzi kutoka kwenye tovuti ya mtandao wa LinkedIn, yamebaini kuwa waajiri wa mwaka 2019 wanatafuta mchanganyiko wa ujuzi pamoja na ubunifu.

Baadhi ya ujuzi unaotafutwa na waajiri mwaka huu ni pamoja na ule wa "Kujiimarisha kiujuzi katika kazi husika, na kuhakikisha mhusika anakwenda na wakati," anaandika mhariri wa LinkedIn, Paul Petrone katika blogu moja.

### MCHANGANYIKO WA UJUZI

Pamoja na kukua kwa sekta ya viwanda, waajiri wanatafuta mchanganyiko mkubwa wa ujuzi.

Huku teknolojia ikiendelea kuimarika, inatoa nafasi mpya za kazi zinazohitaji ujuzi wa hali ya juu.

Hali hiyo inaleta ushindani unaofanya kazi zingine kupitwa na wakati.

Ujuzi wa hali ya juu pia umekuja na mahitaji ya mbinu madhubuti ya kuhifadhi data kutokana na kuimarika kwa teknolojia ya digitali duniani.

Mbali na ubunifu, LinkedIn inasema kuwa ujuzi mwingine kama vile ushawishi, ushirikiano, uwezo wa kumudu mazingira tofauti ya kazi na kuzingatia muda wa kazi ni muhimu.

Watafiti walichunguza iwapo kuna uwezekano wa vigezo hivyo kubadilika siku zijazo wakizingatia vigezo hivyo.



Wafanyakazi katika majukumu yao. **PICHA: MTANDAO**

### VIGEZO 5 VINAVYOLENGWA NA WAAJIRI MWAKA 2019

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na mtandao wa LinkedIn unaowaleta pamoja waajiri na waajiriwa, hivi ndivyo vigezo vitano vinavyolengwa na waajiri mwaka 2019.

Navyo ni ubunifu, ushawishi, ushirikiano, kumudu mazingira tofauti ya kazi na usimamizi wa muda.

### UJIO WA ROBOTI

Kwa mujibu wa utafiti, suala la kuimarika kwa ujuzi bado linayumbayumba kutokana na teknolojia kubadilika mara kwa mara. Hii inamaanisha teknolojia ikibadilika, ujuzi mpya unahitajika kufanya kazi husika.

Inakadiriwa kuwa nusu ya wafanyakazi watalazimika kutafuta upya ujuzi, la sivyo watapoteza nafasi zao za kazi miaka michache ijayo.

Watunzi wa sera sasa hawana budi kubuni mbinu mbadala ya kukabiliana na mabadiliko yanayoshuhudiwa katika sekta ya ajira.

"Mabadiliko yanayoshuhudiwa katika sekta ya ajira kwa sasa yatatimua wafanyakazi wengine, huku ikibuni fursa mpya za kazi kwa wengine," inasema ripoti hiyo.

Moja ya changamoto wanazokutana nazo watu wanaotafuta kazi ni kutokufahamu waajiri wanataka nini.

Hali hiyo huwafanya kutoa taarifa zisizo sahihi au zisizohitajika kwenye usaili.

Kujua nini waajiri wanatafuta kwenye usaili humsaidia msailiwa kuandaa taarifa zilizo sahihi kumwezesha kushinda usaili.

Unapoitwa kwenye usaili, inamaanisha kuwa umeshafikia vigezo vya kupewa kazi kwa kuzingatia taarifa za awali ulizotoa kupitia wasifu na barua ya kuomba kazi.

### WAAJIRI WANATAFUTA SIFA ZIPI?

### KUJIAMINI

Hili ni suala muhimu sana katika utendaji wa kazi. Wasailiwa wengi huonyesha uwoga na wasiwasi hata kabla hawajaanza kujibu maswali.

### UBUNIFU

Taasisi nyingi zinakumbana na changamoto ya ushindani, hivyo waajiri hupenda kuajiri watu wenye sifa ya ubunifu.

### UJUZI NA UWEZO WA KUFANYA KAZI HUSIKA

Ufaulu unaoonekana kwenye vyeti, hautoshi kuthibitisha kuwa msailiwa anafaa kwenye nafasi aliyoiomba. Ujuzi na uwezo wa kazi hutathminiwa kupitia uzoefu alionao msailiwa.

### TAARIFA KUHUSU NAFASI UNAYOTARAJIA KUPEWA

Ni muhimu kufanya utafiti juu ya taasisi kabla ya kwenda kwenye usajili. Mara nyingi taarifa hizi hupatikana kwenye tovuti ya taasisi husika na kupitia watu wanaofanya kazi na taasisi hiyo.

### UJUZI KATIKA MAWASILIANO

Kubaini kama una uwezo mzuri katika kuwasiliana, wasaili huangalia matumizi ya lugha katika kujibu maswali; hii hujumuisha matumizi sahihi ya maneno, matamshi na lugha ya mwili kama kutumia mikono na mwonekano wa sura.

Vigezo vingine ni pamoja na:

### MATARAJIO YENYE UHALISIA

Ni dhahiri kuwa hakuna mwajiri atakaye kuajiri kama hana uwezo kufikia matarajio yako. Hii inajumuisha matarajio ya kiwango cha mshahara; kama utataja mshahara mkubwa ambao taasisi itashindwa kukulipa inaweza ikawa sababu ya kukosa ajira.

### KUMUDU MAZINGIRA TOFAUTI YA KAZI

Ufanisi na tija kazini hutegemea uwezo wa mfanyakazi kuweza kumudu mazingira tofauti tofauti ya kazi.

### KITU CHA ZIADA UTAKACHO ONGEZA KWENYE TAASISI

Mara nyingi waajiri hawapendi kumpa kazi mtu wa kawaida. Kando na uwezo wako wa kufanya kazi ni nini cha ziada utakachokiongeza kwenye taasisi au kazi husika.

### UTAYARI WA KUJIFUNZA

Ni vyema katika maelezo yako kuonyesha kuwa unapenda kujifunza na uko tayari kuongeza ujuzi wako pale fursa itakapopatikana.

### UWEZO WA KUJITAMBUA

Uwezo wa kujifanyia tathmini na kujua sifa ulizonazo ikiwamo udhaifu ulionao unaweza kusaidia kutoa taarifa zitakazoonyesha kuwa unajitambua.

**BBC**

JE, WAJUA?

# Aliyekamatwa 'akijiibia gari lake' sasa alipwa fidia nono

MTU mmoja ambaye alitiwa nguvuni na polisi jijini Illinois, Chicago nchini Marekani, kwa wizi wa gari ambalo ilibainika kuwa ni mali yake, amefikia makubaliano ya nje ya mahakama na mamlaka za jiji kumlipa fidia.

Lawrence Crosby, alikuwa mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu cha Northwestern, akiwa na umri wa miaka 25 wakati tukio hilo lilipotokea mwaka 2015.

Mwanamke mmoja alipiga simu polisi wakati Crosby alipokuwa akirekebisha gari yake na kudhaniwa kuwa ni mwizi anayejaribu kuliiba.

Mamlaka ya Mji wa Evanston watapigia kura baadaye juu ya kiasi gani alipwe lakini wakili wake anasema itakuwa dola milioni 1.25.




Dk. Lawrence Crosby anayeripotiwa kupigwa makonde na polisi, wakati akitiwa mbaroni kwa tuhuma ya kujiibia gari yake. **PICHA: MTANDAO**

Timothy Touhy, ambaye ni wakili wa Dk. Crosby, alitaja kima hicho alipohojiwa na gazeti la Chicago Tribune.

Dk. Crosby, ambaye ni Mmarekani mweusi ameiambia CBS Chicago kuwa tukio lake litasaidia kuangazia suala la ubaguzi wa rangi nchini humo.

Mwanasheria wa jiji amenukuliwa na runinga ya ABC News akisema: "Malipo haya ya fidia ni kielelezo tu cha nia njema na si kukubali tuhuma."

Kwa mujibu wa Touhy, mteja wake alikuwa akirekebisha gari yake na kuonekana na mwanamke mmoja aliyedhani kuwa analiiba.

Alimfuatilia wakati akielekea kwenye makazi yake chuoni na kisha kuwapigia simu polisi.

Baada ya kusimamishwa na polisi alitoka kwenye gari mikono ikiwa juu, lakini polisi walimvamia wakidai hakulala chali baada ya kuamriwa kufanya hivyo.

Polisi wanadaiwa kumshambulia wakati wakimkamata.

Crosby inaripotiwa alipigwa makonde na mateke zaidi ya 10 wakati akitiwa mbaroni. Kamera ya polisi ilinasa tukio lote.

Maofisa wa polisi waligundua kuwa alikuwa mmiliki halali wa gari hilo, lakini akaendelea kumshikilia wakidai aligoma kukamatwa.

Msemaji wa polisi wa eneo hilo alitetea matumizi ya nguvu kwenye tukio hilo akidai kuwa walidhani ilikuwa ni kesi ya wizi wa gari.

Dk. Crosby aliachiwa huru na kufutiwa mashtaka yote, hata hivyo alifungua mashtaka dhidi ya jiji na polisi. **BBC**

# ELIMU

## DK. RAYMOND NUSURA MGENI



Wanachuo wakifurahia maarifa wanayopatiwa na mhadhiri wao (aliyesimama). **PICHA: MTANDAO**

# UCHAMBUZI WA KITABU;

## THE ASSIGNMENT, Powerful Secrets for Discovering your Destiny by Mike Mudrock

### ■ Kazi uliozaliwa uifanye, siri zenye nguvu za kugundua hatima yako

HUKUZALIWA kwa bahati mbaya, hukuzaliwa bure, hukuzaliwa uje uishi na usubiri ufe.

Ulizaliwa kuna kazi, kuna kusudi la kuliishi kwa uwepo wako Duniani. Ni wewe tu unaweza kufanya hili kusudi, ni wewe ndio jibu ambalo Dunia inategemea kutoka kwako.

Ni wewe ndiye mtatuzi wa matatizo ambayo Dunia inahangaika kupata mtatuzi, ni wewe umeumbwa kipekee na umezaliwa uifanye Dunia iwe sehemu salama ya kuishi pale unapoishi kazi uliyozaliwa uifanye.

Wewe ni jibu na furaha ya mtu mwingine, unavyojicheleweshа kuishi katika ulichozaliwa kwacho basi kuna mtu sehemu anateseka sababu wewe hujaamua kuishi kazi ambayo umepewa kufanya.

Usijishushe na kuona huna mchango, juwa kuwa uwepo wako ni sababu ya mtu mwingine kupiga hatua na kuona kumbe mambo yanawezekana.

Ukigundua kazi ambayo unayo Duniani na kuamua kuiishi basi unakutana moja kwa moja na utoshelevu mkubwa ndani yako.

Pia unakuwa umetimiza na kumfurahisha Mungu kwa kutii ambacho umezaliwa kukifanya na kuwa njia kwa ajili ya wengine nao wakapiga hatua na kufanikiwa.

Kazi uliyopewa ya kufanya Duniani inahitaji uwe na 'fokasi' kubwa sana (mtazamo mkubwa sana).

Kinachowakwamisha watu wengi zaidi Duniani washindwe kufanikiwa katika kazi walizopewa kuzifanya ni kupoteza fokasi kwa kuwa na mambo mengi ambayo yote wanatamani kuyafanya.

Ukiwa na mambo machache, unaipa akili utulivu na unaepuka kutawanya nguvu zako hivyo ufanisi wa kazi unaongezeka.

Muda ni fedha ya Dunia "Time is the currency of Earth". Kazi ambayo umepewa ya kufanya Duniani itachukua muda mpaka ikamilike, na kadri ambavyo utagundua mapema ulizaliwa uje kufanya nini unajipa nafasi kubwa ya maandalizi na kufanikisha mapema zaidi.

Unaona ambavyo habari itakuwa ya huzuni kuwa katika uzee wako au siku za mwisho za uhai wako ndipo unagundua ulichopaswa kufanya ni huzuni ilioje ? na hasara.


Kazi uliyopewa ya kufanya Duniani itapitia vipindi mbalimbali mpaka uone matokeo yake, hivyo juwa kuwa utapitishwa pia katika nyakati tofauti tofauti; kuna vipindi vya maandalizi, vipindi vya upweke, vipindi vya vita ya ndani na mateso, vipindi vya kujifunza, vipindi vya kutengwa, vipindi vya magumu, vipindi vya uweza wa Kiungu na vipindi vya ushindi.

Hivyo, usiogope pale ambapo umeshajitoa kuishi kazi ambayo umeitiwa na ndio sababu ya wewe ukazaliwa maana umepewa nafasi hii ni yako kuwa unaweza ukaifanya wewe na si mtu mwingine.

Kitu ambacho unakichukia sana na unakerwa nacho basi umezaliwa kukitatua kwacho na una nafasi ya kukirekebisha na sio kubaki ukilaumu sana wakati wewe ndiye umeona na uwezo wa kuchukua hatua uko katika maamuzi yako sasa.

Hasira sio kitu kibaya inategemea ni hasira gani ?. Hasira ni nishati, ni nguvu ambayo inapelekea kufanya maamuzi fulani.

> Kuna raha ya kumaliza kazi uliyopewa kuifanya duniani na hata siku unapoondoka, unaondoka tayari umemaliza kazi na kifo chako kinakuwa ni furaha sababu ya unaenda kaburini mtupu hauna ulichobakiza.




Je hasira ya kutopenda umaskini ni mbaya ?, hasira ya kutotaka ujinga ni mbaya ?. Hivyo jiulize ni eneo gani ambalo unatiwa hasira kisha chukua kazi ya kufanya na ulete majibu katika jamii.

Maumivu katika maisha yana faida maana kupitia maumivu ndipo huwa tunaanza kujifunza, ndipo ndio tunaanza kuwa wasikivu na faida ya mwisho kubwa tunatengenezwa zaidi na kuwa watu imara kupitia maumivu, maumivu ya kujenga mwili imara, maumivu ya kujisukuma kusoma vitabu na maumivu ya kujenga tabia mpya yote yapo kutusaidia kuwa watu imara na bora sana katika maisha yetu.

Utafanikiwa tu pale utakapojitoa mzima mzima juu ya kazi uliyopewa kuifanya, na kadri kazi hiyo unapoifanya ndivyo itakavyokuwa ikikifungulia maajabu na fursa nyingi sana katika maisha yako hapa Duniani.

Lipa gharama ya kujitoa kuifanya maana kwa wakati usiodhani itakuletea mafanikio makubwa.

Haitoshi kuwa na kazi isiyo na mikakati au mpango. Unahitaji kumshirikisha Mungu, unahitaji uwe na malengo madogo madogo kila siku na yasiwe kichwani ila katika maandishi na yapo katika utelekezaji.

Kuna raha ya kumaliza kazi uliyopewa kuifanya Duniani na hata siku unapoondoka, unaondoka tayari umemaliza kazi na kifo chako kinakuwa ni furaha sababu ya unaenda kaburini mtupu hauna ulichobakiza.

Je mimi na wewe siku tukiwa katika nyakati zetu za mwisho tutakuwa tayari kusema naweza kufa sasa kazi nimeimaliza ?

Kazi uliyopewa unaweza ukapoteza watu wako wa karibu, rafiki zako wote wanaweza kukukimbia na kukuacha peke yako na inaweza isieleweke lakini isiwe sababu ya wewe ukaacha kuifanya.

Mwisho usisahau hili kuwa muda wako maishani ni rasilimali ya ukomo. Pangilia saa zako 24 zenye uzalishaji, tumia kila saa vizuri kwa kujijenga kifikra, kiroho, kiujuzi, kijamii na kiuchumi.

Weka lengo lako kuu kutafuta maarifa na hekima, kazana pia kutunza afya na kubwa jikubali na jipende siku zote.

**Na Mchambuzi wa vitabu**
**Dk. Raymond Nusura Mgeni**
**2018**
**+255 676 559 211**
**raymondpoet@yahoo.com**



WADAU
SABATO KASIKA

# BAADHI ya wazazi wamekuwa wakikiuka haki za watoto wa kike kwa kuwaingiza katika ndoa ili wapate mahari.

Wadau wanasemaje?



**JAMES GAYO (MKURUGENZI WA KAMPUNI GABA AFRIKA)**

SUALA la mimba za utotoni limepata kufanyiwa tafiti nyingi zilizotoa sababu nyingi zinazochangia tatizo hilo. Wazazi kuridhia watoto wao kuolewa inaorodheshwa kama moja ya sababu.

Binafsi nadhani kuna sababu tatu zinazochangia wazazi kuridhia binti zao kuolewa mapema.

Nazo ni ufukara wa kupindukia hasa vijijini, mila zilizopitwa na wakati na mwamko mdogo kielimu kwa wazazi.


Madhara ya sababu hizi ni chimbuko la matatizo mengi mengine yanayolikabili taifa kama vile, njaa, maradhi, uharibifu wa mazingira nk.

Maadam tafiti zimekwishaainisha vyanzo hivi, ni vizuri serikali ibuni mkakati wa kukabiliana na vyanzo hivyo.

Kuwapa kifungo kikubwa wanaume wanaooa mabinti wadogo au kuwazuia mabinti wanaopata mimba kurudi shuleni hakutamaliza tatizo.

Serikali ijitahidi kuinua vipato vya wananchi hasa waishio vijijini ili familia zijitosheleze kimahitaji. Pili, serikali kama ilivyokuwa wakati wa awamu ya kwanza, ikazanie kutoa elimu za kimaendeleo katika ngazi ya familia.

Wakati wa awamu ya kwanza serikali ilifundisha watu wake kusoma na kuandika, ilifundisha elimu ya afya, usafi, lishe na stadi mbalimbali za kimaendeleo. Awamu hii ifanye hivyo pia.



**HASSAN MBILU (MWANASHERIA WA HAKI ZA WATOTO)**

KWANZA ni jambo la kusikitisha kuona mzazi anaamua kumuoza mtoto wake ili tu apate mahari kwa kigezo kwamba familia ni maskini... hili ni jambo baya sana. Mtazamo wangu ni kwamba; Kwanza kundi kubwa la watu katika jamii hawamjui mtoto ni nani kwa maana ya kisheria.

Watoto wengi wanapovunja ungo, jamii inawaona tayari wameshakuwa watu wazima na wanaweza kutoa maamuzi yao bila hata kuwashirikisha wazazi.

Hili ni tatizo kubwa, kwani watoto wengi wanaozwa na wazazi wao kutokana na kwamba wameshapata ujauzito, ambao umechangiwa na kutokuwepo kwa malezi mazuri kutoka kwa wazazi na walezi.

Watoto wengi wa kike wanaomaliza shule ya msingi huozwa hata kabla ya majibu ya mtihani wa darasa la saba.

Hii ni kwasababu wazazi hawajui umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike kama chanzo cha kuondoa umaskini wa mtoto na familia kwa pamoja.

Jamii ikumbuke kwamba elimu ni haki ya mtoto kisheria na ndoa kwa mtoto ni kosa kisheria.

Tunayo sheria nzuri ya mtoto ya mwaka 2009, ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kupunguza tatizo la ndoa za utotoni na kuwapa watoto fursa ya kusoma.

Ili kuwasaidia watoto wa kike kuepukana na janga la ndoa za utotoni, ni muhimu serikali kuweka mazingira rafiki kwa watoto hao, hasa kuyafanya mazingira ya shule kuwa rafiki, pia shule ziwe karibu na nyumbani.`



**JUDITH MREMI (MWALIMU SHULE YA SEKONDARI MNAZI MMOJA, DAR)**

UKATILI na unyanyasaji wa kijinsia ni miongoni mwa matatizo makubwa ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikemewa na viongozi wa serikali pamoja na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali zinazotetea haki ya mtoto wa kike.

Lakini bado kuna baadhi ya Watanzania wenzetu, ambao hawajajua umuhimu wa elimu na wanamkosesha mtoto wa kike haki ya kupata elimu kwa kumuingiza katika ndoa.

Huu ni ukatili wa kijinsia, na ukifuatilia utabaini kwamba wazazi wanaokiuka haki za watoto wao wa kike ya kupata elimu kwa kuwaingiza katika ndoa ili wapate mahari ni ukosefu wa elimu ya kujua kuwa kumpa elimu mtoto wa kike ni kuelimisha jamii nzima.

Hawa nao wana haki kama watoto wa kiume.

Wakisoma wanakuwa na uwezo wa kufanya kazi za ofisini au kujiajiri na kupata kipato na hata kukabiliana na changamoto katika maisha yao ya baadaye.

Hivyo ninaishauri serikali tukufu kutoa elimu hiyo ili kumwezesha mtoto wa kike kupata haki yake ya elimu.



**ZAINABU MSALAMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TABIA hii imekuwa ikikemewa sana serikali na wadau wengine wakiwamo marafiki wa elimu. Hata hivyo, inashangaza kuona katika karne hii bado wapo baadhi ya wazazi wanaoendelea kukumbatia mila zilizopitwa na wakati zikiwamo hizo za kuwanyima watoto wa kike elimu kana kwamba hawana haki ya kuipata.

Elimu ni haki ya kila mtoto awe wa kiume au wa kike. Umefika wakati sasa jamii ibadilike na kutambua kwamba hata mtoto wa kike ni muhimu.

Hivyo asomeshwe hadi kufikia kiwango cha elimu anachokitaka. mtindo wa kumuoza angali mdogo si tu unamkosesha haki ya kupata elimu, bali pia ni hatari kwa afya yake.

Watu wasiotaka kubadilika katika jambo hili ni vizuri wakachukuliwa hatua kali za kisheria ili kuepusha watoto wa kike na biashara hiyo hatari.

Tumekuwa tukisikia baadhi ya wazazi wakiwakatisha masomo watoto wao ili waolewe.

Na mbaya zaidi watoto wengine hata wakati wanasubiri matokeo ili waingie sekondari, wanalazimishwa waolewe ili wazazi wao wapate mahari.

Yaani ni kama wamekuwa vitega uchumi vya wazazi! Hii si haki kabisa.



**JUMA HAMIS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HILI tatizo linatokana na sababu tatu. Ya kwanza ni wazazi kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu kumsomesha mtoto wa kike.

Sababu ya pili ni kwamba hawajui madhara ya kumuozesha mtoto wa kike katika umri mdogo na pia hawajui madhara ya mimba za utotoni.

Sababu ya tatu ni wazazi kuwa na tamaa ya kumiliki mali, ubabe wa wazazi wa kiume kutumia nguvu nyingi kudhibiti wazazi wa kike ili kutimiza malengo yao ya kuozesha watoto bila ridhaa.

Yaani kwa ujumla ni kwamba ukosefu wa elimu ya uzazi ni tatizo kubwa.

Lakini chanzo kikuu ninachokiona hapa ni tamaa ya kumiliki mali, hali ambayo husababisha baadhi ya wazazi kunyima watoto wao haki ya kupata elimu.

Cha msingi na kinachofaa kufanywa ni kupeleka elimu kwa wazazi wa aina hii na hasa kule vijijini ambako ninaamini tatizo ni kubwa na mkazo mkubwa uwe ni kwa wazazi wa kiume.

Aidha, viongozi wa maeneo husika wapewe sheria ndogondogo za kuwadhibiti wale wanaohusika katika tatizo hilo.



# Miti milioni 1.5 kupandwa ifikapo 2020

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

MITI milioni 1.5 inatarajiwa kupandwa hadi kufikia mwaka 2020 wilayani Mbarali mkoani Mbeya, likiwa ni lengo la kitaifa la kuhakikisha jamii inathamini na kuendelea kutunza mazingira kukabiliana na ukame.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya ambao ulifanyika katika kitongoji cha Kata ya Lugelele eneo ambalo hospitali hiyo inajengwa.

Mfune alisema kuwa kipindi hiki cha mvua wanaendelea kuhamasisha wananchi kupanda miti katika maeneo yao na kusisitiza watumishi na viongozi wengine kupanda miti kwenye maeneo ya ofisi zao.

"Kila wilaya nchini imepewa idadi ya kupanda miti, tunajukumu kubwa la kuhakikisha maeneo yetu yanapambwa na miti, tuendelee kuotesha mbegu na miche ili kupanda maeneo yaliyosalia na tuoteshe miti yenye faida zaidi ya moja kwa mfano mikorosho na miti ya matunda badala ya kuotesha mijohoro. Matokeo ya uoteshaji miti hii tutaanza kuyaona ndani ya miaka 5," alisema Mfune.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Ofisa Misitu na Maliasili wa Wilaya, Charles Patrick, alisema kipindi cha mwaka 2018 walifanikiwa kupanda miti takribani 560,000 kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye vyanzo vya maji, kandokando ya misitu ya hifadhi ya vijiji, maeneo ya makazi, mashambani na kwenye maeneo ya malisho.

Alisema katika kufanikisha zoezi hilo viongozi wa vitongoji na vijiji walipewa jukumu la kuwahamasisha wananchi kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali wanayoyazunguka.

Aliongeza kuwa wakati wanatekeleza zoezi hilo walikabiliana na changamoto mbalimbali kama vile mwamko mdogo kwa jamii, juu ya suala la upandaji miti, uhaba wa mvua, uchomaji moto ovyo pamoja na uchungaji holela wa mifugo.

Alisema baadhi ya jamii hazikuonyesha ushirikiano badala yake walitumia viongozi wa mila pamoja na Mkuu wa Wilaya kuielimisha jamii iliyokuwa inapinga zoezi hilo.

"Mwaka huu wilaya ina mpango wa kupanda miti takribani 750,000 katika maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za umma, binafsi, makazi na kwenye vyanzo vya maji, na hadi kufikia sasa tayari kuna miti takribani 1,000 imeshapandwa kwenye maeneo mbalimbali, alisema Patrick.

# Utafiti wabaini uelewa mdogo kikwazo ujenzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ZAIDI ya kaya 300 katika kata tatu za Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, hazina vyoo kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya afya pamoja na jamii kuwa na imani potofu.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa Mradi wa Ushirikishwaji Vijana katika ujenzi wa vyoo bora wa (YESB) kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Catholic Relief Service (CRS), Mhandisi Ephraim Tonya, wakati wa kuhitimisha mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 42 wanaoishi kwenye mazingira magumu wilayani Mbarali.

Alizitaja kata zenye changamoto hiyo kuwa ni Lugelele, Ubaruku na Rujewa na kwamba kaya hizo ni sawa na watu 1,200 hali ambayo alisema ni hatari kwa afya za watu hao.

Tonya alisema mradi huo wenye ubunifu unafadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la UKaid na kutekelezwa na CRS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

**Mradi huo wenye ubunifu unafadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la UKaid na kutekelezwa na CRS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.**

"Utafiti huo tuliufanya Oktoba mwaka jana kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mbarali, ambapo mbali na kubaini baadhi ya kaya kutokuwa na vyoo kabisa pia tuligundua kuwa kwa sasa wenye vyoo vilivyoboreshwa ni asilimia 18 pekee," alisema Tonya.

Aidha, alisema asilimia 82 bado wanatumia vyoo vya asili na kwa kata hizo tatu jumla ya kaya 1,692 sawa na watu 6,843 zilitembelewa kwa wakati wa utafiti huo.

Aliongeza kuwa mradi huo wa miaka mitatu ambao ulianza 2018, ambao unatarajiwa kufikia ukomo mwaka 2021, una lengo la kuboresha afya ya jamii kupitia ujenzi wa vyoo bora, unaolenga kuwapatia mafunzo ya ufundi vijana 11,070 katika Chuo cha Veta.

"Ili kufanikisha lengo la mradi huu tumetumia njia ya kuwajengea uwezo vijana walio katika mazingira magumu na walio katika sekta rasmi ya ajira, ubunifu huo utawafanya vijana hao kunufaika na mikopo ya asilimia nne itokanayo na mapato ya ndani ya halmashauri," alifafanua Mhandisi Tonya.

Akisoma risala kwa mgeni rasmi wakati wa kukabidhiwa cheti cha usajili pamoja na katiba kwenye kikundi cha vijana 42 kinachoitwa Vijana Mafundi Ujenzi Mbarali, Vaileth Majura, aliomba kikundi chao kupatiwa mkopo wa vijana ili waweze kupata mtaji wa kujiendesha.

Vaileth aliomba serikali kuwahusisha kwenye kazi za ujenzi zinazoendelea ili waonyeshe uwezo na umahiri wao walioupata na kuendelea kujifunza kwa kushirikiana na mafundi wazoefu waliopatiwa kandarasi za ujenzi na kuwa sehemu ya kuisaidia jamii.

Akikabidhi vyeti kwa wahitimu, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Oliver Sulle, aliwapongeza vijana kwa kuhitimu mafunzo ya ujasiriamali pamoja na ufundi uashi na kwamba ujuzi walioupata wakautumie katika kuisaidia jamii kujenga vyoo bora.

Aliwaomba kutumia fursa ya ujenzi wa vyoo katika maeneo yao na kuwasisitiza mabinti kutorubuniwa na baadhi ya washika kandarasi badala yake wajiamini na kutafuta kazi kwa njia ya halali.

Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Kivuma Msangi, alisema mwezi ujao kikundi hicho kitaanza kupata kazi za ujenzi kwa kuwa wilaya hiyo ina miradi mingi ya ujenzi ambayo inaanza hivi karibuni.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kushoto), akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya zana za kijadi za Chifu Kingalu Mwanabanzi wa kwanza, zilizokuwa zimeibiwa na kurudishwa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Kijiji cha Kinole, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: MAELEZO**

# Magereza waanzisha mkakati kuzalisha chakula

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

JESHI la Magereza limeanzisha mkakati wa miaka mitano wa kuzalisha chakula kitakachokidhi mahitaji ya wafungwa na mahabusu kwa asilimia 100, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli.

Kauli hiyo ilitolewa na Kamishna Jenerali wa Magereza, Faustine Kasike, akiwa katika ziara ya kukagua shughuli za uzalishaji wa chakula katika Gereza la Kilimo la Songwe mkoani Mbeya, ambapo alisema kwa sasa jeshi hilo linajitegemea kwa asilima 30 katika upatikanaji wa chakula.

Alisema pia magereza wamejiwekea mkakati kabambe wa miaka mitano wa kuzalisha chakula cha kukidhi mahitaji ya wafungwa na mahabusu kwa asilimia 100.

"Agizo la Rais Magufuli tumeanza kulitekeleza kwa vitendo, tayari magereza mengi hapa nchini yameanza kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na kila eneo litalima zao ambalo ni rafiki, hii itasaidia kukabiliana na changamoto ya uhaba wa chakula," alisema Kasike.

Awali kabla ya kufanya ziara ya kutembelea na kukagua mashamba ya kilimo, Gereza la Songwe, Kasike alikutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na kuishauri serikali kutunga sera inayoelekeza kuwa kila inapoanzishwa wilaya na mkoa kuhakikisha gereza jipya linajengwa ili kukabiliana na msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alimwomba Kamishna Jenerali wa Magereza kukamilisha ujenzi wa gereza jipya la Wilaya ya Chunya, ili kusaidia Jeshi la Polisi kuachana na kadhia ya kusafirisha mahabusu na wafungwa kila siku umbali wa zaidi ya kilometa 70 kutoka wilayani Chunya hadi jijini Mbeya.

Katika mkakati wake wa kujitosheleza kwa chakula, Jeshi la Magereza limetenga magereza 10 kutoka mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa, Njombe na Ruvuma ambayo yatajikita kwenye kilimo kwa ajili ya kuzalisha chakula cha kukidhi mahitaji ya magereza yote nchini.





# IGP avitaka vyombo vya ulinzi kukaza buti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VYOMBO vya ulinzi na usalama vimetakiwa kuzidisha mapambano ya kukomesha vitendo vya ujangili, ili kuzuia mauaji ya tembo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, alipofunga mafunzo ya vyombo vya ulinzi na usalama, watumishi wa maliasili pamoja na wanasheria.

Alisema licha ya kukamata silaha 355 na risasi 22,565, ambazo zilikuwa zinatumiwa na majangili kufanya uhalifu, lakini bado juhudi za ziada zinahitajika.

Sirro alisema hakuna sababu ya kupunguza kasi ya ulinzi inayofanywa na maofisa usalama wa wanyama pori, kinachotakiwa ni kukabiliana na majangili na kuyafikisha sehemu husika ili sheria ichukuwe mkondo wake.

**Tutaendelea kuwa pamoja kuhakikisha tunafanikisha kutokomeza ujangili katika hifadhi zetu.**

Alifafanua kuwa lengo ni kuona hifadhi za wanyamapori zinakuwa salama. Kamanda alisema askari hawatakiwi kuwa rafiki na majangili kwa sababu wataendelea kufanya uhalifu kila iitwapo leo.

Alisema wanahitaji kuona majangili yanatoweka na siyo kusumbua wanyama pori kila kukicha kwenye hifadhi hususani mauaji ya tembo na kuchukua meno yao.

"Kwa kweli mnanitia moyo sana askari kazi mnayofanya ni kubwa mnastahili pongezi,"alisema Siro.

Hata hiyo, alisema hawapaswi kupunguza kasi kwa sababu majambazi wanasikilizia upepo kuona askari wanafanya nini ili nao waingie kazini.

Aliwapongeza kwa kukamata watuhumiwa 963 wa uhalifu, hatua ambayo inaonyesha kwamba kazi wanayoifanya ni nzuri.

Sirro aliwapongeza Palm Foundation ambao ndiyo wadhamini wa semina hiyo ya kuvijengea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini.

Naye Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz alisema hakuna sababu ya kurudi nyuma kwa sasa kinachotakiwa ni kusonga mbele ili kuhakikisha hifadhi zinakuwa salama.

Alisema majangili kwa karne hii na awamu hii hawana nafasi kutokana na kuwa jeshi la polisi liko imara kuhakikisha wanafanikisha kile walichokikusudia.

Naye Mkurugenzi wa Palm Foundation, Krissie Clark alisema wanayo kila sababu ya kuandaa mafunzo hayo ili kuhakikisha sekta ya utalii inakuwa salama.

"Tutaendelea kuwa pamoja kuhakikisha tunafanikisha kutokomeza ujangili katika hifadhi zetu," alisema Krissie



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiweka dole gumba kwenye fomu ya kufungulia akaunti binafsi mbele ya Meneja wa Huduma kwa Wateja wa tawi la NMB Kambarage jijini Dodoma, alipofika kufungua akaunti binafsi mwishoni mwa wiki. Anayeangalia ni Meneja Uhusiano Huduma za Serikali , Josephene Kulwa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Magonjwa ya mifugo hatari kwa binadamu

**Oscar Mirindo,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa asilimia 60 hadi 80 ya magonjwa ya mifugo yanaweza kuambukiza binadamu na kwamba hali hiyo inaweza kudhibitiwa iwapo wafugaji watazingatia chanjo na kuogesha wanyama hao kwa kutumia majosho.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma na Msajili wa Baraza la Veterinari Nchini, Dk, Benad Masuruli, alipozungumza na Nipashe juu ya hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na tatizo hilo.

Dk. Masuruli alisema kuwa magonjwa makuu kwa mifugo hasa ng'ombe ni yale yanatokana na kupe ambayo yanasababisha, vimeta, kichaa cha mbwa, bonde la ufa na mengineyo.

Aidha, alisema kuwa athari ya magonjwa kama hayo siyo kwa mifugo pekee na binadamu bali pia kwa upande wa biashara kwa ng'ombe huwa dhaifu hivyo kukosa masoko mazuri.

Alisema kuwa katika kupambana na magonjwa ya mifugo, serikali imeanzisha mikakati ya kuimarisha majosho ili mifugo mingi iweze kuogeshwa.

Awali alisema kuwa kabla ya mabadiliko hayo majosho yalikuwa katika mazingira mabaya ya uchakavu, uchache wa majosho na uhaba wa dawa.

# Mifumo ya taarifa za watoto wa mitaani kuunganishwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi wa Huduma za Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Rasheed Maftah, ameitaka mifumo inayokusanya taarifa za za ustawi wa jamii katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuungana na kuweka mmoja ili uweze kuhudumia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Maftah aliyasema hayo wakati wa kikao maalum cha kuwapitisha wataalamu na wadau kwenye mfumo wa MVC-MIS wa taarifa za ustawi wa jamii unaowezeshwa na taasisi ya Measure Evaluation.

Alisema wakati umefika kwa wataalamu kukutana pamojana kuona namna gani mifumo hiyo ambayo inakusanya taarifa za ustawi wa jamii inunganishwa kupata mmoja ambao utafanya kazi zote zinazofanywa na mifumo hiyo kwa sasa.

Aliongeza kuwa kazi hiyo ni lazima ifanywe na wataalamu wa mifumo wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya wakishirikiana na wale waliotengeneza mifumo hiyo hapo awali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Measure Evaluation pamoja na Path Kizazi Kipya.

"Ni wakati sasa wa watalaamu wetu kujengewa uwezo na kuifahamu mifumo hii kwa undani na kushiriki katika kuiunganisha ili hapo baadaye miradi itakapomaliza muda wake na kuikabidhi mifumo hiyo kwa Serikali tuwe na watu watakaoweza kuindeleza na kuisimamia, " alisema Maftaha.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angelista Kihaga akichangia wakati wa kikao hicho alisema, hata kama mifumo hiyo inawezeshwa na wafadhili, lakini lazima waangalie uwezekano wa kuwajengea uwezo watumishi wa serikali.

Alisema watumishi hao wataendelea kuihudumia mifumo baada ya mradi kumalizika kuliko kuajiri watumishi wa muda au kuwajengea uwezo wataalamu wa kujitolea, ambao huondoka mara tu mradi unapomaliza muda wake.

"Sisi kama serikali ni lazima tuangalie namna ambavyo mifumo hii inakuwa endelevu na siyo siku wadau wakitukabidhi basi ndiyo itakuwa mwisho wa matumizi ya mifumo hiyo. Imefika wakati ambapo wataalamu wanatakiwa kufahamu kila kitu katika mifumo hii ili waweze kuiendeleza hapo baadae" alisema Kihaga.



# Waziri awataka watumishi kuacha majungu, fitina

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Muhammed Aboud, amewataka watendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kufanya kazi kwa bidii huku wakijiepusha fitina na majungu.

Alisema cheo watakipata iwapo watafanya kazi kwa bidii na wala hakipatikani kwa kujengeana fitina na majungu miongoni mwao, hivyo ni vyema kutoa huduma bora kwa unyenyekevu nidhamu na uadilifu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na watendaji wa mamlaka hiyo katika sherehe fupi ya kuwaaga baadhi ya wafanyakazi ambao wanakwenda nchini Oman kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali.

"Mna wajibu wa kupendana na kuhurumiana, msipigiane majungu kwa nafasi uliyonayo fanya kazi kwa bidii, kwa kuwa cheo kitakuja kwa bidii yako ya kazi na siyo kwa kumfitini mwezako,"alisema.

Alisema kufanyakazi kwa ushirikiano na upendo, mafanikio yake ni makubwa katika nchi kwa kuwa viwanja vya ndege ni kioo cha nchi.

**Sisi huduma yetu zaidi ni biashara ya utalii, umuhimu wa kupata wageni wengi ndiyo msingi wa mafanikio yetu kiuchumi na kimaendeleo na chanzo cha wageni ni bandari na viwanja vya ndege.**

"Mwende mkaionyeshe sura ya Zanzibar, sura ya upendo, nidhamu, umoja, kufanyakazi kwa bidii na kuwa tayari kujifunza...mutakapo kwenda Oman na kufanya hivyo mtaweka heshima kubwa na kuendeleza undugu kati ya Oman na Zanzibar," alisema.

Aboud alisema Oman imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo ikiwamo ya kuimarisha viwanja vyao vya ndege.

"Sisi huduma yetu zaidi ni biashara ya utalii, umuhimu wa kupata wageni wengi ndiyo msingi wa mafanikio yetu kiuchumi na kimaendeleo na chanzo cha wageni ni bandari na viwanja vya ndege," alisema.

Alisema kuwa viwanja vya ndege wanaingia watu wengi wazuri na wabaya hivyo ni vyema kuwa makini na kutoa taarifa pale wanapoingia wageni wakiwa hawana nia njema na Zanzibar.

"Wengi wa wageni wetu wanakuja kwa nia njema, hivyo kuwakaribisha kushirikiana nao vizuri na kutowapa usumbufu, lakini tuwe makini na tufanye kazi zetu kwa vizuri," alisema.

Aidha, aliwataka wahakikishe wanadhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya kwa kuwa athari zake ni kubwa.

Naye Balozi mdogo wa Oman visiwani Zanzibar, Dk. Ahmad Hamood Al Hobs, alisema serikali ya Oman imeamua kutoa nafasi hiyo, ili wafanyakazi hao kujifunza kwa vitendo na kuendana na kasi ya mabadiliko ya viwanja vya ndege ulimwenguni.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Mulhat Yussuf Said ambaye ni miongoni mwa wafanyakazi wanaokwenda nchini Oman, alizishukuru serikali mbili za Zanzibar na Oman kwa kuwapatia nafasi hiyo na kuahidi kuwa watatumia vyema fursa hiyo ili kuimarisha utendaji wa kazi zao.

Wafanyakazi 10 wameenda nchini Oman kujifunza shughuli mbalimbali za uendeshaji wa viwanja vya ndege kwa muda wa wiki mbili.

# Mwenyekiti wa CCM amwaga ushauri kwa wananchi

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Magharibi kichama, Muhammed Rrajab Soud, amewataka wakazi wa Shehia ya Mnarani, kutunza miondombinu ya maji ili iwe endelevu.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa visima vya maji katika shehia ya Mnarani Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, mwenyekiti huyo alisema serikali inatarajia kutatua kero zote zinazowakabili wananchi katika maeneo yao bila ubaguzi.

Alisema miradi yote inayoanzishwa ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo inalenga kuwapatia huduma zote muhimu za kijamii.

"Ni vyema kuunga mkono juhudi hizo za serikali kwa kuitunza na kuenzi miondombinu hiyo ili kuhakikisha inakuwa ya kudumu na kuwanufaisha wananchi," alisema.

Aidha, aliwataka kushirikiana katika kuilinda miondombinu hiyo ili watu wenye nia mbaya na wasiopenda maendeleo wasiweze kuiharibu.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, Khamis Juma Maalim, aliwataka wakazi wa shehia hiyo kutumia vizuri huduma ya maji waliyopatiwa ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

Kwa upande wao wakazi wa shehia hiyo wameahidi kulinda mradi huo ili uweze kudumu kwa muda mrefu.

ITV Daima
Kwa matangazo na Burudani saa 24



Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Juma Ali Juma (kulia), akitoa maelezo kwa Kiongozi wa Ujumbe wa Mfuko wa Maendeleo wa Khalifa kutoka AbubDhabi, Falme za Kiarabu (UAE), Nizar Cheniour, walipotembelea Ushirika wa Fakirice Milling Enterprises Kisongoni, unaojishughulisha na kukoboa mpunga, katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Serikali yaonya watendaji 'watakaodokoa' fedha za miradi

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeonya kwamba haitasita kumwajibisha mtendaji yeyote wa halmashauri ya wilaya atakayebainika kutumia vibaya fedha za mfuko wa jimbo zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza miradi ya wananchi.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema serikali haitasita kuchukua hatua kuhusu jambo hilo na kwamba watakaobainika watafikishwa hata mahakamani.

Alieleza kuwa, zipo hitilafu zinazojitokeza ambazo zinazorotesha uendelezaji wa miradi ya wananchi majimboni ambazo husababishwa na baadhi ya watendaji wa halmashauri za wilaya kufanya utapeli hasa katika matumizi ya fedha.

Akizindua mradi wa majisafi na salama katika Shule ya Msingi Mangapwani, Wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja, Balozi Iddi, alisema wapo baadhi ya watendaji kwenye halmashauri za wilaya wanaonyesha udhaifu kwa kuzorotesha miradi iliyoanzishwa na wananchi kwa fedha zilizoidhinishwa na viongozi husika.

Alieleza kuwa kuanzia sasa atalazimika kufuatilia changamoto zote anazowasilishiwa zinazohusiana na kadhia hiyo na hatasita kumchukulia hatua za kinidhamu mtendaji atakayebainika kuhusika na matumizi binafsi ya fedha.

Aliwataka wananchi wa Mangapwani kutoa taarifa mapema pale yanapojitokeza matatizo ya kiufundi katika uendeshaji wa mradi huo wa majisafi na salama na kuacha tabia ya kuwatumia mafundi wa vichochoroni wanaoweza kuleta athari zaidi ya kiufundi kwenye mradi huo muhimu kwa ustawi wa jamii.

Aidha, aliwapongeza na kuwashukuru wananchi wa vijiji vya Mangapwani, Kiomba Mvua, Vuga Mkadini na Matetema, kwa jitihada zao za kujisogezea huduma mbalimbali za kijamii na maendeleo kwenye maeneo yao.

Katika ziara hiyo Balozi Iddi akiwa pia Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda alipata nafasi ya kukagua mradi wa kisima cha maji safi kilichochimbwa kupitia fedha za mfuko wa mbunge.

## HABARI KIMATAIFA

# Waziri Mkuu Ethiopia ang'ara kongamano la uchumi

**DAVOS,** Uswis

KONGAMANO la Uchumi Duniani lililokuwa linafanyika Davos, limemalizika huku baadhi ya viongozi muhimu akiwamo Rais wa Marekani Donald Trump kutohudhuria. Kwenye kongamano hilo Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed Ali alipongezwa kwa kuweza kutafuta suluhu ya amani na Eriteria.

Akizungumza katika Kongamano hilo, Abiy Ahmed Ali alisema kuwa nchi za Kiafrika ni lazima ziimarishe zaidi mahusiano yao.

"Tunaamini kuwa muungano huu lazima uangaliwe sio tu kama ni mradi wa kiuchumi lakini pia kama hatua muhimu ya kutafuta suluhu ya amani na maridhiano katika Pembe ya Afrika," alisema Ali.

Wachambuzi wanasema kuwa baadhi ya viongozi walishindwa kuhudhuria akiwamo Rais wa Marekani, Donald Trump kwa sababu ya kufungwa kwa baadhi ya idara za serikali.

Rais wa China Xi Jinping naye hakuwapo, pia Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May, na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron.

Baadhi ya masuala yalijitokeza katika ajenda ya Davos, ni suala la mabadiliko ya tabia nchi. Waziri Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern alihimiza hatua zichukuliwe.

"Hili suala ni kuhusu kuwa upande sahihi wa historia. Je unataka kuwa kiongozi na baada ya uongozi wako unakuja kuona na kusema kuwa ulikuwa upande uliotoa hoja potofu wakati dunia ilikuwa inapiga kelele kuhimiza upatikane ufumbuzi? Na ni rahisi hilo kama vile ninavyo fikiria," alisema Ardern.

Mmoja wa wachambuzi kutoka taasisi ya Chatham House, Vinjamuri alieleza kuwa mkutano wa Davos 2019 huenda ukakumbukwa kwa kukosekana usimamizi wa kimataifa.

**VOA**



Maandamano dhidi ya serikali katika mji mkuu wa Sudan, Khartoum. **PICHA: REUTERS**

# Rais wa Sudan azuru Misri

**CAIRO,** Misri

RAIS wa Sudan, Omar al-Bahsir amesema kuna jitihada za makusudi zinazofanyika ili kuiangusha serikali yake kwa kisingizio cha mapinduzi ya kiarabu.

Bashir ametoa kauli hii akiwa ziarani jijini Cairo nchini Misri baada ya kukutana na mwenyeji wake Abdel Fattah al-Sisi, kwenye ziara ya saa moja.

Baada ya Qatar, Misri ni nchi ya pili ambayo Rais Bashir amezuru tangu kuzuka kwa maandamano yaliyosababisha vifo vya watu 27.

Maandamano hayo ambayo awali yalikuwa ya kupinga bei ya mkate ambayo iliongezwa maradufu yalibadili mwelekeo na kuwa maandamano dhidi ya Rais Omar al-Bashir, huku waandamanaji wakimtaka ajiuzulu.

Nchi nyingi za Kiarabu hazikutia saini kwenye mikataba ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), ambayo imetoa hati mbili za kukamatwa dhidi ya Rais Omar Al-Bashir kwa uhalifu dhidi ya binadamu na mauaji ya kimbari katika jimbo la Darfur.

Bashir anavishutumu vyombo vya habari kwamba vinachochea maandamano na kukuza habari za uongo kuhusu maandamano hayo yanayoendelea nchini Sudan.

Waandamanaji nchini Sudan wameendeleza maandamano kumtaka kiongozi huyo ambaye ameongoza taifa hilo kwa miaka 30, kuondoka madarakani.

Kwa mujibu wa wachambuzi wa masuala ya kisiasa Rais Omar Al- Bashir anatafuta uungaji mkono kutoka nchi za Kiarabu na zile za ukanda. **RFI**

# Idara za serikali zaanza kutoa huduma Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

BAADHI ya idara mbalimbali za serikali ya Marekani zilizo kuwa zimefungwa kwa siku 35 zimefunguliwa, siku mbili kabla ya Idara ya Mapato ya Ndani (IRS) kuanza kushughulikia mchakato wa kupokea mawasilisho ya kodi za wananchi kwa mwaka 2018.

Kufungwa kwa huduma za kiserikali nchini Marekani kulifikia tamati siku ya Ijumaa usiku, baada ya Rais Donald Trump kusaini muswada wa matumizi ya wiki tatu uliopitishwa na Bunge kumaliza kufungwa kwa serikali.

Takribani wafanyakazi wa serikali kuu 800,000 hawakulipwa mishahara yao kwa mara ya pili siku ya Ijumaa, mwishoni mwa wiki.

Mwishoni mwa wiki hii Bunge la Marekani lilipitisha na Trump alisaini sheria inayoagiza idara za serikali kuu kuwalipa wafanyakazi mishahara iliyokuwa haijalipwa kwa haraka.

Lakini maafisa wa serikali wametahadharisha kuwa inaweza kuchukua siku kadhaa kwa wafanyakazi wa serikali kuu kupata malipo yao yote waliokuwa hawajalipwa.

Ofisi ya Utawala na Bajeti ya Marekani ilituma waraka jioni Ijumaa kwa idara na ofisi za serikali zilizo kuwa zimefungwa kuwajulisha kuwa vitengo vyao sasa vimefunguliwa na kuwa wafanyakazi wao wanaweza kurejea kazini. Waraka huo pia ulizitaka idara hizo kufungua ofisi hizo tena mara moja na kwa kufuata utaratibu.

Ujumbe kwa wafanyakazi wote wa idara ya kodi ya ndani uliyokuwa katika tovuti yao ulisema wafanyakazi wanatarajiwa kuripoti kazini masaa manne baada ya tangazo hilo kuwekwa Januari 25, mwaka huu.

Na zaidi ya hilo, tangazo hilo liliwashauri wafanyakazi kuripoti kazini kwa mujibu wa kuanza kwa ratiba inayofuatia ya siku ya kazi.

**VOA**

# 10 wauawa shambulio la kigaidi Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** Bukina Faso

WATU 10 wameuawa katika shambulio la kigaidi katika Kijiji cha Sikiré, kilomita 20 kutoka Manispaa ya Arbinda, katika mkoa wa Soum, nchini Burkina Faso.

Jeshi la Polisi la nchi hiyo limeeleza kuwa washambuliaji waliwasili katika kijiji hicho wakiwa na pikipiki. Shambulio hilo ambalo lilitokea siku ya Jumapili asubuhi, siku ambayo watu walikuwa wamefurika sokoni.

Watu zaidi ya 20 ambao walikuwa wamejihami kwa silaha waliwafyatulia risasi wakazi wa kijiji hicho.

Kwa mujibu wa kiongozi aliyechaguliwa katika kijiji cha Sikire, alieleza kuwa washambuliaji hao walikuwa wakizunguka kijiji hicho, huku wakiwafyatulia risasi wananchi.

Washambuliaji hao pia waliipora na kuchoma moto maduka na biashara nyingine, kwa mujibu wa chanzo cha habari kutoka kijiji hicho ambaye hakutaka kutaja jina.

Januari 10, mwaka huu watu 12 waliuawa katika kijiji cha Gasseliki, kilomita 30 kusini mwa Arbinda, katika mkoa wa Soum, uliyowekwa chini ya hali ya dharura tangu mwanzoni mwa mwaka.

**RFI**

# 58 wafariki bwawa likipasuka

**BRUMADINHO,** Brazil

IDADI ya watu waliofariki baada ya bwawa kupasuka katika mji wa Brumadinho, kusini mashariki mwa Brazil imeongezeka na kufikia 58, watu wengine zaidi ya 300 hawajulikani walipo.

Maofisa wa ulinzi wa raia katika mji wa Brumadinho wamethibitisha kuongezeka kwa idadi hiyo ya watu.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kuna hofu ya idadi ya vifo kuongezeka zaidi baada ya waokoaji wakiwa na helikopta 13 kushindwa kuwapata watu walionusurika.

Kwa siku ya jana waokoaji walianza tena juhudi za kuwatafuta waliokumbwa na mkasa huo baada walinzi wa raia kusema kuwa hakuna hatari ya kupasuka kwa bwawa la pili.

Kwa mujibu wa idara ya zima moto watu wapatao elfu 24 walihamishwa kutoka kwenye nyumba zao katika eneo hilo la kusini mashariki mwa Brazil.

**DW**

# Polisi yaua 8 tuhuma za ujambazi

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

JESHI la Polisi mkoani Kigoma, limesema limeua watu wanane kwa tuhuma za ujambazi. Kamanda wa Polisi mkoani Kigoma, Martin Ottieno, amethibitisha kuwa jeshi lake limeua watu hao katika pori la Muyowozi wilayani Kakoko.

Kamanda Otieno alisema jana mjini hapa kuwa tukio hilo lilitokea Jumamosi katika Pori la Muyowozi, baada ya kupewa tarifa na baadhi ya raia wema katika kijiji cha Mganza kwa kuwatilia shaka watu hao waliojificha humo.

"Tulipata taarifa kutoka kwa wakazi wa kijiji cha Mganza kuhusu uwapo wa vibarua wa mashambani wanaowatilia shaka na walipokuwa wakiwafuatilia ndipo watu hao walipoanza kurusha risasi na majambazi nane yameuawa sambamba na kukamata bunduku moja aina ya AK 47 ikiwa na risasi 10.

Alisema maiti zimehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kakonko.



Baadhi ya wafanyabiashara jijini Dodoma, wakiwa kwenye foleni ya kupata vitambulisho vya wafanyabiashara ndogondogo jana vilivyotolewa na Rais John Magufuli. **PICHA: IBRAHIM JOISEPH**

# Ndoto ya Tanesco sasa kutoa gawiwo kwa serikali

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Dk. Tito Mwinuka, amewahimiza watumishi wote wa shirika hilo kutoa huduma bora, sahihi na kwa wakati kwa wateja wao huku akieleza ndoto yake ni kuona shirika hilo linajiendesha kwa faida na kutoa gawiwo kwa serikali.

Dk. Mwinuka alieleza hayo jijini Arusha, wakati anazungumza na wahariri wa vyombo vya habari baada ya kukamilika kwa ziara ya kukagua miradi ya umeme inayotokelezwa na Serikali.

Ziara hiyo imefanyika katika mkoa wa Arusha na Kilimanjaro na miongoni mwa miradi ambayo wahariri wameona ilivyotekelezwa ni ile iloyopo kwenye Mifumo ya Usambazaji umeme nchini (TEDAP).

Akifafanua zaidi wakati anajibu baadhi ya maswali ya wahariri, Dk. Mwinuka alisema pamoja na kuwapo kwa pongezi nyingi zinatokana na kuwapo kwa huduma bora zinazotolewa na shirika hilo, lakini alisisitiza kwa watumishi wote wa Tanesco kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wateja.

"Tunataka kuona Tanesco inatoa huduma nzuri na hiyo iwe kwa nchi nzima. Tunataka mteja anapokwenda Tanesco au kokote ambako tunatoa huduma basi apate huduma nzuri, sahihi na kwa wakati pamoja na kuheshimiwa.Hivyo niendelee kutoa rai kwa watumishi wa ngazi zote tuliyopo tutoe huduma nzuri," alisisitiza.

Alisema ndoto yake ni kuona Tanesco inajiendesha na kufanya kazi zake kwa faida na kwamba wanakwenda vizuri, huku akifafanua kwa miaka miwili sasa shirika hilo linajiendesha bila kupewa ruzuki.

"Malengo yetu ni kuhakikisha Tanesco tunafanya kazi zetu na kutengeneza faida na hii imeanza kuleta tija,ni mwaka wa pili tunajiendesha bila ruzuku ya Serikali na hiki ndicho tunachosisitiza tuwe shirika ambalo linapata faida na hatimaye tutoe gawiwo kwa Serikali," amefafanua Dk. Mwinuka.

Kuhusu madeni, Dk. Mwinuka alisema Tanesco ilikuwa inadaiwa madeni makubwa ambayo yaliionekana sugu, lakini kupitia mikakati yao wamedhamiria kulipa madeni hayo na kwamba kwa sasa wamefanikiwa kwa kuwa deni haliongezeki, hivyo wanatarajia kuyamaliza.

"Kutokana na hali iliyokuwapo miaka ya nyuma Tanesco ilijikuta inadaiwa, hivyo tunaendelea kulipa madeni ya nyuma," alisema na kusisitiza pamoja na muelekeo mzuri wa shirika hilo, bado wamejipanga kutoa huduma ikiwamo ya kuhakikisha nchi yetu inakuwa na umeme wa uhakika na kuendelea kutatua changamoto zilizopo," alisema.

Kuhusu miradi ya TEDAP, Dk.Mwinuka alisema wamefanikiwa kuitekeleza miradi hiyo kwa mikoa ya Arusha,Kimanjaro na Dar es Salaam na kwamba imeleta tija kubwa.

Alipoulizwa iwapo Tanesco itapeleka mradi wa TEDAP katika mikoa mingine, Dk. Mwinuka alisema: "Ni kweli tunatamani kuipeleka miradi hiyo nchi nzima maana tumeona faida yake kwa mikoa ambayo tuimeitekeleza.

" Wananchi wasichome moto katika maeneo ambayo miundombinu ya umeme. Ni jukumu letu sote kuhakikisha tunailinda na kuitunza miundombinu yetu ya umeme ambayo uwekezaji wake katika kutekeleza miradi ya umeme inatumia gharama kubwa. Tuitunze miundombinu yetu."

ITV

JARIDA LA WANAWAKE SAA 1:00 USIKU

KATIKA KIPINDI CHA LEO FUATILIA WANAWAKE WANAKIKUNDI KUTOKA TUNDURU WAKIONYESHA UBUNIFU KATIKA KAZI ZA UKULIMA WA KISASA NA PIA WAKITUMIA KILIMO HICHO ILI KUTUNZA FAMILIA ZAO.

## Vijiji vyanufaika fedha uwekezaji

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

BAADA ya Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, kutoa agizo kukamatwa kwa mmiliki wa kampuni ya uwindaji ya Greenmiles Safari Ltd kwa kushindwa kulipa vijiji 23 zaidi ya Sh. milioni 329, kampuni ya uwindaji ya Wengert Windrose Safari Ltd, yenye kitalu eneo la Lake Natron Game Control North, imekabidhi hundi ya Sh. milioni 36 kwa vijiji 12 vinavyozunguka kitalu chao.

Januari 15, mwaka huu, DC Mwaisumbe, alimwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Longido, kukamatwa mwekezaji wa Greenmiles Safaris Ltd kwa kushindwa kulipa Sh. milioni 329 kwa vijiji 23 kwa zaidi ya miaka minne sasa.

Vijiji ambavyo Wengert Windrose Safari Ltd imevilipa fedha ni Origrah, Matale A na B, Alaililai, Kimwati, Lumbwa, Mairowa, Magadini, Orpuken, Ilchangit Sapukin, Wosiwosi na Ngoswaki vilivyopo Tarafa ya Kitumbeine na Engarenaibor.

Aidha, Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Clearance Msafiri, alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali ndani ya jamii na ni nje ya fedha zilizopo kwenye mikataba kama inavyosema kila kijiji kilipwe dola 5000.

"Hizi fedha tunatoa kwa vijiji zisaidie maendeleo, zipo nje ya zile dola 5000," alidai.

Alieleza walifanya makubaliano na vijiji mwaka jana juu ya fedha hizo na waliahidi kuzitekeleza Januari mwaka huu, hivyo wametoa fedha hizo ambazo kila kijiji kitapewa cheki ya Sh. milioni 3.

Alisema lengo hasa la kampuni yao kufanya hivyo ni kuhakikisha vijiji vinanufaika na uhifadhi uliopo kwenye maeneo yao na kuwataka kuzitumia fedha hizo kwa kujiletea maendeleo ndani ya maeneo yao.

Akifafanua pia kuhusu upande wa ajira kwa wazawa wilayani hapa, alisema kwa kipindi cha nyuma walipokuwa katika shughuli za uwindaji walitoa ajira kwa wazawa na hata sasa watatoa ajira pia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lumbwa, James Mollel, alipongeza kampuni hiyo kwa kuonyesha ushirikiano na uaminifu kwa jamii na kuwataka wadau waendelee kuwalinda wanyamapori waliopo katika kitalu chao na hata nje ya kitalu ili mazingira ya uhifadhi yawe rafiki kwao.

Naye Semet Mollel, Mtendaji wa Kijiji cha Magadini, alisema fedha hizo watazielekeza katika shughuli za maendeleo ikiwamo kusaidia ujenzi wa majengo ya madarasa pungufu ndani ya wilaya.

Diwani wa Kata ya Mundarara, Alais Moshao, DC Mwaisumbe kwa kuonyesha kuwajali wananchi wanyonge waliokuwa wakikandamizwa na watu wachache.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii. Mawasiliano:0767574701/0758753063. www.tracdi.ac.tz

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU

## VYETI VIMEPOTEA




**LAURIAN MARIRAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0110/0106 kilichotolewa na ILBORU SEKONDARI mwaka 1993. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0156/053 kilichotolewa na TANGA SEKONDARI mwaka 1996. Cheti cha Ualimu chenye namba E.523/147 kilichotolewa na MONDULI T.T.C.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KW/RB/14184/16.**

115028702

## PASSPORT IMEPOTEA



**SAEED YASLAM SAEED BIN HUWAIL** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba 06843621 iliyotolewa RIYADHI tarehe 31/10/2016.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi KIL/RB/1770/2019.**

115028602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**
**SHAURI NA. 324 LA 2015**

**MUSSA AMRI RAJABU……………………………MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **ACCESS BANK (T) LIMITED**
2. **MASHOKA AUCTION MART TANZANIA LIMITED**
3. **CHRISTA AMRI MUSSA**

… WADAIWA

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA: MASHOKA AUCTION MART TANZANIA LIMITED NA CHRISTA AMRI MUSSA

Unafahamishwa kwamba wajibu maombi hapo juu wanaendelea na Shauri/Ombi ulilofungua katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 18/02/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAENI- Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 11/12/2018.

MASAO .E
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

2150283002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No.24/2019**

Ombi la **ASHA SAID SHOMARI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SAID SHOMARI HAMSINI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **21/02/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

tarehe 24/01/2019.

Tarehe 24/1/2019
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115028502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IRENE S LELO** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya TOYOTA IST yenye namba za usajili T987 DEF Chassis namba NCP500239312 Engine no 2N22557822

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOM/TR/RB/113/2019**

115029202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HARUDI ALLI KISHAKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUZUKI CARAY yenye namba za usajili T 982 CWG. Chassis No. DD5IT576141. Engine NO.F6AEAA6141.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MUH /RB/3299/2018.**

115029402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**RODRICK KALISTI TEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 353 CAL BOXER.

Chassis namba MD2A21BYOJWB93463.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**OB/RB/863/2019.**

115029502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE NICHOLAUS SAMBALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COASTER yenye namba za usajili T 697 AAW Chassis namba HB310000246. Engine NO.12H113789.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/149/2019.**

215028402

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Familia ya Sala yachangisha milioni 788/-

**LONDON,** England

FAMILIA ya mchezaji aliyepotea na ndege, Emiliano Sala (pichani chini), imefikisha kiasi cha euro 300,000 sawa na Sh. milioni 788.7 za Tanzania ilizochangisha kwa watu kwa ajili ya kutaka zoezi la kumtafuta mchezo huyo wa Cardiff City liendelee.

Polisi wa kisiwa cha Guernsey eneo inapodaiwa kupotea ndege hiyo ndogo, Alhamisi iliyopita walisitisha zoezi la kumtafuta Sala, ambaye alipotea na akiwa na rubani David Ibbotson wakati wakitoka Nantes Ufaransa Jumatatu iliyopita.

Sala alikamilisha usajili wa kujiunga na Cardiff wikiendi hiyo kabla ya kurudi Ufaransa kwa ajili ya kukamilisha mambo mengine pale Nantes na Jumatatu alikuwa akirejea kwenye timu yake mpya.

Zoezi la kumtafuta yeye na ndege hiyo lilidumu kwa siku tatu bila kupata chochote na hivyo wakaamua kusitisha.

Baada ya hapo familia ya Sala ikaamua kuanzisha ukurasa maalumu kwenye mtandao wa kijamii kwa ajili ya kuchangisha fedha za kuendeleza zoezi la kumtafuta mchezaji huyo.

Watu mbalimbali walitoa michango yao na kufikia euro 300,000 Jumapili, huku mchezaji wa Klabu ya Paris Saint-Germain akitoa kiasi cha euro 30,010 kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo.

Mbappe si mchezaji pekee aliyejitolea kutoa kiasi hicho cha fedha, kwani mchezaji mwenzake wa PSG, Adrien Rabiot alichangia 25,000 Jumamosi na nyota wa Marseille, Dimitri Payet aliahidi kutoa euro 10,000.






# PERISIC

## akisepa si tatizo - Spalletti

**MILAN,** Italia

KOCHA Luciano Spalletti amethibitisha kwamba ataendelea kumuacha nje Ivan Perisic baada ya winga huyo wa Inter Milan kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka.

Meneja Mkuu, Beppe Marotta alisema Jumapili kabla ya mchezo dhidi ya Torino kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwamba Perisic amewasilisha maombi ya uhamisho, huku akihusishwa na mpango wa kutakiwa Atletico Madrid na Arsenal.

Lakini Arsenal imeripotiwa kwamba ipo tayari kumsajili Perisic kwa mkataba wa awali wa mkopo, wakati Inter hawataki kumuachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia kwa mkataba wa muda mfupi.

Perisic aliachwa kwenye mchezo dhidi ya Torino, ambapo bao la Armando Izzo lilikiwezesha kikosi hicho cha Spalletti kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

"Ni rahisi," alisema Spalletti akinukuliwa na Sky Sport Italia. "Wachezaji wanaweza kusema wanachokitaka, lakini wanamilikiwa na klabu.

"Wamesaini mikataba, na ili kuondoka wanahitaji mtu ambaye atawalipia. Huwezi kuondoka ukiwa huru tu huku ukiwa unalipwa mshahara.

"Kama ambavyo Marotta amesema, hataki kucheza hivyo kwa uhakika kabisa nitamuacha nje ya uwanja. Hilo si tatizo kwangu mimi. Mtu ambaye hatoi mchango kwa timu anatakiwa kuwa nje."

Spalletti alielezea kwamba, kutokuwapo kwa Perisic ndio kulisababisha kubadilisha mfumo wa ushambuliaji ambapo mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Mauro Icardi anacheza pamoja na Lautaro Martinez kwenye safu ya ushambuliaji.

"Nilibadilisha washambuliaji wawili, kwa sababu sikuwa na mawinga," aliongeza. "Perisic hayupo, hivyo na mfumo nao unabadilika.

# SOLSKJAER:

## Yajayo kwa Sanchez yanafurahisha

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatarajia mambo makubwa zaidi kutoka kwa mshambuliaji wa klabu hiyo, Alexis Sánchez ambaye alianza kuwasha cheche dhidi ya Arsenal.

Gazeti la Daily Mail limemnukuu Solskjaer akisema kwamba, Sanchez ameonyesha uwezo mkubwa kuanzia mazoezini tangu alipopewa nafasi ya kuiongoza Man United, na kwamba anaamini mashabiki watafurahia yajayo kutoka kwa mchezaji huyo.

"Sawa, kwa Kiingereza changu kibovu na Kiingereza chake kibovu... unajaribu kukaa naye chini na kuzungumza, lakini ni mchezaji anayechapa kazi, wa kujivunia, na amejikita katika kuonyesha thamani yake," alisema Solskjaer.

"Naamini mashabiki watafurahia zaidi kinachokuja kutoka kwake, amekuwa vizuri tangu mazoezini. Na kiwango chake kimekuwa kizuri zaidi," aliongeza.

Sanchez ambaye alihamia Man United akitokea Arsenal Januari mwaka jana, alifanikiwa kufunga bao la kwanza dhidi ya klabu yake hiyo ya zamani, timu hizo zilipokutana kwenye Kombe la FA Ijumaa iliyopita, ambapo waliwazamisha 'Washika Bunduki' hao wa London 3-1.

Sanchez alikuwa katika wakati mgumu wa kujitibu majeraha na saikolojia kiasi cha kwenda mapumzikoni nyumbani kwao nchini Chile kwa muda, enzi za kocha Jose Mourinho, lakini ameanza kugeuka lulu akiwa na Solskjaer.

Hilo lilikuwa bao lake la pili kwa Man United tangu Machi mwaka jana.





## Arsenal: Koscielny hajavunjika taya

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Laurent Koscielny, hakuvunjika taya kwenye mchezo wa Ijumaa wa Kombe la FA waliofungwa na Manchester United, lakini Sokratis Papastathopoulos atakuwa nje ya dimba hadi mwishoni mwa Februari.

Koscielny alilazimika kupewa huduma ya ziada na uangalifu mkubwa, baada ya kugongana na Romelu Lukaku usoni katika kipindi cha pili cha mchezo huo wa raundi ya nne.

Kocha Unai Emery wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo, alionyesha kuhofia kwamba, Koscielny amevunjika taya, lakini Arsenal imethibitisha kwamba mchezaji huyo wa Ufaransa hakuvunjika taya ila alipata majeraha madogo.

Hakuna muda maalumu uliotajwa ambao beki huyo wa kati atarudi uwanjani, ingawa Gazeti la Ufaransa la L'Equipe limeripoti kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye alikosa nusu ya kwanza ya msimu kutokana na kuumia mguu mwishoni mwa msimu uliopita, bado atahitaji kufanyiwa upasuaji.

Kuumia kwa Koscielny ilikuwa ni mara ya pili kwa Arsenal kupata pigo kwenye mchezo huo wa Ijumaa, kwani beki mwenzake, Sokratis alitolewa baada ya kuumia enka ya mguu wa kushoto katika kipindi cha kwanza.

Emery alionyesha kwamba majeraha ya Sokratis hayakuwa makubwa zaidi, lakini Arsenal hawamtarajii mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund kabla ya mwishoni mwa Februari.

'Washika Bunduki' hao msimu huu wamekumbwa na pigo kubwa, huku Hector Bellerin na Rob Holding wakiwa nje kwa muda mrefu kutokana na majeraha.




# HIGUAIN atakuwa bora zaidi - Zola

**LONDON,** England

GONZALO Higuain atakuwa na mchango mkubwa zaidi kwa Chelsea pale tu atakapoanza kuelewana na wachezaji wenzake, kwa mujibu wa kocha msaidizi, Gianfranco Zola.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina aliwachezea kwa mara ya kwanza 'Blues' hao Jumapili, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Sheffield Wednesday kwenye Kombe la FA raundi ya nne katika Uwanja wa Stamford Bridge.

Higuain alitua hapo kwa mkopo akitokea Juventus Jumatano na alicheza katika mchezo huo ambapo Willian alifunga mara mbili na moja likifungwa na Callum Hudson-Odoi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, angeweza kufunga goli lake la kwanza kwa timu hiyo, baada ya kukataa kupiga penalti ambayo ilipigwa na Willian dakika ya 26 na kuiweka mbele Chelsea.

Olivier Giroud aliingia katika dakika ya 82 kuchukua nafasi ya Higuain, na Zola anaamini kwamba kuna mengi yanakuja kutoka kwa mchezaji huyo.

"Ukimchukwamba angalia kwa namna alivyocheza kwenye mchezo wake wa kwanza, unaweza kuona kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwake," alisema kocha huyo msaidizi akiwaambia waandishi wa habari.

"Katika kipindi cha kwanza alifanya vizuri vikubwa, lakini hakuweza kupata nafasi ya kufunga.

"Kama binadamu nimeridhika kabisa na kiwango chake, lakini atakuwa bora zaidi na anahitajika kujiimarisha zaidi kuweza kuelewana na wachezaji wenzake.

"Kuna wakati kipindi cha kwanza alifanya vitu vizuri, lakini huwezi kuviona kwa haraka."

## Van Persie atupia mawili Feyenoord ikiipiga 6 Ajax

**ASMTERDAM,** Uholanzi

ROBIN van Persie amepaza sauti kusifia morali iliyoonyeshwa na Feyenoord wakati wakipigana kuibuka na ushindi wa 6-2 dhidi ya Ajax ambao ni wapinzani wao wakuu kwenye soka la Uholanzi, juzi Jumapili.

Akiwa amefanya kazi ya ziada ya kusaidia kupatikana kwa mabao mawili ya kwanza ya Feyenoord, Van Persie alifunga mara mbili, huku Tonny Vilhena na Yassin Ayoub kila mmoja akifunga moja.

Mara baada ya mchezo huo Van Persie, alisisitiza kwamba morali ya wachezaji wa Feyenoord ilikuwa juu zaidi na kuweza kufunga mabao hayo sita dhidi ya Ajax ikiwa ni mara ya kwanza tangu Novemba mwaka 1964.

"Ilihamasisha," alisema Van Persie, ambaye ameonekana kurudi kwenye kiwango chake hivi sasa.

"Mchezo huu ulikuwa na kila kitu. Magoli, soka zuri, hamasa, kupambana kwa nguvu. Najisikia fahari kwa namna tulivyopambana kupata matokeo haya.

"Kila mmoja uwanjani alipigania matokeo. Morali yetu ilikuwa juu zaidi.

"Wakati tulipokuwa mbele kwa 3-2, niliangalia nyuma na kuona kwamba kuna kitu kizuri zaidi kinakuja. Kwa uhakika tulicheza kwa umakini mzuri na kufanikisha kupata ushindi huu mtamu.

"Nawaamini wachezaji hawa. Wanaweza kucheza vizuri. Tulicheza kwa umakini na utulivu mkubwa zaidi."

Lasse Schone alifungia Ajax bao la kuongoza dakika ya nane, lakini mabao ya Jens Toornstra na Steven Berghuis yakaiweka mbele Feyenoord katika kipindi cha kwanza.



## HABARI MICHEZO

### KWA UFUPI

**ARSENAL KUMNASA MALCOM**
ARSENAL bado ina matumaini ya kukamilisha dili la kumsajili winga wa Barcelona, Mbrazil Malcom, 21, kabla ya dirisha dogo kufungwa Alhamisi saa sita usiku. **(Sun)**

**GIROUD KURUDI UFARANSA**
STRAIKA wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, 32, amesema anaweza kurudi kucheza nyumbani baada ya 'Blues' kumsajili nyota wa kimataifa wa Argentina, Gonzalo Higuain kwa mkopo kutoka Juventus. **(Goal)**

**RABIOT AITAKA LIVERPOOL**
KIUNGO wa Paris St-Germain, Mfaransa Adrien Rabiot, 23, ameikataa Tottenham kwa sababu anataka kujiunga na Liverpool. **(Sun)**

**BOLASIE AWINDWA NEWCASTLE**
WINGA wa Everton na DR Congo, Yannick Bolasie, 29, ameiambia klabu hiyo anataka kuondoka kwa mkopo na kujiunga na klabu nyingine ya Ligi Kuu England baada ya kukatisha kukaa kwake kwa muda Aston Villa. Newcastle, Burnley na Cardiff zinamtolea macho mchezaji huyo. **(Mirror)**

**PSG YAKWAMA KWA GUEYE**
PARIS St-Germain imetoa ofa ya pauni milioni 21.5 kwa kiungo wa Everton, Idrissa Gueye, 29, lakini 'Toffees' hao wamesema Msenegal huyo hauzwi. **(Sky Sports)**

**SOUTHAMPTON YAMFUATA ADAMS**
SOUTHAMPTON imetoa ofa ya pauni milioni nane kwa mshambuliaji wa Birmingham, Che Adams, 22, wakati huu Muingereza huyo akitazamwa na klabu 12 za Ligi Kuu England. **(Mirror)**

**CITY YAKOMAA NA PALAVERSA**
MANCHESTER City imefanya mazungumzo zaidi kuhusu kutoa pauni milioni 5.5 ili kuipata huduma ya kiungo wa Hajduk Split, Mcroatia Ante Palaversa, 18. **(Mail)**

**LIVER, TONALI WATETA**
LIVERPOOL imefungua mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Brescia, Mtaliano Sandro Tonali, 18. **(La Gazzetta dello Sport via Express)**

**TUCHEL AKOMALIA USAJILI PSG**
KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel amewataka mabingwa hao wa Ligue 1, kuharakisha kusajili mchezaji mpya kabla ya dirisha dogo kufungwa Alhamisi saa sita usiku. Miamba hiyo ya Ufaransa inavutiwa na kiungo wa Napoli, Mbrazil Allan, 29. **(Goal)**

**SILVA KUONDOKA LEICESTER**
KIUNGO wa Leicester na Ureno, Adrien Silva, 29, anataka kuachana na klabu hiyo kabla ya dirisha dogo kufungwa Alhamisi wiki hii baada ya kutoanzishwa katika mechi za Ligi Kuu tangu kufunguliwa kwa msimu. **(Guardian)**

**DEULOFEU DADO LULU MILAN**
AC Milan bado ipo tayari kumsajili winga wa Watford, Mhispania Gerard Deulofeu, 24. **(Di Marzio)**

**WOODBURN KUPELEKWA HULL**
MSHAMBULIAJI raia wa Wales, Ben Woodburn, 19, ambaye ni mfungaji kinda zaidi katika historia ya Liverpool, anaweza kujiunga na Hull City kwa mkopo baada ya kurejea akitokea Sheffield United. **(Mail)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR VIGUMU KUIVAA MAN UTD

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR inawezekana akaikosa Manchester United wakati Paris Saint-Germain itakaposafiri kwenda Old Trafford kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi ujao, kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Thomas Tuchel.

Mabingwa hao wa Ligue 1, wametangaza kuwa mchezaji huyo ghali zaidi duniani anasumbuliwa na "maumivu" katika majeraha aliyoyapata kwenye mguu wake wa kulia alioumia awali msimu uliopita baada ya kuutonesha wakati wakishinda 2-0 wiki iliyopita kwenye Kombe la Ufaransa dhidi ya Strasbourg.

PSG ilirejea uwanjani kwenye mechi ya Ligue 1 Jumapili bila ya nyota huyo na kuichapa Rennes mabao 4-1 wakati Edinson Cavani akitupia mawili.

Wakati mechi ikiwa inachezwa, RMC Sport iliripoti kuwa Neymar hatakuwa fiti kucheza mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-Bora utakaopigwa Old Trafford Februari 12, mwaka huu.

Akizungumza kupitia Canal Plus baada ya mechi, Tuchel alikiri kuwa inawezekana ikawa hivyo.

"Itakuwa vigumu sana," alisema.

"Kama nilivyoeleza [Jumapili], ni mapema mmno kuzungumza kuhusu tarehe ya kurejea. Tunapaswa kusubiri kwa wiki ya kwanza, kitu ambacho ni muhimu sana, na majibu ya matibabu yake.

"Baada ya hapo tu, tunaweza kuwa sahihi zaidi. Lakini itakuwa vigumu sana hiyo si siri."

Wakati ukiwa na mchezaji kama Cavani na mfungaji mwenza mwishoni mwa wiki, Angel Di Maria na Kylian Mbappe wanaweza kutumika vyakutosha kubeba jukumu la Neymar, hata hivyo kikosi cha Tuchel si kipana sana katika eneo la kiungo wa kati.

Marco Verratti hatakuwapo kutokana na kuwa majeruhi na Adrien Rabiot ameenguliwa katika kikosi cha kwanza kutokana na kutaka kuondoka, hivyo kuwaacha mabeki Wabrazil Marquinhos na Dani Alves wakijenga ukuta wa kati dhidi ya Rennes.

Hiyo inaifanya PSG kuelekeza mpango wake katika kumsajili Leandro Paredes kutoka Zenit, ingawa Tuchel amesema dili hili halikufanyika mwishoni mwa wiki kama ilivyokuwa inatarajiwa.

"Tayari nilikuwa nikimtarajia kwa siku chache, lakini hayupo hapa," alisema.

"Nimekuwa nikitazama bafuni, katika chumba kubadilishia, katika chumba cha matibabu, na makipa, lakini hayupo hapa."

HABARI MICHEZO

# KIPA WA BANDARI AITAMANI YANGA

**Na Faustine Feliciane**

GOLIKIPA wa Bandari FC ya Kenya, Farouk Shikalo, amesema yupo tayari kujiunga na timu yoyote ya Tanzania kama makubaliano ya pande tatu yatafikiwa.

Farouk alikuwa akitajwa kutaka kujiunga na Yanga katika dirisha dogo la usajili huku kocha wa timu hiyo, Mwinyi Zahera akitajwa kumkubali kipa huyo ili aweze kurithi mikoba ya Beno Kakolanya.

**Hata hivyo, viongozi wa Yanga walishindwa kukamilisha usajili wa mlinda mlango huyo kwa wakati na kulazimika kumtumia Claus Kindoki.**

Akizungumza na Nipashe juzi, Shikalo ambaye alikuwa nchini na timu yake kwa ajili ya kushiriki michuano ya SportPesa iliyomalizika juzi, alisema kuwa hana tatizo kuja kucheza katika Ligi Kuu Tanzania Bara kama watafikia makubaliano.

Shikalo alisema kuwa anaifahamu Ligi ya Tanzania Bara na anajua kwamba ina ushindani hivyo hana hofu na ubora wake.

Kipa huyo ameisaidia timu yake kufika hatua ya fainali ya michuano ya Sportpesa kabla ya kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Kariobang Sharks waliotwaa ubingwa huo kwa mara ya kwanza.




Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga, akimkabidhi kombe nahodha wa timu ya Kariobangi Sharks ya Kenya, Patila Omoto, baada ya kuibuka washindi kwa kuwachapa ndugu zao, Bandari FC kwa bao 1-0 katika mechi ya fainali ya michuano ya SportPesa iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Mwenye shati la bluu nyuma ni Rais wa TFF, Wallace Karia. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Serikali, wadau kuibeba Taasisi ya Haji Manara

**Na Somoe Ng'itu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, juzi usiku aliwaongoza wasanii, viongozi wa dini, klabu za soka na wadau mbalimbali kununua manukato kwa ajili ya kuchangia fedha zitakazokwenda katika Taasisi ya Haji Manara (Haji Manara Foundation) ambayo ilizinduliwa rasmi siku hiyo.

Mbali na kuzindua taasisi hiyo, Haji Manara, ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, alitambulisha manukato yake ambayo yatajulikana kwa jina la De la Boss na yataanza kuuzwa katika maduka mbalimbali hapa nchini.

Sehemu ya fedha zitakazopatikana katika mauzo ya bidhaa hiyo, zitakwenda kwenye taasisi hiyo ambayo lengo lake kuu ni kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na watu wenye ulemavu wa ngozi, ambapo Manara ni mmoja wa kundi hilo.

Makonda alisema atanunua manukato yenye thamani ya Sh. 100,000 kwa kutoa Sh. milioni tano na kuongeza kiasi kama hicho kwa ajili ya kumnunulia Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakary Zubeiry Ally na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo.

"Nitanunua yangu kwa Sh. milioni tano na nitamnunulia Askofu Pengo na Mufti (Abubakary), hivyo nitatoa Sh. milioni 10, msiniulize nitatoa wapi," alisema Makonda.

Watu wengine waliochangia katika harambee hiyo ni pamoja na aliyekuwa Kaimu Rais wa Simba, Salim Abdallah alitoa Sh. milioni tano.

Alisema kuwa anawapongeza wazazi wa Haji kwa kukubali kumlea, kumtunza na kukabiliana na changamoto mbalimbali kutoka katika jamii iliyokuwa inawazunguka.

Naye mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde alisema kuwa Serikali imejipanga kuendelea kutoa elimu kwa ajili ya kuwaongezea wananchi uelewa wa kutosha kuhusu watu wenye ulemavu, kwa sababu wao pia wana mchango katika maendeleo ya nchi.

Mavunde alisema kuwa serikali inamtakia kila la kheri katika taasisi yake na inaahidi kumpa ushirikiano huku ikiahidi itaendelea kuboresha huduma kwa kuwapatia vifaa saidizi.

Alisema pia serikali imeandaa mwongozo wa elimu wa kusaidia watu wote wenye ulemavu huku ikiweka kitengo maalumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Manara pamoja na wazazi wake waliwashukuru wadau wote waliojitokeza kuunga mkono taasisi yake, lakini shukrani za pekee zikienda kwa Kampuni ya Asas ambayo Manara ni balozi wao.

## Mwalala -Nilifurahi kuwakabili Simba

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Bandari FC ya Kenya, Ben Mwalala, amesema alijisikia furaha baada ya kuona wanakutana na Simba katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya SportPesa iliyomalizika juzi jijini Dar es Salaam.

Bandari ilikutana na Simba katika hatua hiyo na kuwashangaza mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwafunga mabao 2-1.

Mwalala, alisema alijua Simba ingewapa uzoefu wachezaji wake ambao wengi ni vijana na bado hawana uzoefu na michuano ya kimataifa.

"Simba ni timu kubwa na kwa sasa inacheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kukutana nao ilikuwa furaha kwetu kwa sababu timu yangu inaundwa na vijana wengi hivyo nilijua wangepata uzoefu, ilikuwa vizuri sana," alisema Mwalala, mshambuliaji wa zamani wa Yanga.

Alisema kufungwa katika mchezo wa fainali na wapinzani wao kwenye Ligi Kuu Kenya, Kariobang Sharks ni matokeo tu ya mpira lakini vijana wake walijitahidi kupambana.

"Hatukupewa nafasi ya kufika mbali, tulipokuja hapa hasa kutokana na kuwapo kwa timu kubwa na Simba, Yanga na Gor Mahia, lakini wachezaji wangu walipambana mpaka tumecheza fainali, nawapongeza sana," Mwalala alisema.

Aliongeza kuwa wanarejea Kenya kuendelea na ligi yao wakiwa wameimarika na anaamini watendelea kupata matokeo mazuri.

## FA Zanzibar kuanza J'mosi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Soka Zanzibar (ZFA) kimesema kuwa mashindano ya Kombe la FA ( FA CUP) mwaka huu yamepangwa kufanyika kuanzia Jumamosi kwenye viwanja sita tofauti Kisiwani Unguja.

Michuano hiyo inatarajia kushirikisha timu 22 za Daraja la Pili Taifa, timu 16 za Draja la Kwanza Kanda ya Unguja, timu 10 za Ligi Kuu Zanzibar ambazo zipo Unguja pamoja na timu nne za mabingwa wa Wilaya za Unguja .

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Ufundi wa ZFA, Salum Ali Haji alisema michuano hiyo itachezwa kwa mfumo wa mtoano.

Haji alivitaja viwanja hivyo ambavyo vitatumika katika michuano hiyo kuwa ni pamoja na Maungani, Bungi, Amaan, Misuka, White Bird na Mchangani.

Kiongozi huyo alizitaja baadhi ya timu zitakazochuana kuwania kombe hilo ni Bweleo, Mfenesini, Dulla Boys, Mhaonda Kids, New King, Ujamaa, White Bird, Charawe, Gulioni, Sebuleni, Mchangani Star, Raskazone, Kimbunga, Villa FC, Polisi Bridge, Mundu, Idumu, Ngome, Black Mamba, Wemba, Kilimani City, Kijichi, Mpapa, Kwerekwe City na Negro.

Timu nyingine ni pamoja na Kizimkazi, Super Tiger, Mwembeladu, Mchangani United, Sharb Boys, Kundemba, Uhamiaji, Zantex, African Coast, Taifa Jang'ombe Boys, Kijanja, Shangani, Maungani, New boys na Kitope.

Michezo
Jumanne Januari 29, 2019
Nipashe

## Neymar vigumu kuivaa Man Utd



HABARI UK. 30

TULIA...




Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa Lazio, Bartolomeu Jacinto Quissanga 'Bastos' (kulia), kwenye mechi ya Serie A iliyopigwa katika Uwanja wa Stadio Olimpico juzi. Juve ilishinda 2-1, bao la pili likifungwa na Ronaldo kwa mkwaju wa penalti. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga, Biashara zatunishiana misuli

**Na Mwandishi Wetu**

INAWEZEKANA! Kocha Mkuu wa Biashara United, Amri Saidi, amesema timu yake imejiandaa kusaka ushindi na kuwataka Yanga wajiandae kisaikolojia kupokea matokeo yoyote baada ya dakika 90 za mchezo dhidi yao utakapomalizika.

Yanga inatarajia kuwakaribisha Biashara United katika mechi ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Saidi, alisema tayari amesharekebisha makosa yaliyojitokeza katika mchezo wao uliopita dhidi ya Azam FC na sasa wataingia uwanjani wakiwa makini kwa lengo la kusaka ushindi.

Kocha huyo alisema mechi zote ni ngumu, lakini za mfumo wa mtoano huwa ngumu zaidi kwa sababu kila upande unaogopa kuondolewa katika mashindano.

"Tunaijua Yanga, tumejiandaa kufanya vizuri, tunawaheshimu na tunaingia uwanjani tukiwa tumejipanga zaidi, kikubwa ni wachezaji wangu kufuata maelekezo niliyowapa," alisema kwa kifupi kocha huyo wa zamani wa Lipuli FC ya Iringa na Mbao FC ya jijini Mwanza.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wa timu hiyo wanaendelea vizuri na mazoezi huku wakijipanga kushinda mechi hiyo na kusonga mbele.

"Tunahitaji kusonga mbele na hasa kushinda kombe hili, litatusaidia kujenga heshimu yetu kwa msimu huu," alisema meneja huyo.

Mtibwa Sugar ndio bingwa mtetezi wa michuano hiyo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# SIMBA 20 WAIFUATA AL AHLY KWA HASIRA

### ●●● Meneja atangulia, kikosi na viongozi kufuata leo, mechi kupigwa saa nne usiku huku...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha wachezaji 20 Simba kikitarajia kuondoka nchini leo jioni kuelekea Misri kuwafuata Al Ahly katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, meneja mpya wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, amesema atahakikisha kila kitu kinakwenda sawa ndani ya timu hiyo ambayo pia inajukumu la kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Al Ahly wanatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya raundi ya tatu ya Kundi D itakayochezwa mjini Alexandria, Misri Jumamosi kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Kauli hiyo ya Rweyemamu imekuja siku chache baada ya baadhi ya wachezaji nyota wa timu hiyo kudaiwa kwenda kula "bata" huku wakikabiliwa na mchezo wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya SportPesa ambao walifungwa na Bandari FC ya Kenya mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rweyemamu alisema tayari ameshaanza rasmi kazi katika klabu hiyo na jana alitangulia Cairo kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuipokea timu yao.

Rweyemamu alisema anafahamu vema majukumu ya meneja, na anaamini hatawaangusha viongozi waliompa dhamana ya cheo hicho.

"Ulikuwa ni mchakato, niliitwa nikahojiwa na taratibu nyingine za kazi zilifanyika, lakini kwa kifupi nimeanza kazi leo (jana) na hapa naelekea Uwanja wa Ndege kwa ajili ya safari ya kwenda Misri," alisema Rweyemamu ambaye aliwahi kuwa meneja wa timu ya vijana ya klabu hiyo maarufu Simba B.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema jana kuwa msafara wa kuelekea Misri utakuwa na wachezaji 20 pamoja na viongozi wengine wa benchi la ufundi kwa ajili ya mechi hiyo ya tatu.

"Uongozi wa Klabu ya Simba katika kuongeza ufanisi wa timu, umemteua, Patrick Rweyemamu kuwa meneja wa muda, huku Abbas Ally akiendelea na majukumu yake ya awali ya mratibu wa timu," alisema Manara katika taarifa yake.

Rweyemamu ameteuliwa kurithi mikoba iliyoachwa na Richard Robert ambaye alisimamishwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kile kilichoelezwa kuihujumu Timu ya Taifa "Taifa Stars".

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >